**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi - Tarehe 22 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Hotuba ya Waziri ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. CHRISTOWAJA M. MTINDA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 76

**Manufaa ya Uwekezaji kwa Taifa**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Uwekezaji katika sekta mbalimbali ni njia mojawapo ya kulipatia Taifa mapato:-

(a) Je, nchi yetu imenufaika kiasi gani na uwekezaji?

(b) Je, ni wawekezaji wa sekta ipi walioleta matumaini makubwa kwa Watanzania?

(c) Je, kuna uwekezaji wowote waliowahi kupewa vikwazo vya uwekezaji hapa nchini?

**WAZIRI WA NCHI,OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nchi yetu imenufaika kwa uwekezaji wa ndani na nje kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kuongea upatikanaji wa mitaji, ujuzi na teknolojia mpya na ya kisasa, kuongeza fursa za ajira, fursa za masoko ya nje ya nchi kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini, idadi ya watalii kutoka nje, mapato ya fedha za kigeni, mapato ya Serikali kutokana na makusanyo ya kodi ushuru na mrahaba na hivyo kuongeza kukua kwa uchumi.

Mathalani mitaji kutoka nje, iliongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 520 mwaka 2005 hadi dola za Marekani bilioni 1.1 mwaka 2011. Uwekezaji pia umetuwezesha kuongeza ujuzi wa wataalam Wazalendo kukuza uwezo wa uendeshaji na menejimenti ya miradi mikubwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Nchi yetu pia imenufaika na uwekezaji kutokana na kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa hapa nchini na hivyo kuongeza ushindani wa bidhaa zetu katika soko na kukuza biashara ya ndani na nje. Hivyo, uwekezaji ni njia ya uhakika ya kuiwezesha nchi yetu kunufaika na rasilimali mbali mbali zilizopo nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 200/ 2012 kituo cha uwekezaji Tanzania kimesajili jumla ya miradi 7,012 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 60 iliyotoa fursa za ajira kwa Watanzania 1,029,737.

Sekta ya viwanda iliongoza kwa kuwa na miradi mingi zaidi ambapo jumla ya miradi 2,095 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 9,776.06 iliyotoa fursa za ajira 229,269 kwa Watanzania ilisajiliwa kwenye sekta hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuvutia uwekezaji wenye tija kutoka ndani na nje kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC).* Serikali imeanzisha kituo cha utoaji wa huduma kwa pamoja kwenye kituo hicho ili kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali na kuondoa vikwazo vyovyote katika uwekezaji.

Hadi sasa hakuna taarifa zinazoonyesha kwamba kuna wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza hapa nchini na kuwekewa vikwazo bila sababu za msingi. Aidha, Serikali inatekeleza mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini kwa nia ya kuondoa urasimu usio wa lazima na vikwazo kwa wawekezaji.

**MHE.KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayajaniridhisha ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a)Mheshimiwa Spika, Mwekezaji Mzalendo Said Salim Bakhresa alitaka kuwekeza katika sekta ya kilimo Mkoa wa Rukwa Wilaya ya Katavi, lakini mpaka leo hajapatiwa kibali cha kuwekeza katika sekta hiyo tukijua kuwa sekta hii inawasaidia vijana wengi katika kuwapatia ajira.

Je, ni kwa nini Mheshimiwa Waziri anasema kuwa hakuna pingamizi?

(b) Mheshimiwa Spika, inasemakana kuwa katika kuwekeza au wawekezaji kutoka nje wanafanyiwa urasimu wanapokuja nchini kutaka kuwekeza na hatimaye kupelekea kwenda kuwekeza nchi nyingine na wanaonufaika ni watu wa nchi nyingine. Ni kwa nini Serikali yetu haiweki mikakati ya msingi katika kuwapatia wawekezaji kuwekeza katika nchi yetu?

**SPIKA:** Ninaamini kuwa ile ya Bakhresa ulitoa kama mfano sidhani kama umekuja kumtetea Bakhresa hapa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kujibu swali na nimelijibu kwa ukweli sasa kama kwa ajili ya Ndugu Bakhresa Mheshimiwa Mbunge hajaridhika, ninasikitika lakini ninafurahi sana kwamba ametupa taarifa hiyo tutaifanyia kazi.

Lakini vilevile Said Salim Bakhresa na kampuni yake ni moja ya kampuni ambayo inashirikiana sana na sisi na tumeiwezesha mambo mengi na yeye ameinufaisha nchi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, hiyo ya Rukwa tutafuatilia na nina uhakika kuwa angekuja ofisini na angeenda *TIC* badala ya kwenda kwa Mbunge nina hakika kuwa tungeshughulikia uwekezaji wake haraka sana. *(Makofi)*

Mimi ninashukuru sana Watanzania walio wengi walikuwa na wasiwasi sana kwa uwekezaji ndani ya nchi kutoka nje, lakini kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Kombo nimeshukuru sasa kuona mambo yanabadilika na wote tunatetea uwekezaji kutoka nje lakini tuhakikishe kuwa nchi yetu inanufaika na uwekezaji huo.

Kwa hiyo, tumeiweka *TIC* ili kuondoa urasimu. Ninajua kuwa bado kuna changamoto ninataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba *TIC* pamoja na Serikali na Watanzania wote tujitahidi sana kuwasaidia wawekezaji ambao watanufaisha nchi yetu na kuwapiga vita wale ambao wamekuja kuvuna bila sisi kunufaika. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuiuliza Serikali kuwa kwa kipindi cha miaka zaidi ya 20 sasa Serikali imekuwa inatoa *incentives* kwa makampuni yanayowekeza nchini.

Je, Serikali inatambua kuwa makampuni haya yanakuwa hayana mitaji lakini zile *incentives* ambazo tunawapa ndizo wanazotumia kama mitaji na kuwaumiza wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, mitaji ni moja kati ya mambo ambayo tunavutia kutoka nje lakini pamoja na mitaji kama nivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni pamoja na teknolojia, ni pamoja na kutusaidia kupata masoko kwa ajili ya bidhaa

zetu lakini mitaji bado inabakia kuwa ni muhimu sana kwa sababu kama tuna tatizo humu ndani zaidi ya elimu na mambo mengine hatuna mitaji kwa sababu uwekaji wetu wa akiba bado ni mdogo sana. Kwa hiyo, ninazingatia maoni ya Mbunge kuwa tutaangalia zaidi mitaji lakini bila kusahau maeneo mengine muhimu katika uwekezaji.

Kuhusu vivutio ambavyo tunawapa, tunawapa vivutio ambavyo havipunguzi mitaji. Kwa mfano mtu anapokuja na *Capital Goods,* vile vitu ambavyo vinatakiwa katika kuwekeza ukitoza kodi pale maana yake unapunguza uwekezaji hata sisi wenyewe tunajinyima manufaa. Tunaangalia sana suala hili la vivutio tutaona kuwa vivutio vinavyotolewa ni vile ambavyo vinatupa manufaa na siyo wawekezaji wenyewe. *(Makofi)*

**MHE. HANRY D. SHEKIFU**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ninaamini uwekezaji mzuri kwa sasa ni katika kilimo, lakini eneo hili la kilimo limegubikwa na migogoro ya ardhi na kuna wawekezaji wamechukua maeneo lakini hawayaendelezi kama vile Mnazi katika Mkoa wa Tanga. Serikali inachukua hatua gani hasa hawa wakulima ambao wamewekeza katika kilimo lakini hawafuati masharti ya kuwekeza?

**WAZIRI WA NCHI,OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa nchi nzima na Serikali kwa pamoja tunavutia sana uwekezaji katika eneo hili la kilimo kwa sababu ndilo litatusaidia sana kuleta maisha bora na kuondoa umasikini Tanzania.

Lakini ni kweli kuwa suala la ardhi ni changamoto kubwa kwa jinsi ambavyo ninakumbuka Sheria ya ardhi yenyewe imetuelekeza ni nini kifanyike kama mtu akipewa ardhi na haitumii.

Katika miaka mitatu pengine miaka mitatu ni michache sana lakini hili suala la ardhi ni lazima tulifuatilie kwa sababu bila kuondoa mgogoro kwenye ardhi hata uwekezaji kwenye Kilimo utakuwa na Mgogoro.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana kupitia Kilimo Kwanza na hasa sehemu ya *SAGOT* kuona kuwa maeneo tunayoainisha ili wawekezaji wanapokuja wasikutane na migogoro hiyo. Lakini jambo lingine ambalo ningependa kuwakumbusha wawekezaji wa ndani na wa nje ni vizuri wakapitia njia rasmi badala ya kupitia njia zingine ambazo zinaleta migogoro mikubwa zaidi.

Na. 77

**Kuvipatia Maji Vijiji vya Mbeya Vijijini**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Bomba linalopeleka Maji kwenye Uwanja wa Ndege wa Songwe linapita kwenye Vijiji vya Nsalala, Ikumbi na Mwashiwawala ambavyo havina Maji.

(a) Je, ni sahihi Serikali kuwanyima wananch hao maji wakati yanapita kwenye maeneo yao?

(b) Je, Serikali iko tayari sasa kuwapatia Maji wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Lackson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa bomba linalopeleka maji katika Uwanja wa Ndege wa Songwe linapita katika Vijiji vya Nsalala, Ikumbi na Mwashiwawala. Bomba hili limelazwa kuanzia mwezi Novemba 2012 na kukamilika Februari, 2013 likiwa na kipenyo cha milimita 150 na urefu wa kilomita 13.9.

Bomba hilo linachukua maji kutoka katika mradi wa Maji wa Jiji la Mbeya kwenye tanki la hifadhi maji lenye ujazo wa lita milioni 2.5 katika mlima wa Iwambi. Mradi huu umegharimu jumla ya shilingi milioni 605.0 ambazo zimetolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maji kwa wakazi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe ni mita za ujazo 200 kwa siku, lakini mradi una uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 500 kwa siku. Hivyo, ipo ziada ya maji sawa na mita za ujazo 300. Serikali imeazimia ziada hiyo kupeleka huduma za maji kwa wakazi wa Vijiji vya Nsalala, Ikumbi na Mwashiwalala ambavyo vinapitiwa na bomba hilo.

Mabomba yatajengwa kutoka katika bomba kuu linalopeleka maji Uwanja wa Ndege wa Songwe kwenda katika vijiji hivyo ambavyo havina huduma ya maji inayotosheleza mahitaji. Aidha, vituo vya kuchotea maji (Vilula) vitajengwa katika Vijiji hivyo ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

Hivyo, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wa Vijiji vya Ikumbi, Nsalala na Mwashiwawala wananufaika na huduma ya maji ya bomba kutoka Iwambi bila ubaguzi wowote hasa kwa kuzingatia matatizo ya maji yaliyopo katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini yamekuwa ya ujumla mno *too ambiguous* kwasababu sijajua ni lini kazi hiyo itaanza, ninaomba Serikali inijibu ili wananchi wale waweze kupata matumaini kuwa ni lini kazi hiyo ya kuwapelekea maji wananchi hao itafanyika au itaanza.

**NAIBU WAZIRI,OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hapa mimi nina Bajeti ya hivyo Vilula tunavyovizungumzia hili jina linalonishinda kutamka hapo Mwashiwalala tumelipangia

milioni 1.6, Ikumbi na vijiji vingine tumeweka milioni 1.2 na hii ninazungumzia kuhusu suala la Vilula na Mjii huu unaozungumzwa hapa ni ule Mji wa Mbalinzi ambao uko pembeni ambao unakua kwa haraka sana na Professor atakaposimama hapa wakati atakapokuwa analeta hii hoja yake ya Maji atakuwa anazungumzia hili. Lakini hili liko ndani ya uwezo wetu kwa sababu tume- *check* naye na anasema hakuna madhara yoyote yatakayotokea katika Kiwanja hiki cha Songwe.

Ninataka kumthibitia Mheshimiwa kuwa kazi hii ya shilingi milioni 4 hivi ni kazi ya kukaa na kuanza kufikiria itakuwa ni lini! Hili ni suala la kwamba Bajeti hii ikishapita maana yake ni kuwa kazi hii itafanyika.

**MHE.DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, mwaka jana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua mradi mkubwa sana wa maji eneo la Nzovwe katika Jiji la Mbeya lakini ajabu ni kuwa mpaka leo hii wakazi wa Jiji la Mbeya wanapata shida ya maji na bili za maji zinapokuja zinakuwa ni za kiwango cha juu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu, ninashukuru.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi mkubwa wa maji Mjini Mbeya ulikamilika na kufunguliwa mwaka jana na kulikuwa na matumaini makubwa kwamba asilimia 95.5 ya watu wa Mbeya watapata maji kutokana na uzalishaji wa mradi ule.

Kumekuwa na matatizo madogo ya kiufundi katika maeneo mbalimbali ambayo yanashughulikiwa sasa na mamlaka ya maji safi na uondoaji wa majitaka Mjini Mbeya na sitegemei kwamba tatizo hili litaendelea. *(Makofi)*

Na. 78

**Kusambaza Umeme kwa Maeneo Mengi ya Kibiti**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. ABDUL J. MAROMBWA)** aliuliza:-

Umeme katika Miji ya Kibiti, Bungu na Mchukwi umesambazwa katika maeneo machache sana:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme kwa wateja wengi zaidi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme Vijiji vya Kinyanya, Mtwawanya na Pagai ambavyo vimepitiwa na nguzo za umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia wakala wa Nishati Vijijini, ina mpango wa kutekeleza miradi miwili ya umeme katika Wilaya ya Rufiji, miradi hiyo ni:-

(i) Mradi Kabambe wa Awamu II *(Turnkey Phase II)* ambao utahusisha maeneo ya Mpima, Mbunju, Ruwe, Mkongo, Kilimani, Ngorongo, Ndundunyikanza, Kipo, Kipugila, Nyaminywili, Mtanza, Msona, Miguu Saba, Mwasemi, Mloka, Nyamwage, Nambunjo Sekondari, Mbwara, Nyamisati na Jaribu Mpakani; na

(ii) Mradi wa Msongo mdogo *(Underline Distribution Transformer),* mradi huu unatekelezwa katika maeneo ambayo umepita umeme wa Msongo Mkubwa *(High Voltage)* na utahusisha maeneo ya Pagai, Malendegu, Mtawanya A, Mtawanya B na Kijiji cha Kiwanga.

Mheshimiwa Spika, Zabuni za miradi hii zilifunguliwa mwezi Machi, 2013, ambapo mchakato wa kuwapata wakandarasi uko katika hatua za mwisho. Makadirio ya gharama ya miradi hii ni shilingi bilioni 1.3. Miradi hii itaanza kutekelezwa wakati wowote ndani ya mwaka huu wa 2013. Aidha, Serikali itaandaa mpango mwingine wa kupeleka umeme katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge lakini hayapo katika orodha ya utekelezaji wa sasa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yanayowiana ya Waziri lakini ningependa nimwulize maswali mengi ya nyongeza kama ifuatavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ni maswali mawili tu siyo mengi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika sana. Kwanza Katika swali la msingi la Mheshimiwa Marombwa alitaka kujua pia na Kijiji cha Kinyanya, pamoja na Mchukwi. Katika majibu yako hukuainisha hivi vijiji. Kwa hiyo, ningependa kujua katika utekelezaji huu Mchukwi na Kinyanya ambapo kuna hospitali kubwa pale ni lini vitakuwa vimeingizwa katika mpango huo na utekelezaji wa mpango huu mzima utakamilika lini?

Umeme unaozalishwa Somanga Fungu ndiyo ambao unafika mpaka maeneo haya ya Rufiji. Kumekuwa na tatizo la ukatikaji wa umeme kama wiki mbili zilizopita karibu siku kumi na tano umeme ulikuwa haupatikani na ukirudi unakatika kila baada ya dakika tano, hii inatokana na *incompetence* ya watalaam ambao wanasimamia mitambo.

Ni lini Serikali itazingatia maelekezo yaliyotolewa na aliyefunga mitambo hii *REMCO* na kuweka utalaam wa kutosha ili kuzalisha umeme na uwe wa uhakika kwa wananchi wa Rufiji na Kilwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, nilisema vijiji ambavyo havikutajwa hapa vitawekwa katika mpango unaokuja baada ya *phase II* ya *REA* kukamilika na mpango huu utafuatia na utakuwepo wakati wowote baada ya kukamilisha mpango ule wa mwanzo wa awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili ni kwamba Somanga Fungu kuna tatizo. Ni kweli umeme umekatika kwa takribani siku zaidi ya kumi na tatizo ni hili alilosema Mbunge kwamba mitambo imekuwa ikisumbua. Lakini tatizo hilo limesharekebishwa na hatua nyingine kwa maoni yake ambayo anayasema tutazingatia.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni muhimu sana katika maendeleo vijijini na hasa katika shule za sekondari za Kata. Kutoka Karatu kwenda Sekondari ya Florian, Endamarieki waliweka umeme na kuweka nguzo na wananchi walisadia lakini kazi hiyo imesimama, naomba kujua kutoka kwa Waziri hiyo kazi itakamilika lini?

**SPIKA:** Hili ni swali lingine, mimi nilifikiri kwamba Serikali ina mpango gani wa kuweka umeme kwa sehemu kama Sekondari na nini, hilo ndilo lingekuwa swali lenyewe. Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ujumbe aliotaka kuusema Mheshimiwa Natse ni mpango gani upo katika kuweka umeme kwenye shule za Sekondari. Mimi nadhani nijibu kwa ujumla wake.

Ni kweli kwamba umeme utakuwa na tija pale ambapo unaenda katika huduma za kijamii, pale ambapo unaenda kwenye maeneo ya uzalishaji.

Kwa hivyo, sisi katika utaratibu wa sasa, Serikali tumeamua kwamba umeme ukifika kwenye Kijiji ni lazima uende kwenye zahanati, ni lazima uende kwenye sekondari ni lazima uende kwenye shule ya msingi, ni lazima uende kwenye visima vya maji na sehemu yeyote ambapo pana huduma za kijamii au za uzalishaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilufi usije ukauliza yanayohusu Jimboni kwako, uliza ya kisera.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina uzalishaji wa mazao mbalimbali ambayo yanahitaji kusindikwa na pengine kukobolewa kwa mitambo mikubwa, lakini kwa bahati mbaya sana haijaingizwa kwenye mpango wa huduma ya umeme vijijini.

Nataka kujua ni lini Wilaya ya Mbarali itaingizwa kwenye mpango ili ahadi ya Rais ya kupeleka umeme Madibira iweze kutimia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, bado siyo swali zuri la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika majibu ya swali lililotangulia, kwamba umeme unapokwenda vijijini ikiwepo pamoja na Mbarari ni lazima uweze kwenda kwenye maeneo ambayo ni ya uzalishaji hii ni pamoja na viwanda vya usindikaji. Kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba katika miradi yetu yote ya sasa ikiwemo Mbarari tunao mpango huo na kwamba tuwasiliane aweze kujua ni maeneo gani umeme utaenda katika maeneo ya Mbarali.

Na. 79

**Wachimbaji Wadogo Kutambuliwa**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

(a) Je, ni lini wachimbaji wadogo wadogo wa Ng'omberi, Kararami, Kigwasi watatambuliwa na Serikali na kupewa kipaumbele kwenye uchimbaji?

(b) Je, ni lini wachimbaji hao watapewa mikopo ya kujikimu wakati wakitafuta madini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza Mkakati wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwatambua wachimbaji hao na mahitaji yao ya mitaji, vifaa, mafunzo na maarifa. Utekelezaji wa Mkakati huu unashirikisha wachimbaji wenyewe kwa kuimarisha vyama vyao vya kimkoa na chama cha Kitaifa *(FEMATA)* na kujadili masuala yao katika vikao vya pamoja vya kila baada ya miezi sita baina ya wawakilishi wao na Wizara yangu. Kwa kutambua umuhimu na mchango wa wachimbaji wadogo, Wizara yangu imetoa jumla ya viwanja 612 vya uchimbaji mdogo wa madini katika maeneo ya Ng'ombeni, Kalalani na Kigwase ikiwa ni hekta 3,864. Aidha, Serikali kupitia shirika la Madini la Taifa na Wakala wa Jiolojia inaendelea kubainisha maeneo yanayofaa kwa uchimbaji mdogo ili yaweze kutengwa kisheria na kugawiwa kwa wachimbaji hao.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakamilisha taratibu za mfuko rasmi wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kupata mikopo na vifaa vya uchimbaji na mitaji. Mikopo hiyo itapitia benki ambayo tunaamini kuwa

wana uwezo wa ufuatiliaji wa marejesho ili inufaishe wachimbaji wengi. Hata hivyo, tunawahimiza wachimbaji wadogo umuhimu wa kulipa kodi. Mikopo hiyo haitakiwi kutumika kwa ajili ya kujikimu wakati wachimbaji hao wakitafuta madini kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza. Mikopo hiyo inatakiwa itumike vizuri kwa shughuli za uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na kupata vifaa vya kisasa ili shughuli zao ziwe bora zaidi na waweze kuwa na uhakika wa kuzalisha madini na kujipatia kipato. Hivi sasa Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za manunuzi ya vifaa hivyo ikiwemo, *excavator*, *jackhammers*, pampu za kusukuma maji na *compressors* kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika Kanda zote nane.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana Serikali kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, wachimbaji wadogo wadogo wanaiingizia kodi Serikali kwa kiwango kikubwa. Je, ni lini wachimbaji hawa wadogo wadogo watapatiwa hiyo mikopo?

Serikali imesema wachimbaji wadogo wadogo watapatiwa vifaa vya kuchimbia madini kama vile *compressor, excavator,* sasa ninataka kujua.

Je, katika hawa watakaopata mikopo hiyo, Wachimbaji wadogo wadogo wa Mkoa wa Tanga wamo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli wachimbaji wadogo wana mchango mkubwa hasa kwenye kulipa kodi na kutoa ajira kwa vijana wengi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini, lakini Serikali inaendelea na taratibu za kuandikisha wachimbaji wote wadogo watambulike rasmi kama walipa kodi kwa kuhakikisha kwamba leseni zao ndogo na zenyewe zinakuwa na usajili wa *TIN Number* ili *TRA* pia iweze kuwa na *data base* ya wachimbaji wadogo na mchango wao uweze kuonekana moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mikopo kama nilivyoeleza awali, huko nyuma mfumo uliokuwa ukitumika, fedha hizi za wachimbaji wadogo zilikuwa zikikaa Wizarani na Serikali imeamua kwa maksudi kuzipeleka fedha hizi kwenye benki kama ilivyo mifuko mingine kama mfuko wa kilimo na kwenye madini pia tumekusudia kwa maksudi kuwa na mfuko wa madini kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili waweze kufikia fedha hizi kwa wingi. Lakini pia itasaidia kuwahimiza wachimbaji wadogo kutunza kumbukumbu zao za hesabu ikiwa ni sehemu ya vigezo vya kupata fedha na mauzo yao yote yaweze kutambulika rasmi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachoendelea sasa hivi ni tenda ambayo ilikuwa imetangazwa kwa mabenki yetu yaweze kugombania na benki itakayoshinda kati ya mabenki yetu ya nyumbani mabenki ya kizalendo *then* fedha hizo tutazipeleka moja kwa moja huko kwenye Bajeti iliyopita na Bajeti hii tunakusudia kuongeza fedha zingine ili wachimbaji wengi waweze kunufaika na fedha hizo.

**SPIKA:** Naomba ujibu kwa kifupi Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa kwenye jibu langu nimeeleza kwamba vifaa hivi tutapeleka kwenye kanda zote nane ukiwemo Mkoa wa Tanga kama Kanda ya Mashariki.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Mji wa Mpanda umezungukwa na wachimbaji wadogo wadogo katika umbali usiozidi maili 15, Kijiji cha Mtisi, Machimboni, Ibindi, Katisunga, Dilifu na Kampuni na wachimbaji hao wadogo wamekuwa hapo kwa takribani zaidi ya miaka 40. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kuwamilikisha wachimbaji hao wadogo wadogo maeneo yao?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo haya aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yana wachimbaji wadogo

na mimi mwenyewe nimeyatembelea, lakini tatizo kubwa la msingi hapa wachimbaji wetu wengi wamekuwa wakichimba kwenye maeneo yao bila kuomba leseni. Sasa inapotokea kwamba wanataka kuomba leseni wanakuta maeneo hayo tayari yanamilikiwa na leseni kubwa za utafiti.

Lakini Serikali inaendelea kufanya jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba tunatafuta na kutenga maeneo mengi ya wachimbaji wadogo na kuwaomba wenye leseni kubwa kuachia baadhi ya leseni zao ambazo wanadhani hazifai au hazitoshi kwa uwekezaji mkubwa na maeneo hayo yote tunayagawa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, namwahidi Mbunge kwamba tunalifanyia kazi eneo la Mpanda na Kigoma kuhakikisha wachimbaji wadogo pia tunawatengea maeneo yao kwa kuwapatia leseni ili waweze kuchimba kisheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumetumia zaidi ya dakika tano, tunaenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Agripina Buyogera atauliza swali hilo Mhehsimiwa Machali kwa niaba yake.

Na. 80

**Soko kwa Mazao ya Wakulima Kasulu.**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA)** aliuliza:-

Wakulima wa Wilaya ya Kasulu hususani katika Jimbo la Kasulu Vijijini, hawana soko la uhakika kwa mazao yao kama ilivyo kwa baadhi ya maeneo mengine ambako Serikali hununua mazao ya Wakulima:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga soko la uhakika kwa ajili ya Wakulima wa Kasulu?

(b) Wauzaji wa mazao wamekuwa wakisumbuliwa kulipa ushuru kwa gharama tofauti kwa kila Kijiji na wakati mwingine hulazimika kulipa ushuru mara mbili.

Je, Serikali inatoa ufafanuzi gani kwa hali kama hiyo kwa manufaa ya wananchi wa Kasulu Vijijini na kwingineko nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mhehsimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ina mpango wa kujenga soko la mazao ya wakulima ili kurahisisha uuzaji na ununuzi wa mazao ya wakulima. Hadi sasa, hatua iliyofikiwa katika kujenga soko hilo ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kusaini Mkataba wa Maelewano *(MoU)* na Benki ya Taifa ya Rasilimali *TIB* mwezi Mei, 2012.

Katika makubaliano hayo, benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* imekubali kuchangia asilimia 80 ya gharama za ujenzi wa soko hilo na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imekubali kuchangia asilimia 20. Soko hilo Kuu la mazao ya kilimo linatarajiwa kujengwa eneo lililopo katikati ya vijiji vya Mgombe na Nyachenda.

Aidha, ili kuondoa migogoro ya ardhi hususan katika eneo litakalojengwa soko hilo, Serikali Wilayani Kasulu imekamilisha uwekaji wa maeneo hayo kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji hivyo kabla ya ujenzi huo kuanza.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu inatoza ushuru kwa kuzingatia sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 kifungu cha 7 (1) (g) ya mwaka 1982 ambapo ushuru unaotozwa ni kati ya asilimia 3 na 5 ya bei ya shambani *(farm get price)*.

Kwa mujibu wa sheria hiyo wakulima hutakiwa kulipa ushuru wa mazao mara moja katika maeneo ya mazao husika yanayokozalishwa.

Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto za wakulima kutozwa ushuru mara mbili kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuuza mazao yao bila ya kudai au kupewa stakabadhi za malipo pamoja na baadhi ya wakulima kulipia ushuru sehemu ndogo za mazao yao hivyo kupelekea kutakiwa kulipa ushuru mara mbili.

Mheshimiwa Spika, aidha, zipo tuhuma za baadhi ya watendaji wasio na uadilifu katika kazi hii ya kukusanya ushuru. Hivyo ninawahakikishia wananchi kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu na imani ya wazalishaji wa mazao ya kilimo katika mfumo huu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara na taasisi husika itafanya jitihada za makusudi za kupambana na watu hao. Aidha, ni matarajio yetu kuwa wadau wote katika maeneo ya kilimo watashirikiana na Wizara yangu katika vita hii yenye umuhimu wa kipekee. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa fursa niulize maswlai mawili madogo ya nyongeza.

Suala la ujenzi wa soko la Kimataifa imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Wilaya ya Kasulu. Kwa kuwa *TIB* wameridhia kwamba watachangia asilimia 80 na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu asilimia 20, ningependa kufahamu ni lini sasa utekelezaji wa *TIB* kwa maana ya *TIB* watakuwa tayari kuweza kutoa pesa hizo ambazo ni asilimia 80 ili soko hilo liweze kujengwa?

Mheshimiwa Spika, suala la kutoza ushuru kwa mujibu wa Sheria hiyo, ambayo imetajwa hapa inaongozwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kwamba, ushuru utozwe kati ya 3% na 5%. Tatizo ni nini kuhusiana na suala la kuweza kurekebisha Sheria hii. Ni kwa nini Sheria hii isitaje *exact* kwamba, ushuru unaopaswa kutozwa aidha ni 3% au ni 5%, ili kuweza kuondoa utata kutoka eneo moja na kwenda eneo jingine? Kwa sababu, ina-*course* kama *contradiction;* unakwenda Kijiji X, unawatoza 3% halafu Kijiji kingine unakwenda kuwatoza 5%. Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza nimesema kwamba, makubaliano yaliyofikiwa ni baina ya Halmashauri ya Kasulu na *TIB;* Kasulu wachangie 20% na *TIB* wachangie 80%. Mheshimiwa Mbunge, ananiuliza ni kwa nini limechelewa?

Mheshimiwa Spika, mimi ningefikiri kwamba, yeye ndiye angetuambia ni kwa nini limechelewa? Kwa sababu, Mbunge, wewe ni sehemu ya Halmashauri. Sasa ungeniambia kwa nini tatizo hili limechelewa na yapo makubaliano yaliyofikiwa, mimi kama Wizara sasa ningeweza kuingilia kati kwa kuisukuma *TIB* na kuiambia kwamba, basi wafikie sehemu wakubaliane.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nikuahidi kwamba, kwa sababu, tuna mkakati wa kuimarisha masoko haya na mengineyo maeneo mengine, kuna mradi wa *DASIP* ambao utaongeza masoko saba (7) nchini; tutafuatilia kujua tatizo ni nini. Kwa kushirikiana na *TAMISEMI* na Halmashauri ya Kasulu, tutasukuma kwa sababu, kama makubaliano yalikuwepo basi acha mradi huu uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la pili 3% na 5% kwa Halmashauri, ni jambo ambalo Sheria imeweka, ili Halmashauri yenyewe itathmini na kuangalia ni kiwango gani

ambacho imtoze mkulima bila kumwathiri katika uzalishaji wake. Kwa hiyo, labda niseme tu kwamba, tatizo sio 3% na 5%, tatizo ni kwamba, Halmashauri nyingi zinategemea mpaka 60% kutokana na mapato haya. Lakini wakishakusanya, makusudi ya makusanyo yale yalikuwa yarudi kwa wakulima, ili kuchangia uzalishaji wa ziada. Tumekuta kwamba, katika asilimia ile, hata 3% na 4%, hairudi kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ndio changamoto. Wizara yetu kwa kuhusiana na Wizara ya *TAMISEMI* na Wizara ya Fedha, tunaangalia namna ya kuweka mfumo mpya wa ukusanyaji ushuru wa mazao, ili uwe na maslahi kwa wakulima kwanza, halafu manufaa kwa Halmashauri husika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli kabisa kwamba, wakulima wa nchi yetu ya Tanzania na hasa wakulima wa mazao ya chakula, wamekuwa wakianguka sana kiuchumi kwa sababu, Serikali bado hatujawasaidia kuweka mfumo mzuri wa masoko wa kuuza mazao yao kwa faida ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hivi karibuni Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha, walitengeneza Mpango kabambe wa kufungua masoko maalum ya mazao katika mipaka yote ya nchi ya Tanzania, ukiwemo mpaka unaounganisha Tanzania na Msumbiji, katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Lakini toka mpango huo umeanza kuzungumzwa, hatujui nini kinachoendelea na hatujui hatua gani iliyofikiwa.

Je, Serikali, sasa iko tayari kutoa taarifa ya mpango huo kabambe wa kuwakomboa wakulima, hapa ndani ya Bunge, ili Waheshimiwa Wabunge wote, wayafahamu masoko hayo ni mangapi, yatakwenda kujengwa wapi na yatakwenda kujengwa lini na kuweza kuwaandaa wakulima kufaidika na mpango huo wa kuwakomboa kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, leo Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, atasoma Bajeti ya Wizara yetu na kwa muda wa siku mbili, masuala hayo yote yatajadiliwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Kwa hiyo, hili ni katika moja ya masuala ambayo yatajadiliwa. Ninaomba nimhakikishie tu kwamba, hili suala la masoko ya mpakani, pia ni katika mambo ambayo tunatarajia kuzungumzia wakati tunahitimisha masuala ya Bajeti yetu, kesho jioni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea jamani, kumbe amenikumbusha Wizara yake inakuja sas hivi. Tuendelee tu.

Na. 81

**Uhaba wa Wataalam wa Kilimo Nchini**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA (K.n.y. MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE)** aliuliza:-

Kutokana na upungufu wa watalaam wa kilimo hapa nchini, imekuwa vigumu kuwafikia wakulima na kuwaelimisha juu ya mambo mbalimbali kama vile mwenendo wa hali ya hewa, mbegu bora, pembejeo, mbolea na utaalam wa udongo:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani kupata watalaam wa Kilimo wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mhehsimiwa Mchungaji Dokta, Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali ilifanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za ugani nchini na kubaini kwamba mojawapo ya vikwazo vikubwa vya upatikanaji wa huduma za ugani kwa ufanisi nchini ni upungufu mkubwa wa watalaam. Tathmini hiyo ilionesha kwamba, walikuwepo watalaam kama 3,400 hivi nchini ikilinganishwa na mahitaji ya watalaam 15,000. Katika kukabiliana na upungufu huo, Serikali, iliandaa na kuanza kutekeleza mpango wa kuimarisha huduma za ugani nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango huo, kuanzia mwaka 2007 Serikali imevifufua Vyuo 13 vya kilimo *MATIs* vilivyo chini ya Wizara yangu. Ukarabati mkubwa kwa Vyuo vitatu vya Ukiriguru, Maruku na Naliendele, Mtwara na ukarabati mdogo kwa baadhi ya Vyuo kumi vingine umefanyika. Serikali, pia imenunua samani katika mabweni, madarasa na vifaa vya jikoni, pamoja na kuajiri wakufunzi wapya takribani 156. Aidha, vyuo viwili vya mashirika yasiyo ya kiserikali vilishirikishwa katika kutoa mafunzo yanayolenga kuongeza idadi ya wagani; vyuo hivyo kwa sasa vina uwezo wa kudahili wanafunzi 3,500 kwa mwaka kwa wakati mmoja, ikilinganishwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 600 uliokuwepo kabla ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni 2012, idadi ya watalaam wa ugani imeongezeka kutoka idadi hiyo ya 3,400 mwaka 2007 hadi Wagani 7,975 baada ya kuajiri vijana waliohitimu katika vyuo hivyo.

Aidha, wapo jumla ya vijana 1,500 ambao hawajapata ajira katika mwaka 2012 na pia wahitimu 1,000 wa mwaka 2011/2012 ambao watakuwa ni miongoni mwa vijana 1,800 watakaoajiriwa na Serikali Mwaka huu wa Fedha unaokuja 2013/2014 baada ya Idara Kuu ya Utumishi kuota kibali. Idadi hiyo ya watalaam watakaoajiriwa katika ngazi ya vijiji na Kata itasababisha kuongezeka kwa idadi ya watalaam hao hadi kufikia 9,770.

Aidha, wapo pia wanafunzi 2,400 watakaohitimu Juni, 2013 ambapo, watakapoajiriwa watafikisha idadi ya wagani kufikia takribani 13,000 katika ngazi ya Kata na Vijiji. Hii inamaanisha kuwa, kutakuwa na upungufu bado wa watalaam 2,160 ili kufikia lengo la kuwa na Afisa Ugani katika kila Kata na Kijiji.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na uhaba au uchache wa Wataalamu hao, lakini bado huduma zao hazitoshelezi kwa wakulima. Wabunge, Vikao vya nyuma wamekuwa wanasisitiza Wataalamu Ugavi hawa wanatakiwa wawe na Mashamba Darasa. Sasa ni lini Serikali, itaweka katika Hadidu za Rejea katika Ajira za Wataalamu hawa, ili na sisi tuweze kuwafuatilia kama wanatimiza wajibu wao kwa kupitia Mashamba yao Darasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili ni katika swali ambalo tunatarajia tutalizungumza sana hapa. Suala la Wagani, liko kwenye Mamlaka ya Halmashauri. Wizara yangu, inawajenga, inawasomesha, baada ya kuwaombea kibali inawapeleka kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, utendaji wao kule ni suala la Halmashauri na Viongozi wa huko, Madiwani, na kadhalika, pamoja na Wabunge husika.

Mheshimiwa Spika, lakini tumegundua kwamba, kuna utendaji ambao hauridhishi katika Wagani hawa wanapokuwa katika ngazi za Halmashauri kwa sababu, sisi ndio tunaowapa taaluma, lakini wanasimamiwa na watu wengine. Kwa hiyo, tumekubaliana na TAMISEMI kwamba tutatengeneza kitu kinaitwa *Model by-Laws* ambazo ni Mwongozo wa namna ya Wagani, watakavyofanya kazi wakiwa huko.

Mheshimiwa Spika, hizo *Model by-Laws* zitasimamiwa na sisi Wizara ya Kilimo na wao *TAMISEMI* kwa pamoja, ili kuhakikisha kwamba Wagani watakapokuwa huko wanafanya kazi kwa mujibu wa taaluma na uwezo waliojengewa na Serikali. Kwa hiyo, huo ndio mpango, lakini tutauelezea zaidi wakati wa maelezo ya Bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Na. 82

**Wanafunzi Wanaokosa Elimu kwa Kukosa Mikopo**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Ibara ya 11 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo:-

(a) Je, kwa nini Serikali, imeshindwa kuwapatia mikopo baadhi ya wanafunzi wenye sifa za kuendelea na masomo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa wa makusudi wa kuhakikisha kuwa, wanafunzi hao wanapata elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, ina nia njema ya kuhakikisha kuwa, kila Mtanzania mwenye uwezo wa kusoma Chuo cha Elimu ya Juu anapata fursa hiyo. Kwa mwaka wa masomo 2012/2013, wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza waliowasilisha maombi ya kupata mkopo walikuwa 37,315.

Baada ya uchambuzi, wanafunzi waliobainika kuwa na sifa ya kukopeshwa walikuwa 34,140 lakini wanafunzi waliopata mkopo mpaka sasa walikuwa 30,319 sawa na asilimia 88.9 ya waombaji wote waliostahili kupewa mikopo. Kwa mantiki hii, wanafunzi waliokosa mikopo ki idadi ni 3,821 sawa na asilimia 11.1 ya wanafunzi wote walioomba mkopo. Wanafunzi hawa wachache walikosa mikopo hiyo ni kutokana na ukomo wa kibajeti pamoja na vipaumbele vilivyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 326.0 katika mwaka wa masomo 2012/2013 kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi 95,902 wakiwemo wa mwaka wa kwanza, ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 56.1 kilichokuwa kimetengwa mwaka wa masomo 2005/2006 kilichomudu kukopesha wanafunzi 42,729 tu. Ongezeko hili ni ishara tosha ya nia njema ya Serikali, kuhakikisha wanafunzi wote wenye sifa za kusoma Vyuo vya Elimu ya Juu wanapata mikopo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye sifa wanakopeshwa ili wapate elimu ya juu, Serikali, iliunda Kikosi Kazi, ili kuweza kubaini vyanzo vingine vya kupata fedha za ukopeshaji.

Aidha, Kikosi Kazi hicho kimewasilisha taarifa ambayo tayari inafanyiwa kazi. Kwa sasa Serikali, inatekeleza Agizo la Azimio la Bunge la Mkutano wa 10 kwa kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu na Sheria Namba Tisa ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ili kuweka utaratibu utakaowezesha kubaini vyanzo Mbadala vya Kugharimia Elimu ya Juu.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Elimu, amekiri kwamba, wapo zaidi ya wanafunzi 3,000 wenye sifa za kupata mkopo wa kuendelea na masomo, wameshindwa kupata mkopo huo. Hii ni kwa mwaka mmoja tu, inawezekana miaka mingine wapo wanafunzi kama hao.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kufanya hivi ni kuliangamiza Taifa kielimu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Anawaeleza nini wale wote ambao wamekosa nafasi hii adimu ya masomo kwa miaka yote iliyopita kuendelea na masomo? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge, anaelewa jitihada za Serikali; na hata Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Bunge lililopita alileta Hoja Binafsi ya Serikali, iweze kutafuta fedha au njia mbadala kwa ajili ya kutafuta fedha kuwakopesha vijana hawa.

Serikali, ilisikia na kwa pamoja tuliridhia na tukaagizwa kama Azimio la Bunge kwamba, tuunde Kikosi Kazi kitakachoweza kuleta mabadiliko ya Sheria haya. Tunaahidi katika Bunge lijalo tutaleta maridhiano ya Sheria hii, ili Bunge, liweze kufanya *Ammendment* ya Sheria ya Elimu pamoja na ile ya Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Na. 83

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Ahadi ya kuweka minara ya mawasiliano ya simu maeneo ya Kiyombo, Kitunda, Kiloli na Ibumba ni ya muda mrefu, lakini haijatekelezwa hadi sasa:-

Je, Serikali, ina mikakati gani ya kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF),* inaendelea na utaratibu wa kuainisha na kutathmini mahitaji ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi sasa, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeainisha Vijiji vya Kata za Kitunda, Kiloli, Kipili, ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Kiyombo, na imeonekana dhahiri kuwa, hadi sasa Vijiji hivyo, havina mawasiliano. Hivyo, Vijiji vya Kata tatu kati ya nne alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, ni miongoni mwa maeneo yaliyoainishwa kwenye zabuni ijayo, itakayotangazwa mwezi huu wa Aprili, 2013 ili viweze kupatiwa ruzuku na hatimaye kupata mawasiliano pindi zoezi la Zabuni la kumpata mjenzi litakapokamilika.

Aidha, kwa kuwa, mpango wa kufikisha mawasiliano kupitia Mfuko huu ni endelevu, Vijiji vya Kata ya Mole, ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Ibumba, vitafikiwa katika awamu zijazo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wote zikiwemo kampuni za simu, ili kufanikisha lengo la kufikisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini. Kupitia jitihada hizi Serikali, ina uhakika wa kufikisha mawasiliano nchi nzima, ili kuharakisha maendeleo ya kijamii kupitia huduma za mawasiliano. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba mpaka ifikapo mwezi Aprili, zabuni zitakuwa zinatangazwa. Sasa Serikali, itakuwa tayari kuhakikisha kwamba, mchakato huo unaisha kwa haraka zaidi?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, amekuwa Kiongozi wa mfano, mtu wa kwanza kufika katika maeneo hayo toka uhuru.

Sasa ninyi, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, mtaiga mfano huo tutakapokamilisha kazi hii, kuja kuhakikisha kwamba, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) imetekelezwa, kuja kuhakikisha haya mliyoyafanya yanakwenda kwa wananchi, wananchi wayaone kwa ninyi wenyewe kufika kuja kuja kuyakabidhi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu Maswali mawili ya Mheshimiwa Nkumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mchakato tunauharakisha

kadiri iwezekanavyo, ili kuhakikisha kwamba, tunatekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi. Kwa hivyo, asiwe na wasiwasi, mchakato unakwenda kwa kasi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, , kuhusu kwamba, tufike kule. Basi, ujumbe huu nitamfikishia Mheshimiwa Waziri anayehusika na mimi kama itawezekana, basi nitaongozana na yeye ili niende sehemu anayotoka. Kwa sababu na mimi ni mdau wa eneo hilo.

Na. 84

**Mawsilianoya Simu za Mkononi – Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Asilimia 95 ya maeneo ya Jimbo la Kahama wanapata huduma ya simu za mkononi isipokuwa maeneo ya Kata ya Uyogo, Igwamanoni, Chona, Idahina na Ukune, ambayo hayana mtandao na usikivu wake ni wa matatizo sana. Na kwa sababu, Serikali, katika Bunge la 9 na sasa Bunge la 11, iliahidi kufuatilia kwa karibu tatizo hilo kwa maana ya kuunganisha maeneo hayo kwenye mtandao kurahisha mawasiliano na kumaliza tatizo hilo:-

Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa ahadi zake ilizozitoa Bungeni kuhusiana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, 95% ya maeneo ya Jimbo la Kahama wanapata huduma za simu za mkononi, isipokuwa maeneo ya Kata ya Uyogo, Igwamanoni, Choma, Idahima na Ukune, ambapo hayana mtandao na usikivu wake ni wa matatizo sana. Na kwa sababu, Serikali, katika Bunge la 9 na sasa Bunge la 11 iliahidi kufuatilia kwa karibu tatizo hili, kwa maana ya kuunganisha maeneo hayo kwenye mtandao, kurahisisha mawasiliano na kumaliza tatizo hilo Serikali.

Serikali itahakikisha kwamba, inafikisha mawasiliano katika maeneo hayo kwa kwa asilimia mia moja (100%) na wakazi wa Jimbo watapata mawasiliano.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni kweli makampuni hayo tayari yamekwisha fanya kazi taarifa ya Serikali na kwamba huduma za simu za mkononi sasa zimeshafika katika kata za Chona na Ukune kati ya kata nne ambazo zilikuwa na matatizo hapo awali.

Je, Serikali inasema nini kwa maeneo yaliyobaki ya Kata za Igwamanono na Idahina?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na teknolojia, naomba nimjibu Mheshimiwa Daud Lembeli swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba mawasiliano yapo 95% na katika maeneo ya Mheshimiwa aliyoyasema kwa kweli siyo nia ya watoa huduma kufanya maeneo hayo yasipate huduma nzuri kwa sababu tayari minara ipo. Kwa hiyo, kwa vile ni kufanya tu *optimization* nina uhakika kwamba makampuni haya kwa vile tumewasiliana nayo yataweza kufanya *optimization* na kuhakikisha kwamba maeneo ambayo hayasikiki vizuri yanasikika vizuri hivi karibuni. *(Makofi)*

Na. 85

## Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kazi kubwa ya Serikali ni kuleta maendeleo ya jamii, wanawake na watoto:-

(a)Je, kwa nini Bajeti ya Wizara husika ni ndogo sana ikilinganishwa na sekta nyingine?

(c) Je, Serikali ipo tayari kuelekeza Wizara nyingine kuchangia asilimia thelathini ya Bajeti zao kwa ajili ya Maendeleo ya jamii, wanawake na watoto kama ilivyoelekeza kwenye *desk* la jinsia kila Wizara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali hutenga Bajeti kwa mafungu mbalimbali kutokana na Makadirio ya Mapato ya mwaka wa fedha husika. Ukiangalia Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni bilioni 17 na Mwaka 2012/2013 ni bilioni 14. Ni kweli kwamba haikuongezeka. Aidha Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia shilingi 21.9 bilioni kutoka shilingi bilioni 14 sawa na asilimia 56.4 ya Makadirio ya mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kutafuta njia za kuongeza vyanzo vya mapato ili mapato ya Serikali yaweze kuongezeka. Mapato ya Serikali yakiongezeka ni dhahiri kwamba Bajeti za mafungu mbalimbali zitaongezeka ikiwemo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jibu la swali la (b) napenda ieleweke kwamba moja ya majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni kuratibu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara nyingine na Taasisi za Umma na kijamii ambapo shughuli hizo hutengewa fedha na kutekelezwa na Wizara au Taasisi husika, ikiwa ni pamoja na asasi za Kiraia *(CBOs).* Hii inafanya kazi ya Wizara kuwa ya kuratibu na kusimamia mikakati iliyowekwa kitaifa juu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ongezeko la Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto litatokana na vipaumbele pamoja na ongezeko la Mapato ya Serikali na si kupunguza Bajeti za Wizara nyingine kwa asilimia 30 kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana kwa niaba ya Serikali lakini Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kuongeza Bajeti ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii tunazungumza pia kuongeza Bajeti kwenye fungu la Maendeleo kwa sababu za kimsingi.

Mheshimiwa Spika, takribani sasa miaka nane Serikali imekuwa haitengi fedha kwenye Bajeti ya Maendeleo ili kuiwezesha Wizara kutoa fedha kwenye mfuko wa maendeleo ya wanawake ambao fedha hizo zilikuwa zinakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri na kuendeleza vikundi vya wanawake kwenye Halmashauri zote nchini. Kutokufanya hivyo kumewanyima fursa wanawake wa vijijini kupata fedha kupitia kwenye mfuko wao wa Maendeleo. *(Makofi)*

Je, Serikali inalitambua suala hilo na kama inatambua Bajeti ya mwaka huu itatoa fedha za kuwaendeleza wanawake kiuchumi kupitia mfuko huo baada ya miaka nane kukosa?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili. Wizara hii imekuwa na kazi ya kusimamia Maendeleo yote katika nchi ya Tanzania. Ukizungumza suala la Maendeleo ni katika sekta zote. Sasa hivi tuna matatizo mengi yakiwemo watoto wa mitaani wameendelea kuongezeka na maeneo mengi ya namna hiyo. Serikali inaonaje kwamba matatizo ya kimaendeleo siyo *priority* na kuacha kutenga Bajeti ya ongezeko kwenye Wizara hii. Je, kuanzia mwaka huu wa fedha 2013/2014 Serikali itaona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii ili masuala mtambuka ya Maendeleo yaweze kushughulikiwa?

**SPIKA:** Lakini umepiga hotuba, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana muda umeisha, maana au unaongeza fedha au huongezi si basi!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala zima la fungu la Maendeleo kwa ajili ya Wizara hii. Mara nyingi miradi ya maendeleo inaibuliwa na Wizara wahusika na kutokana na hilo ndiyo Bajeti zinapangwa kufuata hilo. Tutajitahidi kufanya kazi pamoja na Wizara husika kuhakikisha kuwa mipango yote ambayo wanaiibua inakamilika ili tuweze kuipatia fedha. Hatuwezi kutoa pesa kwenye fungu bila kuwa na kitu cha kulipia. Kwa hiyo, tunaomba tunaishauri na kushawishi Wizara yenyewe ije na miradi kamilifu ya kimaendeleo ili tuweze kuitafutia fedha. Wizara ya fedha haipangi pesa bila Wizara yenyewe kuainisha miradi gani ya maendeleo inataka kuiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili kuhusiana na kuongeza fedha kwa ajili ya mifuko ambayo itawasaidia na wananchi hasa wanawake vijijini kuweza kupata mikopo ningependa vilevile kutaarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inahusika na uratibu ni kazi yetu sisi Wabunge kuhakikisha kuwa kila sekta, kila idara ya Serikali inafanya kazi ya kuhakikisha kuwa katika sekta yao inaibua yenyewe miradi au changamoto ambazo zinaweza kusaidia wanawake, mambo ya jinsia yote yanatakiwa yawe katika kila Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwaombe Wabunge katika kamati tunazoingia za Bunge wote tuulize hili swali kila Wizara iweke fungu maalum kwa ajili ya kufanya shughuli hizi ambazo zinaratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hii ndiyo njia itakayowezesha Wizara hii kuweza kutekeleza shughuli zake. Hii Wizara siyo peke yake iliyopewa kazi ya kusimamia masuala haya ni Wizara ni Wizara zote Serikali nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge tumezidiwa na muda ingawa hizi dakika tano ni zile zilizotumika kuwasilisha nyaraka zinazopaswa kufanyiwa kazi leo kwa hiyo, tupo vizuri.

Matangazo leo tuna wageni wa Kimataifa ambao wamekuja kushirikiana na sisi katika shughuli zetu hasa kushirikiana na mfumo mzima wa kamati ya Hesabu za Serikali. Wameanzisha katika kanda ya *South Africa* wameanzisha utaratibu wa Kamati zinazohusika na *Public Accounts Committee* wana umoja wao sasa viongozi wao hawa wamekuja kwa ajili ya kushauriana na ofisi yangu kwa sababu mwaka huu sisi tutakuwa wenyeji wa Mkutano wa namna hii katika nchi yetu hapa mwezi wa tisa.

Kwa hiyo, chama hiki kinaitwa *SADCO-PAC* ambayo tutakuwa tuna mkutano safari hii hapa nchini.

Kwa hiyo, wageni ambao wamekuja hapa ni Mheshimiwa Sinpho Makama, ambaye ni Mwenyekiti wa *SADCOPAC* na ni Mbunge kutoka Bunge la Afrika Kusini *can we have three of you* ahsante sana. *Thank you very much.* Tuna Mheshimiwa Weba Chinyaza yeye Katibu Mkuu wa *SADCOPAC* na pia Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kutoka Bunge la Zimbabwe ahsante sana. Tunaye *Ms*. Catherine Tobejane, yeye katibu wa Kamati ya *APAC* ya Bunge la Afrika kusini, naomba pia asimame *where is she okay.* Kwa hiyo hawa ndiyo waliokuja hapa kwa ajili ya maandalizi na tutakutana nao baadaye kama nilivyosema. Tuna kikao nao na tutakuwa sisi wenyeji wa mkutano huu mwezi Septemba katika nchi yetu.

Baada ya kusema hivyo pia hawa jamaa jana mchezo wa *Bunge Sports Club, Club* yetu wanaeleza kwamba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mchezo wa mpira wa miguu na mpira wa pete iliyochezwa siku ya Jumamosi tarehe 20 Aprili, 2013 kati ya Bunge *Sports Club* na wanachuo kutoka chuo cha Mzumbe, Morogoro kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu hapa mpira wa miguu timu ya Bunge ilipata sifuri na timu ya Mzumbe ilipata goli moja. Kamati ya ufundi ilizidiwa kete wakajaribu kuleta nyuki hazikusaidia kitu nadhani wangekosa nyuki wangekula mabao mengi kweli kweli Waheshimiwa Wabunge.

Kuna wenzetu wanaocheza mpira wa pete timu ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ni mabingwa wa Bunge la Africa Mashariki iliwaburuza bila huruma timu ya Mzumbe jumla ya magoli 43 kwa magoli saba. Kama kawaida na nidhamu yao nyota wa mchezo huo alikuwa ni Mheshimiwa Grace Kiwelu. Kwa hiyo mazoezi yaendelee msituletee tena nyuki baadaye mtaleta simba bure. Kwa hiyo tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na kazi. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2013/2014
### Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika sasa lijadili na kukubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2013/ 2014.

Mheshimiwa Spika, hotuba ninayoisoma ni ufupisho wa hotuba ndefu ambayo ipo katika kitabu changu. Hotuba inaelezea hali ya kilimo na ushirika nchini, mapitio ya utelelezaji wa malengo na mpango wa mwaka 2012/2013 na mpango wa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ambao wengi wao ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa pekee katika kuendeleza Sekta ya Kilimo. Msukumo huo umeoneshwa dhahiri katika shughuli zake mbalimbali mathalan, tarehe 19 Machi, 2013 Mhesimiwa Rais alizindua maabara ya kisasa ya kwanza ya Uhandisi Jeni

katika kilimo Tanzania iliyopo katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni. Katika uzinduzi huo, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kuendeleza utafiti wa Uhandisi Jeni na GMO ili wataalamu wetu waweze kujua vizuri teknolojia hiyo, faida na athari zake.

Aidha, Mheshimiwa Rais alisifu kazi za watafiti wetu na kuagiza kwamba watafiti waendelee kufanya kazi baada ya tarehe za kustaafu kutokana na uchache wao na Wizara iwe na mikakati ya kuajiri watafiti vijana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais, ambaye amekuwa akifanya ziara mikoani na kusisitiza umuhimu wa kilimo katika kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza umaskini. Aidha, nampongeza Makamu wa Rais kwa kushiriki katika kilele cha maadhimisho ya sikukuu ya wakulima Nane Nane yaliyofanyika kitaifa Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake za kuendeleza kilimo kupitia azma ya KILIMO KWANZA nchini. Vilevile, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mfano tosha kwa wale wanaotaka kuingia kwenye kilimo kwa sababu yeye ni mkulima na amekuwa akihamasisha uwekezaji katika kilimo na kuwepo kwa usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu tukufu kwa umahiri mkubwa. Uongozi wenu ndio umetufikisha hapa ambapo hadi hivi sasa Bunge letu halina migogoro yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013 Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa kuondokewa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Jimbo la Chambani – Zanzibar *(CUF).* Nawapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia

ya marehemu. Mwenyezi Mungu ailaze roho za marehemu mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Peter Mahamud Msolla, Mbunge wa Kilolo kwa maoni, ushauri na ushirikiano mkubwa walioutoa na ambao wameendelea kuutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014. Wizara yangu inampongeza Mheshimiwa Profesa Peter Mahamud Msolla kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Maji na Mifugo na Mheshimiwa Said Juma Nkumba kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti. Pia inawapongeza wanakamati wapya walioteuliwa kujiunga na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2013/2014 katika vikao vyake vilivyofanyika Dar es Salaam tarehe 03 na 04 Aprili 2013 na Dodoma tarehe 12 Aprili 2013. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Buyungu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa hotuba yake ambayo imeelezea kwa muhtasari hali ya kilimo chetu kilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, hali ya kilimo na ushirika nchini, sekta ya Kilimo ni moja ya Sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia

75 ya Watanzania na inachangia wastani wa asilimia 95 ya chakula kinachopatikana nchini kwa miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2012, Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 26.8 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 23.7 mwaka 2011. Kwa kuwa asilimia kubwa ya watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo, mchango huo kwa kiasi kikubwa utachangia katika kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa kwa mwaka 2012, kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji, misitu na uwindaji ulikuwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 3.6 mwaka 2011. Katika ukuaji huo, mchango wa mazao ulikuwa asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 3.5 ya mwaka 2011. Mchango wa mifugo ulikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.9 ya mwaka 2011. Mchango wa misitu na uwindaji ulikuwa asilimia 2.4 ikilinganishwa na asilimia 3.5 ya mwaka 2011. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa mazao ya chakula, hususan mahindi uliongezeka kutoka tani milioni 6.5 mwaka 2011 hadi tani milioni 6.7 mwaka 2012 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3.1.

Aidha, uzalishaji wa mpunga uliongezeka kutoka tani milioni 1.6 mwaka 2011 hadi tani milioni 1.7 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Ongezeko hilo limetokana na kuwepo kwa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na juhudi za Serikali za kuongeza uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, hali ya ushirika, Wizara imeendelea kuwezesha na kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za kiuchumi kupitia utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na *modernization* ya Ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernization Program – CRMP*). Katika kuimarisha Ushirika nchini, idadi ya Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 9,769 Machi, 2012 hadi 9,964 Machi, 2013 ikiwa ni ongezeko la Vyama vya Ushirika 195.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Societies – SACCOS*) vimeendelea kuimarishwa ili viweze kutoa huduma za kifedha

kwa wananchi wengi zaidi hususan waliopo vijijini. Idadi ya *SACCOS* imeongezeka kutoka 5,424 Machi 2012 hadi 5,559 Machi 2013 na wanachama wameongezeka kutoka 917,889 hadi 1,153,248 katika kipindi hicho. Aidha, wanachama wameongeza hisa, akiba na amana kutoka shilingi bilioni 236.8 hadi shilingi bilioni 463.5.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika wa Mazao (*Agricultural Marketing Cooperative Societies – AMCOS*) vimeendelea kutoa huduma kwa wakulima zikiwemo za usambazaji wa pembejeo, ukusanyaji na uuzaji wa mazao. Wanachama wameendelea kunufaika na mfumo wa stakabadhi za maghala kwenye mazao ya nafaka na korosho kupitia Vyama vya Msingi na *SACCOS.* Kupitia Vyama vya Ushirika, pembejeo za kilimo zilisambazwa kwa wakulima zikiwemo mbolea, vifungashio na madawa ya kuua wadudu hususan kwa mazao ya tumbaku na korosho, mbegu na miche ya kahawa, miti na matunda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Ushirika bado unakabiliwa na changamoto za baadhi ya viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika kutokuwa waaminifu, uwezo mdogo na kutowajibika katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuimarisha usimamizi kwa kuongeza kasi ya ukaguzi wa vyama, kuwajengea uwezo viongozi na kutoa mafunzo kwa wanachama kuhusu haki na wajibu wao. Katika kuimarisha Ushirika, Sheria ya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 inafanyiwa marekebisho na tayari Muswada wa marekebisho ya sheria hiyo umesomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji na upatikanaji wa chakula, tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2011/2012 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2012/2013, iliyofanywa mwezi Januari 2013 ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia tani milioni 13.34 zikiwemo tani milioni 7.44 za nafaka na tani milioni 5.90 za mazao yasiyo ya nafaka. Uzalishaji huo

ukilinganishwa na mahitaji ya chakula ya tani milioni 11.97 kwa mwaka 2012/2013 ungeweza kutosheleza mahitaji ya chakula kwa asilimia 112. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa uhaba wa chakula katika baadhi ya nchi jirani na Serikali kuondoa vikwazo vya kuuza mazao ya chakula, sehemu kubwa ya mazao hayo iliuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzalishaji huo kumekuwepo na maeneo yenye upungufu wa chakula unaotokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya nafaka uliosababishwa na ukame.

Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa, *TAMISEMI* na wadau wengine wakiwemo *WFP, FAO, UNICEF, TFNC, TMA* na Mashirika ya Misaada ya Kibinadamu *(CARITAS, OXFAM, Care International, World Vision*) ilichukua hatua ya kutathmini hali ya chakula kwa kina na kutoa chakula cha msaada kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa wa chakula.

Wizara itaendelea kupanua wigo wa ushirikishwaji wa wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Madiwani katika kufanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, tathmini za kina zilizofanywa Septemba 2012 na Januari 2013 zilibaini kuwepo kwa jumla ya Halmashauri za Wilaya 47 katika mikoa 19 ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Lindi, Tanga, Mtwara, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Mwanza, Mara, Kagera, Iringa, Mbeya, Rukwa, Dodoma na Singida zenye upungufu mkubwa wa chakula.

Hata hivyo, hali ya upungufu wa chakula imekuwa ikiongezeka kwa viwango tofauti hadi kufikia Halmashauri 70. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2012 hadi Machi 2013, Serikali imeidhinisha chakula cha msaada kiasi cha tani 69,452.

Aidha, Serikali imekuwa ikitoa chakula cha njaa kulingana na maombi yanavyowasilishwa na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Makatibu Tawala wa Mikoa. Hadi tarehe 09 Aprili, 2013 uchukuaji wa chakula hicho cha msaada ulifikia jumla ya tani 35,886.75.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mvua za vuli katika robo ya nne ya mwaka 2011/2012 pamoja na upungufu wa chakula katika nchi jirani na zile za Somalia na Sudan ya Kusini kumesababisha bei za vyakula kuendelea kupanda katika maeneo mengi ya nchi kwa karibu kipindi chote cha mwaka 2012/2013.

Bei hizo zimekuwa juu ikilinganishwa na msimu uliopita au bei za wastani wa miaka mitano iliyopita. Kwa mfano, bei ya mahindi kati ya mwezi Novemba 2011 na mwezi Novemba 2012 iliongezeka kwa asilimia 36. Kwa kuzingatia hilo, Serikali iliamua kuuza sehemu ya mahindi kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* katika soko kwa lengo la kupunguza mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2011/2012 uzalishaji wa mchele nchini ulifikia tani 1,170,358 ambapo mahitaji kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa tani 818,699.

Katika mazingira ya mtandao wa biashara uliopo, uzalishaji huo ni mdogo kukidhi mahitaji yetu ya mchele na mahitaji ya soko katika Kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Mahitaji hayo ya soko yalichangia kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo nchini kutoka wastani wa Shilingi 1,500 kwa kilo mwezi Agosti 2012 hadi wastani wa Shilingi 2,800 kwa kilo mwezi Februari 2013 katika masoko ya jumla.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, mnamo mwezi Desemba 2012, Serikali iliamua kuruhusu wafanyabiashara waagize tani 60,000 za mchele ili kupunguza makali ya bei kwa walaji.

Makampuni tisa yaliteuliwa kufanya kazi hiyo kuanzia wiki ya pili ya mwezi Januari 2013, mchele huo ulitakiwa uwe umeingia nchini ifikapo tarehe 30 Machi 2013. Masharti mengine yaliyotolewa kwa waagizaji yalikuwa ni pamoja na bei ya jumla ya mchele isizidi shilingi 1,300 kwa kilo; bei kwa wasambazaji wa kati isizidi Shilingi 1,450 kwa kilo; na bei ya rejareja isizidi Shilingi 1,700 kwa kilo, hadi tarehe 30 Machi, 2013 jumla ya tani 34,689.54 za mchele zilikuwa zimeingizwa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa uzalishaji wa mpunga katika maeneo mengi nchini uko katika hali nzuri, hali inayoashiria kuwepo kwa mchele wa kutosha sokoni. Kufuatia hali hiyo, Serikali imesitisha uingizaji wa mchele wenye msamaha wa ushuru na kodi utakaofanywa baada ya tarehe 30 Machi, 2013.

Pamoja na hatua hiyo, Wizara inaendelea kuhamasisha matumizi ya vyakula vingine mbadala kama vile muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi, maboga, magimbi na vyakula vingine vinavyopatikana kwa wingi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, matarajia ya hali ya chakula mwaka 2013/2014. Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikifanya Tathmini ya Awali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula katika kila msimu wa kilimo na kutoa utabiri wa hali ya Chakula kwa kila mwaka katika mwezi Mei na taarifa kutolewa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara katika Bunge la Bajeti.

Kutokana na mabadiliko ya ratiba ya Bunge la Bajeti ya mwaka 2013/2014 ambapo Bunge limeanza mapema kabla ya mwezi Juni, taarifa ya tathmini ya awali ya uvunaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2012/2013 na utabiri wa hali ya chakula kwa mwaka 2013/2014 itapatikana mwezi Juni 2013 baada ya kufanyika kwa tathmini hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya utekelezaji wa Malengo na Mipango ya Mwaka 2012/2013. Katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013, Wizara imezingatia Malengo ya Milenia, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo Barani Afrikayaani *Comprehensive Africa Agricultural Development Program - CAADP* kupitia Mpango wa Uwekezaji katika Usalama wa Chakula – Tanzania ambao tumejiwekea, yaani *Tanzania Food Security Investiment Plan – TAFSIP,* Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, MKUKUTA II, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Program – ASDP),* na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reform and Modernization Program - CRMP)* na Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara inaendelea kutekeleza Malengo Mkakati yafuatayo:-

(i) Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo;

(ii) Kuwezesha Upatikanaji wa Masoko ya Bidhaa za Kilimo;

(iii) Kuwezesha Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo;

(iv) Kuwezesha na Kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi;

(v) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa Takwimu;

(vi) Kusimamia Sera, Sheria na Mikakati katika Sekta ya Kilimo;

(vii) Kuboresha Uratibu katika Sekta ya Kilimo;

(viii) Kuboresha Uwezo wa Wizara wa kutoa Huduma; na

(ix) Kuzingatia Masuala Mtambuka katika Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya Sh. 291,437,058,400/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 170,364,421,000/= ni fedha za matumizi ya kawaida na Sh. 121,072,637,400/= ni fedha za maendeleo. Baada ya makato ya bajeti kitaifa, Wizara ilipunguziwa kiasi cha Sh. 2,023,291,610/= za matumizi ya kawaida na Sh. 614,282,274/= fedha za maendeleo za ndani na hivyo kubakiwa na jumla ya Sh. 288,799,484,516/= ambapo fedha za matumizi ya kawaida ni Sh. 168,341,129,390/= na matumizi ya maendeleo ni Sh. 120,458,355,126/=.

Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa kutoka Hazina hadi tarehe 19 Machi, 2013, ni Sh. 89,785,797,567/= sawa na asilimia 53 ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yamefikia Sh. 88,256,414,561/= sawa na asilimia 98.3 ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 19 Machi, 2013 ni Sh. 22,961,014,700/= sawa na asilimia 19 ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yamefikia Sh. 11,266,543,824/= sawa na asilimia 49 ya fedha zilizotolewa.

Wizara kupitia Fungu 24 ambalo ni la Ushirika, lilitengewa jumla ya Sh. 6,104,209,000/= za matumizi ya kawaida. Hadi tarehe 18 Machi, 2013, fedha zilizopokelewa ni Sh. 3,313,840,034/= sawa na asilimia 54.29 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yalifikia Sh. 2,735,539,547/= sawa na asilimia 78.23 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza lengo mkakati la Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo, kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kuendeleza umwagiliaji; kutoa ruzuku ya pembejeo; kuongeza uzalishaji wa mbegu bora;

kuimarisha utafiti, huduma za ugani, ukaguzi wa madawa ya kilimo na mbegu; kutoa mafunzo kwa wakulima; kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo; na kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umwagiliaji, Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinachangia asilimia 25 ya mahitaji ya chakula nchini. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya *GPS* ilifanya uhakiki wa eneo linalomwagiliwa na wakulima wadogo, wakubwa na Taasisi mbalimbali katika sehemu kubwa ya nchi na kubaini kuwa kuna jumla ya hekta 450,392 zinazomwagiliwa. Kati ya hizo hekta 389,529 zinalimwa na wakulima wadogo na hekta 60,863 zinalimwa na wakulima wakubwa. Kazi hiyo ya uhakiki inaendelea katika sehemu chache zilizobaki hususan Kanda za umwagiliaji za Mtwara na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, uendelezaji wa skimu 40 zenye uwezo wa kumwagilia hekta 28,114 unaendelea. Hatua za utekelezaji zinaoneshwa katika Kiambatisho Na. 2. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itakamilisha ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu 37 zenye hekta 19,890 za wakulima wadogo.

Kati ya vikwazo ambavyo vimeonekana kudumaza ukuaji wa Sekta ya Kilimo ni uwekezaji mdogo wa Sekta Binafsi katika kilimo cha umwagiliaji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016, Wizara kupitia Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* imejiwekea malengo ya kuongeza uzalishaji wa sukari kwa tani 150,000, mahindi tani 100,000 na mchele tani 290,000 katika mashamba mapya ya wakulima wakubwa na wadogo. Uwekezaji huo unatarajiwa kuongeza eneo linalomwagiliwa kwa hekta 389,000 ifikapo mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi hususan ukame, katika mwaka 2012/ 2013, Wizara inaendelea na ujenzi wa mabwawa saba ya

umwagiliaji ambapo katika bwawa la Inala (Tabora *MC*) – ujenzi wake umefikia asilimia 47; Kasuga (Kakonko) asilimia 85; Mahiga (Kwimba) - asilimia 85; Mesaga (Serengeti) asilimia 30; Lwanyo (Mbarali) asilimia 80; Dongobesh (Mbulu) asilimia 60; na Itagata (Manyoni) asilimia 95. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa mabwawa hayo na kuanza ujenzi wa bwawa la Ulindwanoni (Urambo). Aidha, Wizara itafanya usanifu wa mabwawa katika maeneo kame ya Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Geita na Simiyu.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa skimu 15 zinazogharamiwa na Mfuko wa pamoja wa Msaada wa Chakula unaosimamiwa na Serikali ya Tanzania na Japan *(Food Aid Counterpart Fund – FACF)* unaendelea. Aidha, ujenzi wa skimu nyingine mbili za Gidahababeig (Hanang) na Kashagulu (Kigoma Vijijini) utaanza katika mwaka 2013/2014. Kukamilika kwa skimu hizi kutaongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji kwa hekta 4,187.

Mheshimiwa Spika, miradi sita inayoendelezwa chini ya programu ya *Feed the Future* na kugharamiwa na Shirika la Misaada la Marekani *(United States Agency for International Development - USAID)* ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika skimu ya Dakawa (hekta 3,000) kazi za ujenzi wa barabara *(access road)* mita 800, jengo la Ofisi ya Mradi na Tathmini ya Athari za Kimazingira *(Environmental Impact Assessment - EIA)* zimekamilika. Taratibu za kuwapata wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa pampu mpya na kukarabati miundombinu ya shambani zimekamilika na ujenzi wa miundombinu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2013.

Aidha, usanifu wa skimu ya Mgongola (hekta 640) umekamilika na taratibu za kupata mkandarasi wa ujenzi zimeanza. Upembuzi yakinifu na tathmini za athari za kimazingira katika skimu za Mgugwe (hekta 2,270), Udagaji (hekta 1,950), Kisegese (hekta 7,200) na Mpanga-Ngalimila (hekta 26,372) unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali *(Pre-feasibility studies and preliminary design)* wa miradi katika ukanda wa Ziwa Viktoria iliyotekelezwa kwa kugharamiwa na Ofisi ya Ushirikiano Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative)* kupitia mradi wa *Irrigation Development and Watershed Management Project in the Lake Victoria Basin in Tanzania*. Upembuzi yakinifu huo umebaini kuwepo kwa jumla ya hekta 22,462 zinazoweza kuendelezwa kwa umwagiliaji katika mabonde ya Mto Mara (hekta 6,974); Mto Ngono (hekta 13,255); na Bugwema (hekta 2,233). Miradi hii itaingizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya husika kwa ajili ya utekelezaji miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara imekamilisha maandalizi ya mradi wa uendelezaji wa skimu 39 zenye jumla ya hekta 16,710 za umwagiliaji kwa njia ya matone *(drip irrigation)* kwa mazao ya zabibu, migomba na pamba. Mradi huo ambao utatekelezwa kwa gharama ya Sh. 677,574,776,560/= utaombewa fedha kutoka Serikalini na vyanzo vingine vya fedha ikiwemo mikopo ya masharti nafuu. Utekelezaji wa mradi huo utahusisha uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone; ujenzi wa barabara za kuunganisha skimu na masoko *(farm to market roads);* upelekaji wa nishati ya umeme katika skimu hizo; uwekaji wa miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao yatakayovunwa; na kujenga uwezo wa wataalamu katika ngazi ya Wilaya na Taifa katika kuendeleza na kusimamia miradi ya aina hiyo nchini kwa ufanisi. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Kigoma, Mwanza, Manyara, Kagera na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya utekelezaji wa Programu ya *ASDP* imeonesha kuwepo kwa fedha ambazo hazikutumika, yaani *Carry Over Funds* katika miaka ya nyuma hususan katika ngazi ya Halmashauri. Hadi Desemba, 2012 takriban Shilingi bilioni 25.8 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji zilikuwa bado hazijatumika. Sababu kubwa zilizochangia fedha hizo kutotumika ni pamoja na upungufu wa wahandisi na mafundi sanifu wa umwagiliaji; mtiririko

mbaya wa fedha ambapo wakati mwingine fedha zinatolewa kidogo na kwa kuchelewa; na ukiritimba wa taratibu za manunuzi. Aidha, kiwango kidogo cha fedha za miradi inayotekelezwa na Halmashauri hakiwavutii makandarasi wa ujenzi wenye uwezo na uzoefu ambao wengi wako katika miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeshirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Rasilimali za Maji kuandaa mitaala ya uhandisi katika fani ya ujenzi na umwagiliaji *(Civil and Irrigation Engineering).*

Aidha, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine nacho kimeanzisha shahada ya Uhandisi wa Umwagiliaji na Maji. Wahitimu wa Vyuo hivyo wanatarajiwa kuingia katika soko la ajira kuanzia mwaka 2013/2014 na hivyo kuanza kupunguza tatizo la upungufu wa wataalamu. Vilevile, Halmashauri zinashauriwa kutumia wataalamu kutoka Sekta Binafsi na Taasisi katika kuandaa, kusanifu na kusimamia utekelezaji wa miradi. Matarajio ya Wizara ni kwamba utaratibu mpya wa bajeti kuanza mapema na kukamilika mwezi Juni utasaidia kuondoa tatizo la mtiririko wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 452,202, mbegu tani 60,000 na madawa tani 328,586. Hadi kufikia Machi 2013, tani 240,350 za mbolea na tani 30,443.0 za mbegu bora zilifikishwa kwa wakulima. Kati ya mbegu hizo, tani 22,403.9 zimezalishwa hapa nchini na tani 8,039.1 ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Kati ya mbegu zilizozalishwa hapa nchini, Wakala wa Mbegu za Kilimo *(ASA)* walizalisha tani 2,484 na tani 1,330 zilizalishwa kupitia utaratibu wa makubaliano na Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Vilevile, *ASA* ilizalisha miche bora ya matunda 287,000 na vipando bora vya muhogo 15,641,866. *ASA* pia ilishirikiana na Sekta Binafsi katika uzalishaji wa mbegu bora kwa kutumia mashamba yake ya mbegu. Katika msimu wa mwaka 2012/ 2013, *ASA* ilishirikiana na *Suba Agro Trading & Engineering*

*Company Limited* kuzalisha tani 2,018 za mbegu bora katika Shamba la Mbegu la Mbozi. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea kuhamasisha uzalishaji wa Mbegu za Daraja la Kuazimiwa *(Quality Declared Seeds - QDS)* ambapo tani 454.35 zilizalishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaazimia kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kufika tani 60,000 ifikapo mwaka 2014/2015. Ili kutimiza azima hiyo, *ASA* inaendelea kujenga uwezo wake wa kitaalamu ikiwa ni pamoja na kusomesha wataalamu watatu katika fani ya teknolojia ya mbegu kwa kiwango cha Shahada ya Uzamili, kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ya Msimba, Kilangali na Arusha; na kununua matrekta na mitambo ya kuvunia mbegu. Aidha, Maabara ya Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* imejengewa uwezo ili iweze kuwa na sifa ya kukagua mbegu kwa kiwango cha Kimataifa.

Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mbegu bora kwa kushirikisha Sekta Binafsi. Aidha, *ASA* itawezeshwa kuzalisha tani 4,000 za mbegu bora za nafaka na mboga mboga, pingili za muhogo 15,000,000 na miche ya matunda 300,000 katika mashamba yake na kwa kushirikiana na JKT, Magereza na wakulima binafsi kupitia Kilimo cha Mkataba. Aidha, kwa kushirikiana na Kampuni za Mbegu za *Suba Agro Trading & Engineering Company Limited* na *Highland Seed Growers* jumla ya tani 2,500 za mbegu za nafaka zitazalishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa nia ya kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji. Ruzuku ya mbolea ilifikia tani 126,118 ambapo wakulima 940,783 walinufaika. Aidha, jumla ya tani 10,741 za mbegu bora zikiwemo tani 8,278 za mahindi; tani 1,694 za mpunga; tani 402 za mtama na tani 366 za alizeti zilisambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

Wizara ilitoa ruzuku ya *acrepacks* 3,500,000 za madawa ya pamba, na lita 158,727 na tani 582 za madawa

ya korosho kwa wakulima wa Mikoa inayozalisha mazao hayo. Ruzuku ya uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya chai 1,568,966 na miche bora ya kahawa 1,926,889 ilitolewa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itawezesha upatikanaji wa tani 400,000 za mbolea, tani 40,000 za mbegu bora, miche milioni 40, tani 2,000 na lita 870,000 za madawa ya pamba na korosho kupitia ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kukabiliana na changamoto ya kuwepo kwa pembejeo zisizokidhi viwango vya ubora katika soko. Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea inakagua na kuchukua hatua za kisheria kwa Makampuni yanayosambaza mbolea zisizo na ubora ikiwa ni pamoja na kutoza faini na kufuta leseni za Makampuni na Mawakala wadanganyifu. Kwa mfano, Makampuni ya *Mohamed Enterprises Ltd* na *STACO* yalizuiliwa kuuza mbolea za aina ya *DAP* na *CAN* zilizoonekana kuwa na kasoro ya kutokidhi viwango vya ubora na kuamriwa kuzikusanya na kuziondoa sokoni kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa mazao ya mahindi na mpunga imekuwa ikitolewa kwa kutumia vocha ambapo mawakala walichaguliwa na Makampuni ya Pembejeo. Utaratibu huo uligubikwa na changamoto nyingi zikiwemo za vocha kuchelewa kuwafikia wakulima kutokana na kutowajibika kikamilifu kwa baadhi ya watendaji; baadhi ya mawakala na watendaji wasio waaminifu kuwarubuni wakulima; na baadhi ya makampuni kutofikisha pembejeo kwa wakati. Makampuni ambayo hayakufanya vizuri katika msimu huu hayataruhusiwa kufanya biashara ya pembejeo ya ruzuku.

Aidha, watendaji na mawakala wote waliohusika katika ubadhirifu wa pembejeo wanaendelea kuchukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria. Vilevile, Serikali imezuia malipo ya mawakala wote ambao ama kesi zao zinachunguzwa na vyombo vya dola au zipo Mahakamani mpaka hapo kesi hizo zitakapokwisha ili kuepusha kuendelea kupata hasara zaidi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imebuni mfumo mpya wa usambazaji wa pembejeo katika msimu 2013/2014 ambapo wakulima kupitia vikundi na Vyama vya Ushirika watapata mikopo ya muda mfupi na yenye riba nafuu kwa ajili ya kununulia pembejeo. Mfumo wa Vocha utaendelea kutumika katika maeneo yale tu ambayo mfumo huo haukuwa na changamoto nyingi. Ili kuongeza ufanisi katika jambo hili Wizara inaandaa semina itakayofanyika mwezi Mei, 2013, ambapo wadau wakiwemo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge, Taasisi za Fedha, Makampuni ya Pembejeo na Wawakilishi wa Wakulima watapata fursa kujadili mfumo huo kwa kina kabla haujaanza kutumika. Mjadala huu tunatarajia kuufanya tukiwa hapa hapa Bungeni Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea, yaani Tanzania Fertilizer Regulatory Authority – TFRA, ambayo inakagua na kuchukua hatua za kisheria, kwa Makampuni yanayosambaza mbolea zisizo na ubora ikiwa ni pamoja na kutoza faini na kufuta leseni za makampuni na mawakala wadanganyifu. Tayari makampuni yaliyodhihirika kuuza mbolea zisizo na ubora yamekwishaamriwa kuzikusanya na kuziondoa sokoni kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009 na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kugharamia mafunzo katika Vyuo vya Kilimo ili kufikia lengo la kuwa na Maafisa Ugani 15,082 wa Vijiji na Kata ifikapo mwaka 2015. Hadi kufikia mwaka 2013 kuna jumla ya Maafisa Ugani 7,974. Pamoja na Wizara kuendelea kugharamia mafunzo, hata hivyo baadhi ya vijana tarajali wanaohitimu wanakabiliwa na changamoto ya kutoajiriwa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013, jumla ya wahitimu 2,514 walikuwa hawajaajiriwa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Serikali inafanya juhudi kuhakikisha wahitimu hawa wanaajiriwa katika mwaka 2013/2014, na hili mtakuwa mmelisikia Waheshimiwa Wabunge wakati Waziri anayehusika na Utumishi alipowasilisha hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya Maafisa Ugani ambao utendaji wao hauridhishi kutokana na kutowajibika na usimamizi hafifu katika ngazi ya Halmashauri. Tathmini ya utekelezaji wa *ASDP* ilibaini kuwa Maafisa Ugani wengi hawatekelezi kazi zao za kuwaelekeza Wakulima ipasavyo licha ya kuwezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imewahimiza Maafisa Ugani kuandaa mipango kazi ikiwa ni pamoja na kila Afisa Ugani kuwa na Daftari la Kilimo. Chini ya utaratibu huu, Maafisa Ugani wa Wizara watafanya ukaguzi wa madaftari hayo na utendaji wa Maafisa Ugani mara kwa mara katika Halmashauri. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Wizara itashirikiana na TAMISEMI kuandaa sheria ndogo za mfano *(Model bylaws)* ambazo zitapitishwa na Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo. Shughuli hizo ni pamoja na Kilimo cha Mkataba, Kilimo cha Umwagiliaji, Kanuni bora za Kilimo, matumizi bora ya ardhi katika kilimo, utunzaji wa Daftari la Kilimo na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, tathmini imeonesha kuwa Mfumo wa Shamba Darasa umeongeza ufanisi katika kueneza teknolojia za kilimo kwa wakulima. Katika mwaka 2012/2013, Mashamba Darasa 16,330 yenye wakulima 344,986 (wanawake 138,461 na wanaume 206,525) yameanzishwa katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Manyara, Mara, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Mwanza. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhimiza matumizi ya Mashamba Darasa katika kueneza teknolojia bora za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imedahili na kugharamia mafunzo kwa wanachuo wa bweni 3,578 wakiwemo 1,145 wa mwaka wa kwanza na 2,433 wa mwaka wa pili. Aidha, Wagani Wanafunzi 2,433 wanaotarajia kuhitimu mafunzo mwezi Juni, 2013 walipelekwa katika Mikoa mbalimbali kwa madhumuni ya kufanya kazi za ugani kwa vitendo. Mitaala ya uzalishaji chakula na lishe na matumizi ya zana katika kilimo imeandaliwa na inatumika kwa vyuo vya Ilonga na Mlingano mtawalia. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itagharamia

mafunzo kwa wanachuo 3,500 katika ngazi ya stashahada na astashahada.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo na kuhamasisha Sekta Binafsi kuingiza nchini zana hizo. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2012, Sekta Binafsi iliingiza nchini jumla ya matrekta makubwa 782 na matrekta madogo ya mkono 949. Idadi ya matrekta makubwa yanayofanya kazi nchini ni 9,148 na madogo ni 5,520. Uingizaji wa matrekta makubwa na madogo umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya matumizi ya matrekta madogo ya mkono katika baadhi ya maeneo kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maopereta kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kuyatumia na mashamba kutotayarishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014, Wizara itawezesha mafunzo kwa maopereta 136 na viongozi wao kuhusu uendeshaji, matengenezo na utunzaji wa mashine za kuvuna mpunga *(Rice combine harvesters)* na usindikaji mpunga *(paddy mini plants)* katika skimu 14 za umwagiliaji. Vilevile, Wizara itaandaa mwongozo wa utumiaji na matengenezo wa mashine za kuvuna, kupandikiza na usindikaji wa mpunga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo mkopo wenye masharti nafuu ambao umewezesha kutekeleza mradi unaosimamiwa na SUMA JKT wenye matrekta 1,846 na zana zake, matrekta madogo ya mkono 400, pampu za umwagiliaji maji 1,100 na mtambo wa kuunganisha matrekta.

Ili kuwezesha wakulima kupata zana hizo, Serikali ilitoa punguzo kubwa la bei mwezi Januari, 2012 na kurahisisha masharti ya mkopo mwezi Julai 2012, matrekta yote yamekwishauzwa. Katika kuhakikisha vipuri vya matrekta yaliyouzwa na SUMA JKT vinapatikana kwa urahisi, Makampuni ya *Incar (T) Ltd, Hughes Motors (T) Ltd* na *Noble Motors (T) Ltd* yanauza vipuri vya matrekta hayo. Aidha, SUMA

JKT inafanya mazungumzo na Makampuni mengine ili waingize vipuri vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi, katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi Kujenga Taifa na TAMISEMI inafanya mazungumzo kwa ajili ya kukopa matrekta zaidi kutoka Serikali ya India. Matrekta hayo yatauzwa kwa wakulima kwa utaratibu uliotumiwa na SUMA JKT. Idadi ya matrekta itategemea makubaliano yatakayofikiwa kati ya Serikali za nchi zote mbili.

Mheshimiwa Spika, trekta la mkono *(power tiller)* ni zana muhimu na lina uwezo wa kufanya kazi nyingi katika mazingira ya shambani na nje ya shamba likiwa limeunganishwa na zana sahihi kwa kazi husika. Trekta hilo linaweza kulima, kuchavanga, kupiga haro, kupanda, kutengeneza matuta, kupalilia *(inter row weeding),* kunyunyizia dawa na kusafirisha mizigo. Aidha, trekta hilo linaweza kuendesha mitambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na vinu vya kusindika mazao kama muhogo, kupura mpunga, kupukuchua mahindi, kukatakata majani, kuendesha pampu za maji na hata kufua umeme.

Hapa nchini trekta la mkono limekuwa na mafanikio makubwa katika kuchavanga au kuvuruga udongo katika majaluba ya mpunga kwa kutumia rotaveta au padla. Ni muhimu shamba liwe na maji kiasi ili iwe rahisi kuchavanga. Mfano wa mafanikio makubwa katika matumizi ya trekta la mkono ni Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya ambayo ina matrekta ya mkono 1,400 yaliyonunuliwa na wakulima kwa mkopo kupitia *SACCOS* au kwa fedha taslimu. Matrekta hayo pia yamefanya vizuri katika kulima katika udongo wa kawaida kwa kutumia jembe la diski au plau.

Mheshimiwa Spika, matrekta madogo siyo mbadala wa matrekta makubwa. Matrekta madogo yakitumika kama ilivyoelezwa katika maelezo yaliyotangulia yanaweza kutoa mafanikio yaliyotarajiwa. Natoa wito kwa watumiaji wa

matrekta hayo kuzingatia maelekezo ya kitaalamu, kuajiri maopereta waliopata mafunzo na kutayarisha mashamba yao vizuri, kuondoa visiki na vizuizi vingine ili kuweza kutumia matrekta kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa wakulima kumudu kutumia matrekta kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vya zana za kilimo. Hata hivyo, utekelezaji wake umekuwa mgumu kutokana na Maafisa wa *TRA* kushindwa kutofautisha vipuri vya zana za kilimo na vipuri vya mashine na mitambo mingine. Ili kuondoa usumbufu wanaoupata waagizaji na watumiaji kutokana na hali hiyo, Wizara imeteua Wahandisi Kilimo wawili wenye ujuzi wa zana za kilimo ambao watasaidiana na Maafisa wa *TRA* kutambua vipuri vya zana za kilimo ambavyo vitapata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa siyo rahisi kila mkulima wa Tanzania kununua na kumiliki trekta, Serikali inahamasisha watu binafsi, Vyama vya Ushirika, *SACCOS* na *NGOs* zenye uwezo wa kuanzisha na kuendesha vituo vya kukodisha zana, kuanzisha vituo hivyo ili kuwezesha wakulima wengi zaidi nchini kupata huduma ya zana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa Shilingi bilioni 2.81 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Hadi tarehe 31 Machi 2013, Mfuko ulipata Shilingi bilioni 2.47 kutoka Serikalini na ulikusanya marejesho ya madeni ya Shilingi bilioni 2.98.

Hadi tarehe 31 Machi, 2013, Mfuko ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.38 kwa ajili ya kununulia matrekta makubwa yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.32; matrekta madogo yenye thamani ya Shilingi milioni 252; pembejeo za kilimo na mifugo (mbolea, vifungashio, viuatilifu na madawa ya mimea na mifugo) zenye thamani ya Shilingi milioni 681.50 na zana za umwagiliaji na usindikaji zenye thamani ya Shilingi milioni 118.50.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo utatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.40 ikiwemo mikopo ya matrekta makubwa na madogo, pembejeo za kilimo na mifugo, vifaa vya umwagiliaji na usindikaji. Changamoto kubwa iliyopo ni baadhi ya wakopaji kutorejesha mikopo kwa wakati na uwezo mdogo wa Mfuko ikilinganishwa na maombi yanayopokelewa. Hivyo natoa rai kwa wote waliokopa kurejesha mikopo kulingana na mikataba ili kutoa fursa kwa waombaji wengine kupata mikopo. Wananchi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge mnashauriwa kutumia fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea; Wizara ilisambaza lita 6,000 za kiuatilifu cha kudhibiti milipuko ya viwavijeshi katika Mikoa ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Geita, Dodoma, Morogoro na Tanga na kunusuru hekta 16,418 za mazao ya nafaka. Udhibiti wa panya ulifanyika katika Mikoa ya Morogoro, Lindi, Pwani, Tanga na Shinyanga ambapo kaya 350,335 zilipatiwa chambo chenye sumu kwa ajili ya kudhibiti milipuko hiyo. Vilevile, Wizara ilidhibiti nzige wekundu katika mbuga za Iku-Katavi, Malagarasi na Wembere ambapo hekta 5,700 zilizovamiwa na makundi ya nzige wekundu zilinyunyiziwa lita 2,500 za kiuatilifu. Aidha, Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa – *FAO* limesaidia kukodisha helikopta kwa ajili ya tathmini ya awali ya maeneo yenye nzige wekundu katika mwezi wa Novemba na Desemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa huduma za udhibiti wa visumbufu vya mimea unategemea huduma ya ndege kutoka kwenye mashirika ya kikanda ya kudhibiti nzige wekundu na nzige wa jangwani ambazo wakati mwingine hazipatikani wakati zinapohitajika, hali ambayo husababisha Wizara kutegemea kukodisha ndege kutoka sehemu nyingine. Ili kujenga uwezo wa Wizara wa kudhibiti milipuko ya visumbufu, Wizara itafufua Kituo cha Kilimo Anga kwa kukiwezesha kuwa na ndege na wataalamu. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imekamilisha viwango vya kiufundi (*Technical Specifications*) kwa ajili ya kutangaza zabuni ya

ununuzi wa ndege moja ya kunyunyizia viuatilifu. Aidha, Wizara itaweka utaratibu wa kuingia ubia na makampuni binafsi au Taasisi zinazotoa huduma kama hizo ili kukijengea uwezo Kituo cha Kilimo Anga.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti tatizo la madawa yasiyokidhi viwango vya ubora, Wizara ilikagua maduka 220 yanayouza viuatilifu katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Manyara na Tanga ambapo maduka 75 yalifungwa kutokana na makosa ya kwenda kinyume na Sheria ya Afya ya Mimea ya mwaka 1997 *(Plant Protection Act 1997).*

Aidha, ukaguzi wa mazao ulifanyika na hati 460 za kuingiza mazao na vyeti 2,645 vya usafi wa mazao vilitolewa kwa tani 46,073.2 za mazao zilizoingizwa nchini na tani 122,312.53 zilizosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa embe umekuwa ukikabiliwa na mashambulizi ya inzi wa embe. Tatizo hili limekuwa kubwa kiasi kwamba embe zetu sasa haziuziki katika baadhi ya nchi hususan Afrika ya Kusini ambapo wameweka karantini dhidi ya mdudu huyo. Ili kukabiliana na mdudu huyo, Wizara imeshirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kuandaa mpango mkakati wa miaka mitatu wa kudhibiti inzi wa embe. Kazi zinazotekelezwa chini ya Mpango huo ni pamoja na kutambua maeneo yaliyoathirika; kufundisha wakulima kanuni za kudhibiti mdudu ikiwemo usafi wa mashamba; kudhibiti madume ya inzi kwa kutumia kivutia wadudu aina ya *"methyl eugenol"*; na mitego ya kupunguza idadi ya inzi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaagiza madawa na mitego kwa ajili ya kudhibiti mdudu huyo na kufundisha Maafisa Ugani katika maeneo yaliyoathirika namna ya kudhibiti mdudu ili wasaidie wakulima.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya kuwepo viuatilifu bandia katika soko. Tatizo hili linatokana na baadhi ya wafanyabiashara wakubwa kushindwa kusimamia soko la viuatilifu vyao na hivyo wafanyabiashara wasio waaminifu kutengeneza viuatilifu bandia; watengenezaji wa

viuatilifu kutoweka alama za siri za bidhaa zao kwenye vibandiko na vifungashio vya viuatilifu na kuzitambulisha kwa Msajili wa Viuatilifu; uhamishaji wa viuatilifu kutoka katika vifungashio vya asili *(repackaging);* kusambaza viuatilifu kwenye vifungashio na vibandiko visivyo sahihi; na upungufu wa wakaguzi wenye uzoefu Mikoani na Wilayani ili kudhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyowekwa na Wizara ili kukabiliana na uwepo wa viuatilifu bandia ni pamoja na kuiwezesha *TPRI* kutekeleza majukumu yake ya utafiti wa viuatilifu kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara italeta mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya *TPRI* ya mwaka 1979 na Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997 *(Plant Protection Act)* ili kutenganisha majukumu ya utafiti, usajili, usimamizi na ukaguzi. Sheria hizo mbili zilivyo sasa zinaipa mamlaka *TPRI* kufanya majukumu yote ya utafiti, usajili, usimamizi na ukaguzi jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, viuatilifu ni sumu na hivyo uteketezaji wake unahitaji mitambo maalum, yaani *incinerators*. Mitambo hiyo haipo hapa nchini na hata nchi jirani. Wizara kupitia mradi wa *African Stockpile* iliweza kuteketeza viuatilifu ambavyo muda wake umekwisha. Kwa sasa viuatilifu visivyofaa vinawekwa sehemu maalum wakati utaratibu wa kuvipeleka nje ya nchi kwa ajili ya uteketezaji unafanywa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafiti wa Kilimo; katika mwaka 2012/2013 Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti na Sekta Binafsi ilipendekeza aina mpya 22 za mbegu bora za mazao kwa matumizi ya wakulima. Kati ya hizo, aina tatu za maharage, nne za viazi mviringo, mbili za kunde na mbili za mpunga zilitolewa na Vituo vya Utafiti vya Wizara na aina nane za mahindi, moja ya mtama na mbili za shayiri zilitolewa na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Vituo na Taasisi za Utafiti itaendelea kugundua na kutathmini aina za mbegu bora za mazao mbalimbali

zinazotoa mavuno mengi, zinazovumilia ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi mahitaji ya soko. Pia Wizara kupitia kwenye vituo vya utafiti itaanza kuingiza na kutathmini aina mbili za mboga, mbili za matunda na mbili za viungo zenye thamani kubwa kwenye skimu 10 za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilizalisha tani 17.4 za mbegu mama *(Breeders' seeds)* ili kukidhi mahitaji ya Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural Seed Agency - ASA)* kuweza kuzalisha mbegu za msingi *(foundation seed).* Vilevile, vipando bora vimeendelea kutolewa na Vituo vya Utafiti na kusambazwa kwa wakulima kwa mazao ya muhogo pingili 1,320,000 na viazi vitamu pingili 4,900,000.

Katika mwaka 2013/2014 Wizara kupitia vituo na Taasisi za utafiti, itaendelea kutafiti aina za mbegu bora za mazao mbalimbali, zinazotoa mavuno mengi, zinazovumilia ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi mahitaji ya soko. Wizara pia inatarajia kuzalisha tani 10 za mbegu mama *(breeders' seeds)* kwa mazao ya nafaka, mikunde, mboga mboga na mbegu za mafuta (alizeti, ufuta na karanga) na pingili milioni mbili za muhogo na viazi vitamu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kufanya utafiti wa bayoteknolojia kwa njia ya tishu *(tissue culture)* kwa lengo la kupata miche bora ya mazao mbalimbali kama mkonge, migomba, muhogo na viazi mviringo. Ili kuzalisha vipando hivyo kibiashara, Wizara inahimiza kampuni binafsi kuanzisha biashara ya uzalishaji wa vipando vya mazao kwa njia ya tishu. Kwa sasa kuna kampuni mbili ambazo zimeanza kuzalisha vipando hivyo ambazo ni *Crop Bioscience Solution Ltd* iliyoko Arusha inayozalisha vipando vya migomba na muhogo, na *Agrobiotech* ambayo iko katika hatua za mwisho za ujenzi wa maabara yake jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa unyanjano wa migomba unaendelea kuwa tatizo katika Kanda ya Ziwa na katika nchi za maziwa makuu. Ili kukabiliana na ugonjwa huo

Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa wakulima na Maafisa Ugani kuhusu njia sahihi ya kuutambua na mbinu za kuudhibiti, zikiwemo za kung'oa na kuchoma migomba iliyoathirika na kuanzisha vitalu vya kuzalisha miche ya migomba safi. Ugonjwa huu unaenea kutoka eneo moja hadi jingine kwa njia ya kusafirisha miche ya migomba.

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia ugonjwa huo usienee katika Mikoa mingine, Serikali inaendelea kuzuia usafirishaji wa miche ya migomba kutoka Kanda ya Ziwa kwenda katika maeneo ambayo bado hayajaathirika. Tatizo lingine lililojitokeza katika kudhibiti ugonjwa huo ni baadhi ya wakulima kutozingatia masharti wanayopewa na wataalamu. Katika mwaka 2013, Halmashauri zote za Mkoa wa Kagera zimeamua kwa pamoja kuhakikisha zinasimamia kanuni na masharti yanayotolewa na wataalamu ili kudhibiti ugonjwa huo. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri hizo kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima na Maafisa Ugani.

Aidha, uzoefu wa kudhibiti ugonjwa huo uliotumika katika nchi nyingine ikiwemo Uganda na baadhi ya Wilaya hapa nchini utatumika kutokomeza ugonjwa huo. Wizara pia itaendelea kufanya utafiti wa magonjwa ya mimea hususan kwa mazao ya migomba, muhogo na mahindi ili kuweza kupata ufumbuzi wa magonjwa yanayoathiri mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za Mimea *(NPGRC)* kilichoko Arusha kilikusanya na kuhifadhi vinasaba 285 vya aina ya mimea kutoka katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani. Kituo kiliweza kutoa nasaba za njugumawe, mtama, kunde na mahindi kwa ajili ya utafiti. Katika mwaka 2013/2014, kituo kinatarajia kukusanya na kuhifadhi nasaba za mpunga chakula na mpunga pori aina 300, na kutathmini mtama aina 33, kunde 20 na mbaazi 17.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia mradi wa *EAAPP* itaimarisha miundombinu ya utafiti na vitendea kazi katika Vituo vya Utafiti vya *KATRIN*, Ukiriguru, Uyole, Dakawa na Mikocheni. Jumla ya hekta 35 za miundombinu ya umwagiliaji

itajengwa katika Vituo vya *KATRIN* (25) na Ukiriguru (10) ili kufupisha muda unaotumika kutafiti teknolojia hasa uzalishaji wa aina mpya za mbegu bora za mazao. Aidha, jumla ya watafiti 18 wataendelea na masomo yao ya muda mrefu katika Vyuo Vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Watafiti 171 na kada nyingine watajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na ziara za mafunzo kwa kuzingatia fani zao.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali ya kwanza katika kuwezesha kilimo endelevu nchini. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa kuna hekta milioni 44 zinazofaa kwa uzalishaji wa mazao. Hata hivyo, eneo hilo limekuwa likipungua kutokana na kupanuka kwa shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi kama vile ujenzi wa makazi, hoteli, shule, uendelezaji wa miundombinu na uchimbaji wa madini.

Aidha, kumekuwepo na shughuli za kilimo zisizozingatia matumizi bora ya ardhi ambazo zinachangia kwa sehemu kubwa kuongezeka kwa tatizo la mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa vyanzo vya maji na mabadiliko ya tabianchi, mambo ambayo yamechangia kuendelea kupungua kwa maeneo yanayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Wizara inaandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kulinda ardhi ya kilimo ambayo italetwa hapa Bungeni. Sheria hiyo itaweka utaratibu wa kuitambua ardhi inayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali kwa kuzingatia sifa zake kitaalamu ikiwemo aina za udongo na mazao yanayostawi. Hatua hizo ni muhimu katika kufanikisha dhamira ya Serikali ya kulinda ardhi ya kilimo na kuwezesha watumiaji kuwa na hatimiliki zitakazokuwa chachu ya kuwekeza mitaji yao katika kuendeleza na kutunza ardhi ya kilimo.

Aidha, kuwepo kwa sheria inayolinda ardhi ya kilimo kutapunguza migogoro ya umiliki wa ardhi ya kilimo kwa kuwa ardhi husika itakuwa imeainishwa na kutengwa mahsusi kwa shughuli za kilimo pekee kama ilivyo kwa Sheria za Wanyamapori, Misitu, Ardhi Oevu na Madini.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara. Katika mwaka 2012/2013 uzalishaji wa mazao makuu ya biashara umeongezeka kwa viwango tofauti kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Mazao Makuu Asilia ya Biashara (Tani)

| Zao | 2011/2012 Uzalishaji | 2012/2013 Uzalishaji |
|---|---|---|
| Chai | 33,000 | 32,700** |
| Sukari | 260,054.70 | 286,380 |
| Tumbaku | 126,624 | 74,240 |
| Pamba | 225,938 | 357,000 |
| Pareto | 5,700 | 6,100 |
| Mkonge | 33,406 | 26,289 * |
| Kahawa | 33,219 | 65,556 |
| Korosho | 160,000 | 127,925 |

**Chanzo: Bodi za Mazao, 2013**

* Uzalishaji hadi Machi mwaka 2013.

** Matarajio ya uzalishaji

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa pamba umeongezeka kutokana na kupanda kwa bei katika msimu wa 2011/2012 na hivyo wakulima kuhamasika kuzalisha zaidi na hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutokana na msimu wa

2012/2013 kuangukia katika uzalishaji wa juu wa kahawa *(higher coffee cycle)* na hali nzuri ya hewa katika kanda za uzalishaji wa kahawa za Mbeya, Ruvuma na Kagera. Uzalishaji wa pareto umeongezeka kutokana na ongezeko la bei ya maua katika msimu wa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa sukari uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa miwa ya sukari kwa wakulima wadogo *(outgrowers)* na kwenye mashamba ya kiwanda cha sukari cha Kagera. Uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kutokana na hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayozalisha chai na bei nzuri iliyotolewa kwa wakulima katika mwaka 2012.

Aidha, uzalishaji wa mkonge unatarajiwa kuongezeka kufikia tani 40,000 kutokana na bei nzuri ya mkonge na bidhaa za mkonge iliyotokana na ongezeko la mahitaji. Aidha, uzalishaji wa korosho umepungua kutokana na kuyumba kwa soko la korosho katika msimu wa 2011/2012 na hivyo wakulima wengi kutokuwa na uwezo wa kununua viuatilifu na msimu wa 2012/2013 kuangukia katika msimu mdogo wa uzalishaji *(low yielding season).* Uzalishaji wa tumbaku pia umepungua kutokana na kuyumba kwa soko, mvua kuchelewa kuanza na kukatika mapema na kuvurugwa kwa utaratibu wa usambazaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia utendaji kazi wa Bodi za Mazao ya Korosho, Sukari, Pamba, Mkonge, Chai, Kahawa, Tumbaku, Pareto na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa lengo la kuhakikisha kuwa kila Bodi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Waraka wa Serikali wa mwaka 2006 uliorazinisha majukumu ya Bodi za Mazao unaelekeza Serikali kugharamia shughuli za usimamizi za Bodi za Mazao kwa asilimia 100 na majukumu mengine kuchangiwa na wadau. Ili kuongeza uwezo wa Bodi kusimamia kikamilifu majukumu yake, Wizara imeelekeza Bodi za Mazao kuanzisha mifuko ya hiari kwa ajili ya kugharamia majukumu ya pamoja na kutumia rasilimali zisizohamishika kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja kuhusu uwakilishi katika Bodi ya Wakurugenzi ya Kahawa na kanuni inayoruhusu uuzwaji wa kahawa mbichi. Serikali imefanya marekebisho katika Bodi ya Wakurugenzi wa Kahawa kwa kuteua Bodi mpya ya Wakurugenzi. Aidha, rasimu ya marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Kahawa ya mwaka 2012 inayozingatia kudhibiti uuzaji wa kahawa mbichi na kuhakikisha kwamba kahawa yote inayouzwa inachakatwa kwa lengo la kuhakikisha ubora wa kahawa ya Tanzania katika soko la kimataifa imeandaliwa. Rasimu hiyo inatarajiwa kujadiliwa kwenye Mkutano wa wadau wa kahawa mwezi Mei, 2013.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uchambuzi wa tumbaku unakabiliwa na upungufu wa wataalamu *(classfiers)* unaosababisha kuwepo kwa malalamiko kwa wakulima. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara inatarajia kuongeza ajira ya wataalamu katika fani ya uchambuzi na kuwajengea uwezo wale ambao wako tayari kwenye ajira. Vilevile, Wizara itaelekeza Bodi ya Tumbaku kuweka utaratibu wa kuwa na jopo la wateuzi kwa lengo la kushughulikia malalamiko ya wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu mbaya wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za tumbaku kupitia Vyama vya Ushirika hususan katika Mkoa wa Tabora ambao umesababisha wakulima kupata bei ndogo wasiyoitarajia. Wizara imemwomba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua mfumo mzima wa usambazaji wa pembejeo za tumbaku unaohusisha Vyama vya Ushirika na Taasisi za Fedha. Aidha, Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika ambaye ndiye mimi, ameteua Kamati maalumu itakayosimamia uboreshaji wa mfumo wa usambazaji wa pembejeo katika Mkoa wa Tabora na kuagiza mfumo mzima wa usambazaji wa pembejeo ukaguliwe na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika mazao ya bustani umeongezeka. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka hasa katika skimu za umwagiliaji maji ambapo vitunguu, njegere, kabichi na nyanya zimekuwa zikizalishwa. Wizara

inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani likiwemo zao la maua ambalo lina fursa za kuongeza uzalishaji katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. Aidha, kufunguliwa kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ni fursa nyingine itakayoongeza soko la maua. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama ilivyo katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)

| Zao | 2009/2010 | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 |
|---|---|---|---|---|
| Matunda | 3,297,910 | 3,751,170 | 3,938,730 | 4,096,280 |
| Mboga | 766,570 | 858,740 | 901,680 | 937,750 |
| Maua | 8,670 | 9,100 | 9,850 | 10,200 |
| Viungo | 7,150 | 7,370 | 8,125 | |

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sekta Binafsi kuendelea kuhamasika katika kilimo cha mazao ya mbegu za mafuta hususan alizeti, ufuta, karanga na mawese, uzalishaji umeongezeka kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3. Uzalishaji wa mazao hayo unafanyika kwa wingi katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Manyara, Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Kigoma, Katavi, Njombe na Mtwara. Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya tathmini ya uzalishaji na mahitaji ya mafuta ya kula.

Aidha Wizara inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya tathmini ya uzalishaji na mahitaji ya mafuta ya kula. Matokeo ya tathmini hiyo yataisaidia Serikali kuamua kiwango cha uagizaji wa mafuta ghafi ya kula kutoka nje kwa lengo la kulinda soko la ndani.

Jedwali Na. 3: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)

| Na. | Zao | 2010/2011 | 2011/2012 | 2012/2013 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Alizeti | 786,902 | 1,125,000 | 2,625,000 |
| 2 | Karanga | 651,397 | 810,000 | 1,425,000 |
| 3 | Ufuta | 357,162 | 456,000 | 1,050,000 |
| 4 | Mawese | 17,000 | 24,880 | 40,500 |

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ni kivutio kikubwa katika kuchochea uzalishaji. Kwa kiasi kikubwa masoko ya mazao makuu ya biashara yana mfumo wa soko unaosimamiwa na Bodi za Mazao husika. Hata hivyo, mfumo huo bado unategemea uuzaji wa mazao nje ambao unaathiriwa na mabadiliko ya bei ya mara kwa mara katika Soko la Dunia.

Aidha, mazao ya chakula, bustani na mbegu za mafuta hayana mfumo rasmi wa soko unaowezesha ushindani. Kutokana na hali hiyo, wanunuzi hununua mazao kutoka kwa wakulima kupitia mfumo usio rasmi ikiwa ni pamoja na kununua mazao yakiwa shambani. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa miundombinu ya masoko.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuimarisha Bodi za Mazao ili zitekeleze majukumu yake ya usimamizi na ufuatiliaji wa masoko ya mazao husika kikamilifu, kuzirejea sheria za mazao na kanuni zake kwa lengo la kuondoa upungufu uliopo, kuhamasisha uongezaji thamani ya mazao, kuimarisha miundombinu ya masoko na kuanzisha Soko la Bidhaa za Mazao *(Commodity Exchange).*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Bodi za Mazao inaendelea kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa mazao makuu ya biashara. Kwa mfano, Wizara imesaini Mkataba wa Makubaliano *(MoU)* na nchi ya China tarehe 24 Machi, 2013 utakaowezesha Tanzania kuuza tumbaku nchini China pasipo kuwa na vikwazo hususan vinavyohusu afya ya mimea *(Phytosanitary).* Hatua hii imefikiwa baada ya Nchi ya China kuridhia ubora wa tumbaku ya Tanzania. Tutafanya hivyo pia kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya kupanda na kushuka kwa bei za mazao ya biashara katika Soko la Dunia, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mazao husika inaandaa utaratibu wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia Bei za Mazao *(Price Stabilization Fund)* kwa ajili ya kusaidia wakulima pindi bei ya mazao inaposhuka katika Soko

la Dunia. Tayari Wizara imekamilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia Bei za Mazao ya Biashara. Rasimu hiyo itajadiliwa na wadau mwezi Mei, 2013 na baadaye kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Waheshimiwa Wabunge pia mtapata nafasi ya kuijadili rasimu hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri katika biashara ya mazao. Mfumo huu ulianza vizuri ambapo wakulima walipata malipo ya kwanza, ya pili na ya tatu *(majaliwa)*. Hata hivyo, mfumo huo unakabiliwa na changamoto zinazotokana na upotoshaji unaofanywa na walanguzi na madalali wanaojinufaisha na ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima kwa kutumia mfumo usio rasmi.

Aidha, watendaji wasio waaminifu wa Vyama vya Ushirika, wasimamizi wa maghala na Taasisi za Fedha wamechangia kudhoofisha mfumo huo. Serikali itaendelea kuuboresha mfumo huo ili kuondoa kasoro zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wanaouhujumu.

Katika mwaka 2013/2014 Wizara itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani ili kuondoa kasoro zote zilizojitokeza katika kuutekeleza. Aidha, Serikali inafanya mapitio ya mjengeko wa bei, yaani *price structure* unaotumika katika minada ili kuondoa makato mbalimbali yasiyo ya kisheria ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha kupungua kwa bei anayopata mkulima na hasa katika Soko la Korosho.

Mheshimiwa Spika, soko la miwa inayozalishwa na wakulima wadogo linakabiliwa na changamoto ya miwa kutochukuliwa kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uwezo mdogo wa viwanda vya kusindika miwa na hivyo kushusha kiwango cha ubora wa miwa. Hali hiyo husababisha wakulima wadogo walioingia mikataba na viwanda vya kusindika miwa kupata hasara.

Ili kupata ufumbuzi wa changamoto hiyo, Wizara itashirikiana na wadau wakiwemo Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma *(CHC),* wamiliki wa viwanda, wakulima na Halmashauri za Wilaya katika maeneo husika ili kuangalia uwezekano wa kujenga viwanda vingine katika maeneo hayo. Aidha, Wizara itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo wa miwa wanaozunguka viwanda kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Serikali iliondoa vikwazo vya kuuza nafaka nje ya nchi *(export ban)* baada ya kubainika kuwa vilikuwa havisaidii kuzuia uvushaji wa nafaka nje ya nchi. Aidha, uzuiaji huo ulikuwa unachangia kudumaza uzalishaji wa mazao hayo kwa kuwa bei aliyokuwa anapata mkulima ilikuwa ya chini ikilinganishwa na gharama za uzalishaji. Hatua ya kuondoa vikwazo vya kuuza nafaka nje imesaidia kuongeza wastani wa bei ya mahindi kwa asilimia 100 kutoka Sh. 30,000/= hadi Sh. 60,000/= kwa gunia la kilo 100. Hata hivyo, matokeo ya bei nzuri yamesababisha wakulima wengi kuuza mpaka akiba yao ya chakula. Natoa wito kwa wakulima nchini kuzalisha kwa wingi, kuuza ziada tu na kujiwekea akiba ya kutosha mahitaji ya kaya. Hata hivyo, tutaendelea kutoweka zuio la kuuza mazao kwa wakulima jinsi wanavyoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2013, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ulinunua jumla ya tani 71,389.002 za nafaka (mahindi tani 67,695.974 na mtama tani 3,693.028) sawa na asilimia 35.7 ya lengo la kununua tani 200,000 na kufanya kiasi cha nafaka kilichokuwa kimehifadhiwa kufikia tani 137,613.045 kabla ya mauzo.

Katika mwaka 2013/2014, *NFRA* itawezeshwa kununua tani 250,000 za nafaka kuanzia mwezi Julai, 2013 kutoka kwa wakulima kwa bei ya soko. Ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao, *NFRA* inajenga ghala lenye ukubwa wa kuhifadhi tani 5,000 katika Wilaya ya Songea. Katika mwaka 2013/2014, ghala la kuhifadhi tani 5,000 litajengwa katika Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mradi wa *DASIP* imekamilisha usanifu wa miundombinu ya Masoko saba ya kimkakati *(Strategic Markets)* katika maeneo ya Busoka (Kahama), Kabanga (Ngara), Remagwe (Tarime), Nkwenda na Murongo (Karagwe), Mtukula (Misenyi) na Mnanila (Kasulu). Utaratibu wa Zabuni za kutafuta wakandarasi wa ujenzi wa masoko hayo unaendelea.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Finland na Norway inaandaa utaratibu wa kutumia mfumo wa *mobile farming (m-farming)* unaotumia simu za viganjani kwa ajili ya kuwezesha wakulima kupata taarifa za masoko, pembejeo za kilimo na huduma zingine za ugani.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu wakulima wa zao la chai katika mashamba ya Lupembe wamekuwa wakikosa soko la uhakika la majani mabichi ya chai. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kwa kushirikiana na wadau, imehamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya chai. Kutokana na juhudi hizo, Mufindi Tea Company – MTC imejenga kiwanda katika eneo la Lupembe ambacho kimeanza kufanya kazi mwezi Novemba 2012. Jitihada hizo zimesaidia wakulima wadogo kupata soko la uhakika la majani mabichi ya chai.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi Kilele ya Mazao ya Mboga na Matunda *(Tanzania Horticultural Association - TAHA)* inaendelea kujenga vituo vya kuhifadhi na kukusanya mboga na matunda wilayani Lushoto kwa ubia na Vikundi vya Wakulima. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya usindikaji (*post harvest handling technologies)*; ufungashaji na usindikaji kwa ubia na Vikundi vya Wakulima na Sekta Binafsi kama vile ujenzi wa *green houses* nne katika mikoa ya Njombe na Morogoro na Vituo viwili vya kukusanya mazao ya mboga na matunda; na kujenga kiwanda cha kati cha kusindika muhogo katika mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeikabidhi Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kinu cha kusagisha mahindi cha Iringa. Kinu hicho kina uwezo wa kusagisha mahindi tani 60 kwa siku. Katika mwaka 2013/2014, Bodi itaanza kutumia kinu hicho kibiashara kwa kushirikiana na *NFRA* kusagisha mahindi. Utekelezaji huo utaiwezesha Bodi kujiimarisha kimapato na kiutendaji kutokana na tozo la usagishaji; kuwezesha ukarabati mdogo wa kinu na vihenge; kudhibiti matumizi mabaya ya mahindi ya msaada kwa kusambaza unga badala ya mahindi; na kutoa ajira. Aidha, Bodi imepanga kutumia mali ilizokabidhiwa kwa kuingia ubia na Sekta Binafsi *(PPP).*

Mheshimiwa Spika, Wizara inahamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kuongeza thamani ya mazao mbalimbali. Katika jitihada hizo, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(National Social Security Fund – NSSF)* umeanzisha mpango wa kuwezesha makampuni binafsi yenye nia ya kuwekeza kwenye viwanda vya nguo kwa lengo la kuongeza thamani katika zao la pamba kwa kuchangia asilimia 60 na asilimia 40 iliyobaki kuchangiwa na wenye viwanda hivyo. Wizara itaendelea kuhamasisha makampuni yanayotaka kuwekeza katika Sekta ya Kilimo kujitokeza ili kutumia vizuri fursa hiyo na wenzetu wa *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Benki ya *TIB Development Bank* imeonesha nia ya kuwezesha Chama cha Ushirika cha *TANECU* kujenga kiwanda cha kubangua korosho. Wizara pia inawezesha vikundi 20 vyenye jumla ya wakulima 631 kununua mtambo wa kusindika muhogo katika Mkoa wa Mtwara, vikundi 11 vya wasindikaji wa alizeti vyenye wakulima 360 kununua mtambo wa kusindika alizeti na skimu 14 kupata mashine zenye uwezo wa kukoboa tani 5 hadi 30 za mpunga kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha ama kujiunga na Vyama vya Ushirika kupitia kampeni zilizofanyika Mikoani. Jumla ya Vikundi 62 vyenye vijana wanaume 536 na wanawake 861 vimefikiwa katika mkoa wa Singida. Aidha, uhamasishaji pia umefanyika

katika Kata 22 za Mkoa wa Dodoma na 58 za Mkoa wa Shinyanga kuanzisha au kurejea katika vyama vyao vya ushirika ambavyo walivitelekeza awali. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya SHIRECU, KACU, RIVACU, NJOLUMA na IFCU ilifanya uhamasishaji kwa wanaushirika katika vyama 248 mkoani Shinyanga, Vyama 25 mkoani Manyara, Vyama 39 mkoani Njombe na Vyama 54 mkoani Iringa kwa lengo la kufufua na kuimarisha Vyama vya Msingi ili viweze kuwahudumia wakulima katika soko la mazao yao na usambazaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa ushirika 57 kutoka mikoa ya Mwanza, Iringa, Njombe, Dodoma, Shinyanga, Manyara na Geita walipatiwa mafunzo maalumu juu ya mbinu za uhamasishaji pamoja na kuandaa mipango kazi yao kwa ajili ya kutekeleza jukumu la uhamasishaji na uelimishaji wa wanaushirika na wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa ushirika. Kutokana na uhamasishaji uliofanyika, hadi kufikia Machi, 2013, jumla ya Vyama vipya vya Ushirika vya Msingi 195 na Chama cha Ubia wa Wakulima wa Tumbaku Iringa *(Iringa Tobacco Growers' Joint Enterprise)* viliundwa na kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika nchini hususan katika skimu za umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya ushirika na ujasiriamali kwa wanachama, watendaji na viongozi wa skimu.

Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza tija na ushirikishwaji wa wakulima katika matumizi na usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Aidha, Wizara itasimamia uundwaji na uendeshaji wa Kamati za Wilaya za Uhamasishaji wa Uanzishaji wa Vyama vya Ushirika na kuwashirikisha Wakurugenzi wa Halmashauri na Madiwani katika uhamasishaji huo. Lengo ni kuwezesha ushirika kuingizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya na kupanua wigo wa ushirika ili uweze kuenea katika sekta nyingi zaidi za uchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha uendeshaji wa SACCOS na Benki za Ushirika. Vilevile, miongozo minne ya uendeshaji na usimamizi wa SACCOS (*SACCOS Regulations, Off-Site Supervision Manual, On-Site Supervision Manual na Information Sharing Scheme*) imeandaliwa. Wizara pia imetoa mafunzo ya uendeshaji wa SACCOS kwa Viongozi na Watendaji 304 kutoka *SACCOS* 76 na Maafisa Ushirika 50 wa Kanda ya Ziwa, Mashariki (Dar es Salaam na Pwani), Nyanda za Juu Kusini na Kusini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa mafunzo ya ukaguzi na usimamizi wa *SACCOS* kwa Maofisa Ushirika 66; Wakufunzi wawili kutoka *MUCCoBS*; Mkaguzi mmoja kutoka *COASCO* na mmoja kutoka *SCCULT*. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 300 kuhusu usimamizi na ukaguzi wa *SACCOS* nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika, Uchunguzi na Ukaguzi Maalumu umefanyika katika ngazi mbalimbali za Vyama vya Ushirika kuanzia Shirikisho la Vyama vya Ushirika *(TFC),* Chama Kilele cha Ushirika wa Tumbaku *(TTCA),* Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SCCULT),* Vyama Vikuu vya Ushirika vya *KNCU (1984) Ltd, WETCU Ltd, CETCU Ltd, TANECU Ltd,* Vyama vya Ushirika vya Msingi 192 vinavyoshughulika na zao la Tumbaku katika Mkoa wa Tabora na 14 vya mkoa wa Singida; Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Mazao *(AMCOS)* 97 mkoani Pwani na 18 vya Wilaya ya Tunduru; Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vya Wazalendo, Kurugenzi Njombe, Mpwapwa *Teachers*, Fune, Gogogo, Luiche, Kisesa na *CHAWAMPU AMCOS.* Vyote hivyo vimefanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa za uchunguzi na ukaguzi kwa vyama hivyo zimeonesha ubadhirifu wa fedha na mali za wanaushirika. Taarifa zimewasilishwa kwenye Bodi za Uongozi wa vyama na baadhi zimewasilishwa kwenye Mikutano Mikuu ya Vyama husika, na hatua stahiki zimechukuliwa. Pale ambapo vyama havitachukua hatua, Serikali itachukua jukumu hili na kuhakikisha kwamba wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano,

taarifa ya uchunguzi na ukaguzi ya Chama Kikuu cha Ushirika cha *WETCU Ltd* imewasilishwa kwenye Mkutano Mkuu Maalumu na wanachama wamefikia uamuzi wa kuwajibisha Bodi ya Uongozi wa *WETCU* Ltd kwa kuiondoa madarakani na kuteua Bodi ya Uongozi ya muda.

Aidha, viongozi na watendaji 883 wa *AMCOS 97* Mkoani Pwani waliondolewa madarakani na kupewa tozo *(surcharge)* kutokana na tuhuma za ubadhirifu ili kufidia hasara walizosababisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kulipatia ruzuku Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* ili kuimarisha shughuli za ukaguzi wa vyama ambapo Vyama vya Ushirika 3,872 vimekaguliwa ikiwa ni pamoja na *TFC*, Vyama Vikuu 34, *AMCOS* 1,541, *SACCOS* 2,217, Benki ya Ushirika moja na Vyama vya Ushirika wa aina nyingine 79. Katika jitihada za kuboresha *COASCO*, Wizara imeanza kushughulikia malalamiko kuhusu utendaji wake kwa kuunda Tume ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa kufanya uchunguzi maalumu kwa Vyama vya Ushirika 500; kukagua vyama 7,000; kutoa miongozo ya ukaguzi; na kutoa mafunzo kazini kwa Maafisa Ushirika 200 wa Halmashauri za Wilaya ili kuimarisha ukaguzi na udhibiti katika vyama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara imetoa mafunzo kwa Vyama vya Msingi 67 vinavyounda *MICU, MBOCU* na *ISAYULA* Mkoani Mbeya kuhusu maandalizi ya kuwa wasambazaji wa pembejeo sambamba na kuandaliwa kwa miongozo ya kusimamia Vyama vya Ushirika vya Mazao *(AMCOS)* wakati wa kutekeleza jukumu la kusambaza pembejeo. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaandaa na kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na wanachama wa Vyama vya Ushirika 3,000 kuhusu matumizi ya fedha za mikopo ya pembejeo na ujasiriamali. Aidha, Wizara itawezesha Vyama vya Ushirika vya Msingi 2,000

kupata mikopo ya pembejeo kutoka katika mabenki na taasisi mbalimbali za fedha.

Mheshimiwa Spika, Asasi za Ushirika. *Wizara imeendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) na Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT) katika kuhamasisha uanzishaji na uendelezaji wa ushirika nchini. Wizara kwa kushirikiana na TFC iliratibu na kusimamia Mkutano wa Uanzishwaji wa Benki ya Kitaifa ya Ushirika ambapo wajumbe wa Bodi ya muda ya Uanzishwaji wa Benki waliteuliwa. Zoezi la uhamasishaji wa kukuza mtaji wa Benki hiyo limeendelea kufanyika kwa vyama vya ushirika vya mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imesimamia uchaguzi katika Vyama vya Ushirika vya Msingi ili kuwapata viongozi wenye sifa katika Benki ya Ushirika wa Wakulima Kagera *(Kagera Farmers Cooperatives Bank – KFCB)* na Benki ya Ushirika Kilimanjaro *(Kilimanjaro Cooperative Bank Ltd – KCBL).* Aidha, masharti ya uendeshaji wa Benki hizo za Ushirika yamepitiwa na kuidhinishwa na Viongozi wa Bodi za Benki hizo ili yaweze kusajiliwa. Wizara pia kwa kushirikiana na TAMISEMI iliratibu na kusimamia mikutano mikuu ya Vyama vya Ushirika 110 ikiwa ni pamoja na *KFCB, KCBL, TFC, CORECU* na kuratibu mafunzo kwa Bodi mpya ya Benki ya *KFCB* kuhusu majukumu ya Benki na usimamizi wa Benki kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 3,750 kuhusu ukusanyaji wa takwimu za kilimo kwa kutumia mtandao wa *TEHAMA* wa *Local Government Monitoring Database System* – LGMD2 katika mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Katavi, Njombe, Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Tabora na Singida. Katika mwaka 2013/2014, mafunzo kuhusu mfumo huo yatatolewa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga na baada ya mafunzo hayo mfumo huo utaanza kutumika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi za hali ya ushirika nchini, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za ushirika wa "*Cooperatives Data Analysis System – CODAS*" kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika wa Wilaya za Mikoa ya Kigoma, Tabora, Arusha, Manyara, Dodoma na Singida ikiwa ni pamoja na kutoa kompyuta moja kwa kila mkoa.

Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 50 kutoka Mikoa ya Mtwara, Lindi, Simiyu, Geita, Katavi na Njombe kuhusu ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za ushirika na kila mkoa utapewa kompyuta moja.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013 ilipitishwa na Serikali tarehe 1 Machi, 2013. Wizara imeanza kutafsiri Sera hiyo katika lugha ya Kiswahili na baada ya hapo itachapishwa na kusambazwa.

Aidha, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 ili kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ulisomwa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge kwa mara ya kwanza tarehe 30/01/2013. Vilevile, Rasimu ya Muswada wa kutunga Sheria ya Umwagiliaji, nayo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea; Sheria ya Taasisi ya Viuatilifu vya Ukanda wa Kitropiki *(Tropical Pesticides Research Institute-TPRI)* ya mwaka 1979; Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo Na. 9 ya Mwaka 1994; na Sheria ya Mamlaka ya Kuendeleza Bonde la Mto Rufiji *(RUBADA)* ya mwaka 1975 kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata utaratibu wa kuziwasilisha Bungeni. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaandaa Muswada wa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Ardhi ya Kilimo na Sheria ya Kilimo cha Mikataba ili kuhakikisha kwamba ardhi inayofaa kwa kilimo inalindwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(SAGCOT),* Wizara imeweka kipaumbele katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya mahindi, mpunga na sukari ili kujitosheleza kwa chakula na kukidhi mahitaji ya soko la nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na nchi za *SADC*. Wizara inahamasisha uwekezaji mkubwa katika uzalishaji wa mazao hayo ili wawekezaji washirikiane na wakulima wadogo kuzalisha kwa kutumia teknolojia bora na kuhakikisha wakulima wanapata soko la mazao ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, makampuni 300 ya wawekezaji wa ndani na nje yameonesha nia ya kuwekeza nchini na yamejiandikisha katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na *SAGCOT center*. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na *TIC* imeainisha maeneo ya uwekezaji kwa kuanzia na mabonde ya Kilombero, Rufiji, Malagarasi na Ziwa Nyasa yanayofaa kwa kilimo cha mpunga na miwa.

Lengo ni kupata mashamba makubwa 16 kwa ajili ya uzalishaji wa sukari nchini na mashamba makubwa tisa kwa ajili ya kilimo cha mpunga. Kwa kutumia mbinu ya kilimo cha mashamba makubwa na ya wakulima wadogo wanaozunguka mashamba hayo *(Nucleus and Outgrowers Model)* mahusiano yanayojengwa yanawezesha wakulima wadogo kupata elimu, pembejeo, mitaji na zana. Katika kuwashirikisha wakulima wadogo, Wizara itakarabati miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo ili kuwezesha wakulima kuzalisha kwa tija zaidi baada ya kupata elimu ya mbinu za kilimo bora. Katika uwekezaji huo, nasisitiza kwamba wakulima wakubwa hawatakuwa mbadala wa wakulima wadogo wala ardhi ya wakulima wadogo haitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, shamba la *Kilombero Plantations Limited (KPL)* la Mngeta limeendelea kuzalisha mpunga kwa tija na mwekezaji amewekeza katika miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 215 ili kuwezesha kuzalisha mpunga mara mbili kwa mwaka. Lengo ni kuwekeza katika

miundombinu ya umwagiliaji kufikia hekta 3,000. Aidha, katika mwaka 2012/2013 kampuni ya KPL kwa kushirikiana na Mradi wa *Feed the Future* unaofadhiliwa na *USAID, Norfund*, na wawekezaji wa Yara na Syngenta imeendelea kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga kwa kutumia mbinu ya *Systems of Rice Intensification (SRI)* kwa wakulima wadogo 3,000 ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mpunga na hivyo kufikia wakulima zaidi ya 4,600 hadi sasa.

Lengo ni kufikia wakulima 20,000 ifikapo mwaka 2015. Wakulima hao wanaotoka katika vijiji vya Mngeta, Mkangawalo, Njage, Merera, Chita, Udagaji, Mgugwe, Ikule, Mchombe na Lukolongo wamepata mafunzo, pembejeo na zana bora. Katika maeneo hayo uzalishaji wa mpunga umefikia zaidi ya tani nane kwa hekta.

Mheshimiwa Spika, mashamba mengine makubwa yanatarajiwa kuanzishwa katika eneo la Mpanga-Ngalimila wilayani Kilombero na Lukulilo wilayani Rufiji. Wizara kwa kushirikiana na *USAID* imeanza upembuzi yakinifu na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika vijiji vinavyozunguka shamba la Ngalimila. Shamba hilo linalozungukwa na vijiji vya Mpanga, Ngalimila, Utengule, Ipugasa, Viwanja Sitini na Ngombo lina jumla ya hekta 31,500 na litanufaisha zaidi ya kaya 10,000 za wakulima wadogo. Maeneo mengine yataendelezwa kadiri ardhi inavyopatikana kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uzalishaji wa sukari, Serikali inafanya majadiliano na mwekezaji wa *Eco-Energy* ambaye ameonesha nia ya kuwekeza katika mradi wa kuzalisha miwa huko Bagamoyo. Mradi huo wenye hekta 7,800 unatarajiwa kuzalisha tani 150,000 za sukari, mita za ujazo 11,000 za *ethanol* na Megawati 10 za umeme. Mradi huo pia utahusisha uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 3,000 za wakulima wadogo 1,500 wa vijijji vya Kiwangwa na Matipwili ambao watawezeshwa kuanzisha mashamba ya kibiashara ya kilimo cha miwa chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa *SAGCOT, RUBADA* imekuwa ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya zilizopo katika eneo la Bonde la Mto Rufiji kuainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji katika Wilaya za Rufiji, Morogoro Vijijini, Kilombero na Mkuranga. Maeneo yaliyoainishwa ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Maeneo yaliyoainishwa kwa Uwekezaji katika Bonde la Mto Rufiji.

| **Zao** | **Mkoa** | **Wilaya** | **Hekta** |
|---|---|---|---|
| Miwa | Pwani | Rufiji | 62,265.78 |
| Morogoro | Morogoro | Vijijini | 21,000.00 |
| Mpunga | Morogoro | Kilombero | 16,328.00 |
| | | Ulanga | 5,000.00 |
| | Pwani | Rufiji | 8,222.20 |
| Muhogo | Pwani | Rufiji | 1,805.00 |
| Mtama | Pwani | Rufiji | 13,481.55 |
| Mahindi | Pwani | Rufiji | 9,119.20 |
| Michikichi | Pwani | Mkuranga | 7,110.00 |
| Ufuta | Morogoro | Morogoro vijijini | 4,720.00 |
| **JUMLA** | | | **50,050.00** |

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wamekuwa wakikimbilia mijini na kuacha kazi za uzalishaji wa mazao ya kilimo vijijini kutokana na kukosa motisha na uwezo mdogo wa uwekezaji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imekamilisha andiko la namna ya kuwavutia vijana kujiajiri katika kilimo cha kibiashara. Andiko hilo linatumika kuandaa programu ya kuwezesha vijana kujiajiri katika kilimo kwa kushirikisha wadau wote. Aidha, wakati programu inakamilishwa, tayari baadhi ya vijana wamekwishaanza kujiajiri katika kilimo kama ifuatavyo:-

Wahitimu 10 wa Vyuo Vikuu mbalimbali hapa nchini wamejiunga pamoja katika kijiji cha Isaka – Malilo – Igunga na tayari wamepewa ekari 150 wanazotumia kulima zao la alizeti kibiashara. Wizara nayo imewawezesha kwa

kuwapatia chakula na pampu mbili kwa ajili ya kuwahakikishia kupata maji kwa ajili ya umwagiliaji;

*Home Vegetable Group* – walioko Arusha, wanazalisha mboga mboga na mahindi machanga. Kikundi kina mtandao wa wakulima 1,000 na wanazalisha mazao hayo na kuyasafirisha nje ya nchi;

Kikundi kingine ni cha vijana katika Mkoa wa Singida, kimewezeshwa kulima zao la alizeti kibiashara katika eneo la hekta 200; na kipo pia kikundi *Big Power Group* katika Wilaya ya Kibondo ni kikundi cha vijana wanaolima muhogo kibiashara. Sasa wanasaidiwa teknolojia ya kuchakata muhogo ili waweze kuuza katika hali ambayo tayari umesindikwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *RUBADA* imejenga Kambi ya Vijana ya Mkongo *(Mkongo Youth Centre)* iliyopo eneo la Mkongo Wilayani Rufiji watakaojishughulisha na kilimo. Kambi hiyo ina uwezo wa kuchukua vijana 250 na itaanza na vijana 50 mwezi Mei, 2013. Vijana hao watapatiwa maeneo yenye ukubwa wa ekari tano kila mmoja na watalima mazao yenye thamani kubwa *(high value crops).* Hekta 528 zimetengwa kwa ajili ya kuwapatia ardhi ili kuwawezesha kuanza kilimo cha kibiashara.

Aidha, utaratibu umewekwa kupitia programu hiyo kuwawezesha kulipia gharama za uendeshaji kutokana na mapato ya sehemu ya mauzo ya mazao watakayolima. Wizara, inaandaa utaratibu wa kuwapatia maeneo ya ardhi, mikopo ya pembejeo kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na kuwaunganisha na mabenki wahitimu wa *SUA* na Vyuo vya Kilimo wenye nia ya kujiajiri katika kilimo kupitia Mpango wa *SAGCOT*.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *DASIP* ilitoa mafunzo ya kilimo na ufugaji bora kwa vijana 179,698 na kuwawezesha kupata ajira katika miradi ya jamii, teknolojia za kilimo na mifugo na kuanzisha mashamba na ufugaji. Kati ya vijana hao, 1,669 wameajiriwa kwenye miradi ya jamii, 1,043 katika

miradi ya teknolojia za kilimo na 176,986 wameanzisha mashamba ya kilimo na ufugaji bora. Tutaendelea na juhudi hizi katika mwaka huu.

Vijana walioajiriwa katika miradi ya jamii ni: wasimamizi wa majosho 429, wakusanya mapato na walinzi 315 katika masoko, walinzi katika maghala 85, wafugaji wa samaki 90 na wakulima wa mpunga na mboga mboga 750 katika skimu ndogo za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika*,* katika miradi ya teknolojia za kilimo na mifugo, vijana 490 wameajiriwa kuendesha *power tillers,* 308 kuendesha mashine za kusaga nafaka, 27 kuendesha mashine za kukamua mafuta, 91 kuendesha mashine za kukoboa kahawa, 27 wasimamizi wa mashine za kusindika matunda na 100 wameajiriwa kuendesha mashine za kuchakata muhogo.

Mheshimiwa Spika*, a*wamu ya kwanza ya *ASDP* inakamilika mwezi Juni, 2013. Tathmini za uwekezaji wa *ASDP* katika kilimo cha umwagiliaji na uendelezaji wa huduma za ugani zimeonesha kuwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji umewezesha upatikanaji wa maji kama pembejeo namba moja kwa ajili ya mahitaji ya mazao. Upatikanaji wa maji na pembejeo nyingine muhimu uliongeza tija katika zao la mpunga kutoka wastani wa tani 1.5 hadi tani 4.5 kwa hekta katika maeneo la wakulima wadogo. Ongezeko hilo limeimarisha upatikanaji wa chakula nchini na kuongeza vyanzo vya mapato ya wakulima. Aidha, uwekezaji wa *ASDP* umeimarisha utoaji wa huduma za ugani kupitia mfumo wa Shamba Darasa ambao umeongeza ufanisi katika kueneza teknolojia za kilimo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika*,* katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipanga kupandisha cheo watumishi 564 ambapo watumishi 282 wamepandishwa cheo. Watumishi waliobaki watapandishwa cheo kati ya mwezi Aprili na Mei 2013 kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itapandisha cheo watumishi 406 katika madaraja mbalimbali. Aidha, watumishi wapya 480 wa kada mbalimbali wataajiriwa. Kati ya hao 28 ni Wahandisi Kilimo, 21 ni Maafisa Kilimo, 30 ni Watafiti Kilimo, 14 ni Wakufunzi Kilimo, 12 ni Wapima Ardhi, 15 ni Maafisa Kilimo Wasaidizi na 360 ni wa kada nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Utawala Bora na Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Wizara itatoa mafunzo ya maadili; mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya; na mafunzo ya kuongeza ujuzi katika masuala ya menejimenti. Aidha, Wizara itaimarisha *OPRAS*, Mkataba wa Huduma kwa Mteja na Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko.

Vilevile, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa watumishi *(Human Resources Audit)* ili kuiwezesha Wizara kusimamia vyema ankara ya mishahara na kupanga vema matumizi ya rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa menejimenti ya taarifa za watumishi kwa njia ya mtandao wa kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa *TEHAMA* katika kilimo kwa kuimarisha miundombinu ya *TEHAMA* wizarani na kuongeza vitendea kazi. Aidha, Wizara imeunganishwa kwenye Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ikiwa ni hatua muhimu ya kurahisisha mawasiliano kati ya Wizara na wadau wengine. Nyaraka na taarifa nyingi zimeongezwa kwenye Tovuti ya Wizara ya www.kilimo.go.tz au_www.agriculture.go.tz. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa TEHAMA hatua kwa hatua kutegemeana na upatikanaji wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia masuala mtambuka katika kilimo, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuratibu, kudhibiti, kutathmini na kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika maendeleo ya kilimo. Wizara imekamilisha Rasimu ya Mwongozo wa Tathmini ya Athari za Mazingira kwenye kilimo na kuiwasilisha Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwa ajili ya kuidhinishwa na

kusambazwa kwa wadau. Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (World Bank), Shirika la Misaada la Uingereza (DFID) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) inaandaa mkakati na mpango kazi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupambana na UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari na kuendelea kuwapatia dawa na vyakula vyenye virutubisho watumishi 17 wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuwezesha watumishi 18 waliojitambulisha, wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata lishe bora na matibabu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Uingereza, Misri, Ubelgiji, Malaysia, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil na Uholanzi.

Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA, Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation* na *Unilever*. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na changamoto wanazokumbana nazo.

Napenda pia kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Adam Kighoma Malima - Mbunge wa Mkuranga, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa

ya Chama cha Mapinduzi; Kaimu Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Mbogo Futakamba; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2012/2013 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2013/2014.

Mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kKwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Sh. 328,134,608,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika Fungu 43 kwa mwaka 2013/2014.

Kati ya fedha hizo, Sh. 247,094,320,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 81,040,288,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Sh. 210,175,943,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC),* Sh. 25,602,969,000/= ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* ya Wizara na Sh. 11,315,408,000/= ni mishahara *(PE)* ya Bodi na Taasisi. Kati ya fedha za bajeti ya maendeleo, Sh. 23,927,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 57,113,288,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Fungu 24 la Ushirika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kupitia Fungu 24 inaomba Sh. 5,783,105,000/= fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh. 3,384,444,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC),* Sh. 766,109,000/= ni kwa ajili ya Mishahara *(PE)* ya Tume na Sh. 1,632,552,000/= ni kwa ajili ya Mishahara *(PE)* ya Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii. Prof. Peter Msolla!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3, 4 na 12 Aprili, 2013 Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makisio ya mwaka wa fedha 2012/2013 pamoja na Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara isipokuwa kwa maeneo ambayo utekelezaji wake ulisababishwa na upungufu na ucheleweshaji wa fedha pamoja na sababu mbalimbali za kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2012/2013. Katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

· Ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha;

· Upatikanaji mdogo wa fedha za mfuko wa pembejeo. Kwa mfano, Mfuko wa Pembejeo ulitengewa

Shilingi bilioni 3.4 wakati mahitaji halisi yalikuwa Shilingi bilioni nane kwa mwaka;

- Uchache wa Maafisa Ugani na Ushirika;

- Uelewa mdogo kuhusu ushirika miongoni mwa wananchi kwa ujumla hivyo kusababisha kuwa na idadi ndogo ya wanachama; na

- Ubadhirifu kwa baadhi ya viongozi wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika chini ya Fungu 43 inaomba jumla ya Sh. 328,134,608,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 247,094,320,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 81,040,288,000/= ni ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo Sh. 23,927,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 57,113,288,000/= ni fedha za kutoka nje. Fungu 24 - Ushirika jumla ya Sh. 5,783,105,000/= zinaombwa.

Mheshimiwa Spika, katika fungu 43, Wizara inakusudia kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Uzalishaji wa mahindi utakaofanyika katika Halmashauri nane za Mpanda, Sumbawanga, Mbozi, Mbeya, Iringa, Mufindi, Njombe na Songea. Wakulima wa mahindi watasaidiwa kuanzisha vikundi vya biashara *(farmer business organizations).* Mpango huu unategemewa kuongeza uzalishaji wa mahindi kwa tani 350,000 ifikapo mwaka 2015;

- Kugundua aina tano za mbegu bora za mazao kwenye kanda saba za ikolojia ya kilimo ifikapo Juni, 2016;

- Kuzalisha tani kumi za mbegumama *(breeders' seeds)* kwa mazao ya nafaka, mikunde, mboga mboga, mbegu za mafuta na pingili milioni mbili za mazao ya jamii ya mizizi;

· Kuiwezesha Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(NFRA)* kununua tani 235,000 za mahindi na tani 15,000 za mtama kufikia Juni, 2014; na

· Kuanzisha kituo cha Umwagiliaji *(centre pivot irrigation system)* katika shamba la mbegu la Msimba, Kilosa (hekta 200) na shamba la Arusha (hekta 100) ifikapo Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ni ndogo na hii inasababisha Sekta ya Kilimo kutochangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Ukuaji wa Kilimo unashuka mwaka hadi mwaka kama inavyoonyeshwa kwenye taarifa tuliyoitoa.

| **Mwaka** | **TShs. Bilioni** | **%** |
|---|---|---|
| 2008/2009 | 440 | 6.4 |
| 2009/2010 | 666.9 | 7 |
| 2010/2011 | 903 | 7.7 |
| 2011/2012 | 926 | 6.7 |
| 2012/2013 | 792 | 5.3 |
| 2013/2014 | | |

Mheshimiwa Spika, kwa mtiririko huo, Kamati inaishauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi ili bajeti ya Sekta ya Kilimo ifikie kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC (Maputo*

*Declaration)* cha 10% ya Bajeti ya Serikali ili Sekta ya Kilimo iweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kilimo katika nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Kamati inashauri Wizara ifanye *Re-allocation* ili maeneo muhimu yaliyotengewa fedha kidogo yaongezewe, mathalan Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority - TFRA).*

Maeneo ambayo Kamati inashauri yapewe kipaumbele cha kupewa nyongeza ni kama yafuatayo:-

· Kuongeza Ruzuku ya Pembejeo kwa wakulima ya Sh. 66,326,180,000/= (kama utaratibu wa Vocha utatumika kutoa ruzuku) na Sh. 108,508,500,000/= (kama utaratibu wa mikopo utatumika kutoa ruzuku).

· Kuongeza *retention* ya Kitengo cha Afya ya Mimea *(Plant Health Services)* kutoka asilimia 62 ya sasa hadi asilimia 92. Kitengo cha Afya ya Mimea na Kituo cha Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki kinatekeleza kazi mbalimbali ambazo ni pamoja na udhibiti wa visumbufu vihamavyo. Wakipewa kiasi hicho cha makusanyo, wanaweza kukusanya Shilingi bilioni saba mwaka.

· Kuajiri wagani 4949 ili kuboresha huduma za kilimo.

· Kulipa Madeni ya Wizara, yanayofikia Sh. 20,326,323,310.94 Madeni hayo yanahusisha Wazabuni mbalimbali waliotoa huduma katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na 2011/2012,

· Kuajiri Wateuzi wa Madaraja ya Tumbuku, yaani *Classifiers* 21 ili kufikia jumla ya 42. Wateuzi hao ni muhimu katika biashara ya Tumbaku kwa sababu ndiyo huthaminisha ubora wa tumbaku ambao bei ya tumbaku hutegemea. Upungufu huo wa *classifiers* una athari zifuatazo:-

- Tumbaku kutonunuliwa haraka kutoka kwa wakulima kwani wanalazimika kuwasubiri Wateuzi na hivyo kuathiri soko la Tumbaku;

- Wakulima kupata hasara endapo tumbaku itakaa muda mrefu bila ya kununuliwa, na

- Wakulima kulalamikia vitendo vya rushwa ambapo malalamiko makubwa ni Tumbaku ya wakulima kupewa daraja la chini hadi hapo watakapotoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, Wateuzi wa Madaraja ya Tumbaku watakaoajiriwa watahitaji mafunzo na vitendea kazi. Gharama ya kuajiri, kuwafundisha na kuwapatia vitendea kazi Wateuzi wapya ni Sh. 1,647,260,670/=.

Jumla ya fedha za ziada zinazohitajika ili Wizara iweze kutekeleza kazi zake vizuri ni Sh. 88,331,764,080.94 (endapo ruzuku ya pembejeo itatolewa kwa utaratibu wa vocha) na Sh. 130,502,083,980/= (endapo ruzuku ya pembejeo itatolewa kwa utaratibu wa mikopo).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa dhana ya Kilimo Kwanza ilibuniwa kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na kibiashara ili nchi iweze kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuzwa kwenye soko la ndani na nje.

Hata hivyo, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara, Kamati imebaini kuwa hakuna mikakati ya dhati ya kutekeleza dhana hiyo. Hivyo, Kamati inashauri kwamba Serikali iangalie upya azma hii ili malengo yake yaweze kufikiwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iweze kuendelea katika Sekta ya Kilimo ni lazima iwekeze katika utafiti. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Utafiti unaoratibiwa na *COSTECH*. Kamati inaishauri Serikali iendelee

kuongeza fedha katika mfuko huu ili hatimaye ufikie angalau asilimia moja ya pato ghafi la Taifa *(1% GDP).*

Mheshimiwa Spika, Taasisi mbalimbali za utafiti nchini hupewa bajeti ndogo na mtiririko wake hauridhishi. Kutokana na hilo Kamati inashauri yafuatayo:-

- Zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti na ukarabati wa miundombinu katika Taasisi za Utafiti;

- Matumizi ya teknolojia ya *GMO (Genetically Modified Organisms)* bado haijaeleweka. Kamati inashauri Serikali itoe elimu kwa Umma kuhusu teknolojia hii;

- Serikali iangalie upya Kanuni za matumizi ya bioteknolojia *(Biosafety Regulations);*

- Utafiti wa matumizi ya bioteknolojia ufanyike ili kutengeneza mbegu bora zenye vinasaba vyenye uwezo wa kustahimili ukame na magonjwa;

- Serikali iongeze juhudi ya kufanya utafiti wa magonjwa ya mimea kama Mnyauko wa migomba, Batobato wa mihogo, ugonjwa wa kuoza wa mahindi *(Maize Lethal Necrosis)* na kadhalika; na

- Serikali ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pembejeo, mbolea. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

§ Ufanyike utafiti wa kina ili pawepo na utaratibu wa uhakika wa namna ya kusambaza pembejeo badala ya utaratibu wa sasa usio wa uhakika na unaobadilika kila wakati;

§ Serikali inashauriwa kufanya matayarisho ya kutosha kabla utaratibu wa kutoa ruzuku kwa mikopo kuanza. Naomba kurudia, Serikali inashauriwa kufanya matayarisho

ya kutosha kabla ya utaratibu mpya wa kutoa ruzuku kwa mikopo kuanza kutumika;

§ Serikali iendelee kuongeza idadi ya wakulima wanaopata ruzuku kwani itasaidia katika kuongeza tija;

§ Serikali iharakishe mikakati ya ujenzi wa Viwanda vya Mbolea nchini ikizingatiwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na gesi asilia na madini ya *phosphate* ambayo ni malighafi muhimu; na

§ Ili wakulima wenye mahitaji ya viwango tofauti waweze kupata mbolea kulingana na uwezo na mahitaji yao ni vyema mbolea zifungashwe katika mifuko yenye ujazo tofauti, mfano kilo 5, 10, 25 na 50.

Mheshimiwa Spika, mbegu bora ni moja ya misingi ya kuleta tija katika kuhakikisha usalama wa chakula. Kamati inashauri kwamba, Serikali itoe bajeti ya kutosha kwa Wakala wa Mbegu *(ASA)* ili kuzalisha mbegu za kutosha hapa nchini badala ya kuagiza mbegu hizo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazao mengi yakiwemo ya chakula na ya biashara kushambuliwa na wadudu waharibifu, na kwa kuwa kuna malalamiko kuwa baadhi ya dawa zinazosambazwa kwamba haziui wadudu, Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

· Ifuatilie na kuhakikisha ubora wa madawa ya mazao yanayoingizwa hapa nchini;

· Iongeze bajeti ya madawa ya mazao ili kuongeza uzalishaji; na

· Utafiti wa kutumia viuatilifu vya kimaumbile *(Biological Control*) uendelee ili wakulima wavipate kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji, ili kuwavutia wawekezaji ni vyema Serikali ikaweka mazingira mazuri katika kilimo, na Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iweke vivutio kwa wawekezaji ili washawishike kuja kuwekeza katika kilimo cha mashamba makubwa;

- Serikali ipunguze urasimu ili kuondoa usumbufu kwa wawekezaji;

- Serikali ihakikishe kwamba kuna eneo la kutosha kwa ajili ya kilimo cha wananchi wenyewe;

- Serikali iwahimize wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujenga viwanda vya kusindika mazao ili kuongeza thamani yake;

- Serikali iangalie mikataba inayoingia na wawekezaji ili kuepuka kuingia mikataba ya miaka mingi na hatimaye kupoteza eneo kubwa la ardhi bila tija yoyote. Aidha, ushirikishwaji wa wanachi katika kutoa maeneo ya uwekezaji uzingatiwe;

- Serikali izingatie matumizi sahihi ya ardhi yanayoendana na mkataba unavyotaka ili kuepuka matumizi mengine yanayowanufaisha wawekezaji na kudhoofisha maendeleo ya wananchi;

- Serikali inashauriwa kwa mara nyingine kutenga maeneo kwa ajili ya Benki ya Ardhi ili yawe tayari kuwapatia wawekezaji mara tu wanapojitokeza kuendesha shughuli za kilimo; na

- Zoezi la upimaji wa ardhi ya vijiji linaenda taratibu sana. Kamati inashauri zoezi hili liwezeshwe ili liende kwa kasi zaidi ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wanakijiji katika zoezi la uainishaji wa maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao, Kamati imetambua matatizo wanayopata wakulima pale ambapo bei za mazao hushuka kutokana na kushuka kwa bei za Soko Duniani. Kamati inaunga mkono juhudi za Serikali kuanzisha Mfuko wa Kuhimili Mtikisiko wa Bei ya Mazao *(Price Stabilization Fund)* lakini Serikali isiwachangishe wakulima kwa ajili ya Mfuko huu.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta matrekta kutoka India na kuwakopesha wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza utaratibu huu na uzidi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ijikite katika kuhimiza uzalishaji wa mazao mengine mapya kama viungo, matunda, mboga mboga na maua. Mazao haya yatasaidia kuliongezea pato Taifa na kukuza uchumi wa nchi. Serikali ihakikishe inawapatia wakulima mitaji na utaalam. Aidha, Serikali itumie Chuo cha Utafiti cha *KATRIN* katika kupeleka utaalam wa mazao ya viungo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Stakabadhi ghalani ni mfumo ambao Serikali imeuweka kwa nia nzuri ya kuwasaidia wakulima katika kupata soko zuri la mazao yao. Pamoja na nia njema ya Serikali, kumekuwa na usumbufu mkubwa kwenye mfumo huu ambapo wakulima hucheleweshewa malipo yao na wakati mwingine hadi msimu mwingine unafika na kushindwa kujiandaa kwa msimu ujao. Mfumo huu utazamwe upya ili kuona namna ya kuuboresha na kuleta manufaa kwa wakulima. Kwa mfano, mfumo wa *Commodity Exchange Markets* uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Vyuo vya Ugani toka vyuo vinane hadi vyuo 14.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika. Hatua hii itaweza kuvipunguzia mzigo wa madeni na kufufua vyama

vya ushirika vilivyokuwa vimekufa. Pamoja na hatua hiyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuongeza wanachama wa Ushirika kwa njia ya uhamasishaji;

- Serikali iajiri Maafisa Ushirika wa kutosha ili kukidhi mahitaji; na

- Ili kuondoa ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika, Serikali irekebishe Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 na Kanuni zake na kuweka adhabu kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi za mazao ni muhimu sana katika kusimamia mazao na kuhakikisha yanazalishwa kwa kiwango kikubwa. Ili Bodi hizi ziweze kusimamia mazao husika vizuri ni lazima ziwezeshwe vya kutosha kifedha. Bodi nyingi bado hazitengewi fedha za kutosha, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kamati inashauri kwamba:-

- Serikali iendelee kuziongezea fedha Bodi hizi kulingana na mahitaji yao;

- Serikali ihakikishe kuwa Bodi hizi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ili kuondoa urasimu wa kutoa leseni za biashara za mazao ambao unaathiri ushindani kwa kiwango kikubwa; na

- Bodi za mazao zihimize umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao kabla ya kuuza mazao ndani na nje ya nchi ili kuongeza kipato cha mkulima na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kuendelea kusaidia Wakala wa Hifadhi ya Chakula nchini. Pamoja na pongezi hizi, Kamati ina ushauri ufuatao:-

- Wakala wa chakula apewe uwezo zaidi wa fedha ili kiwepo chakula cha kutosha ghalani wakati wote;

- Serikali iangalie upatikanaji wa magunia ya kuhifadhia chakula kwani yaliyopo hayatoshi na viwango vyake vya ubora haviridhishi; na

- Serikali ifanye tathmini ya hali ya chakula nchini kabla ya kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukame unaojitokeza mara kwa mara pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa uhakika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara hapa nchini. Ukuaji huo wa kilimo cha umwagiliaji unakwenda taratibu mno ukilinganisha na malengo makubwa ya kilimo hicho. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

- Kuongeza bajeti kwa ajili ya kuanzisha skimu ndogo, za kati na kubwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini;

- Kuainisha na kuyatumia mabonde mengi ya maziwa na mito kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji;

- Kuviongezea uwezo wa kiutendaji Vituo vya Kanda vya Umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kuboresha na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za wakulima wadogo na kujenga skimu mpya katika maeneo yanayofaa kuendelezwa; na

- Kuongeza idadi ya wataalam wa umwagiliaji na kuwaajiri katika Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na kazi nzuri wanayofanya.

Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla - Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Juma Nkumba - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Ameir, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Abdalla haji Ali, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Lolesia Masele Bukwimba, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa na Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa.

Wengine ni Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mheshimiwa Sylvestry Francis koka, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Meshack Jeremia Opulukwa, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika fungu 43 kwa mwaka 2013/2014 jumla ya Sh. 328,134, 608,000/= na nyongeza inayoombwa ya Sh. 88,331,764,080.94 endapo ruzuku ya pembejeo itatolewa kwa utaratibu wa vocha na Sh. 130,502,083,980/= endapo ruzuku ya pembejeo itatolewa kwa utaratibu wa mikopo. Kwa Fungu 24 - Ushirika linaombwa jumla ya Sh. 5,783,105,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mheshimiwa Kamili.

**MHE. ROSE KAMIL SUKUM – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Naomba kusoma hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014. Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yote ninayoiwasilisha iingie kwenye *Hansard* kwa sababu ina maneno mengi.

Mheshimiwa Spika, naanza na dhana ya Kilimo Kwanza. Kwa mujibu wa mpango wa Serikali katika utekelezaji wa dhana ya Kilimo Kwanza, Serikali ilijiwekea nguzo kuu 10 katika utekelezaji wa mpango huo, na pia iliweka ukomo wa utekelezaji wa mpango huo kuwa ni mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu 10 za utekelezaji dhana ya Kilimo Kwanza zilizopitishwa na Serikali zilikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Dira ya taifa ya kilimo kwanza : Hii ililenga kuhakikisha kuwa kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa kiwe cha kisasa na cha kibiashara ifikapo mwaka 2015;

(ii) Kugharamia kilimo kwanza: Hii ililenga kuongeza bajeti ya serikali kwa ajili ya kilimo, kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo yenye mtaji wa kuanzia dola za kimarekani milioni 500 Desemba, 2009, kuanzisha mfuko maalum wa fedha za kilimo kwanza;

(iii) Muundo mpya wa Taasisi kwa ajili ya usimamizi: Hii ilikuwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa uhusiano na wizara nyingine zinazohusiana na maswala ya kilimo na kuimarisha vyama vya wakulima;

(iv) Mabadiliko ya mfumo wa kimkakati : Hii ilikuwa ni pamoja na kubainisha maeneo ya vipaumbele kwa ajili ya vyakula muhimu ili nchi ijitosheleze kwa chakula;

(v) Ardhi kwa ajili ya kilimo kwanza: Hii ilikuwa ni pamoja na kurekebisha sheria ya Ardhi ya Vijiji Na 5 ya 1999 ifikapo 2010 ,kuharakisha mfumo wa upatikanaji ardhi, kuharakisha utatuzi wa migogoro ya ardhi, kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo;

(vi) Vivutio kwa ajili ya kilimo kwanza : Hii ilikuwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vya masoko kwa mazao ya kilimo, kuimarisha utumiaji wa vipimo na viwango halali katika biashara na kuboresha bei ya mazao;

(vii) Viwanda kwa ajili ya kilimo kwanza : Hii ilikuwa ni pamoja na kuanzisha viwanda kwa ajili ya kushughulikia mahitaji ya wazalishaji wa kilimo,kuongeza uzalishaji na matumizi ya mbolea,kuboresha uzalishaji wa mbegu na dawa za kilimo, uzalishaji wa zana na vifaa vya kilimo;

(viii) Sayansi,Teknolojia na rasilimali watu: Hii ilikuwa ni pamoja na kuanzisha bodi ya usajili ya wataalamu wa kilimo,kulipia mikopo ya gharama zote za masomo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya kilimo,kuanzisha vituo vya hali ya hewa katika ngazi ya kata;

(ix) Miundombinu kwa ajili ya kilimo kwanza : Hii ilikuwa ni pamoja na kujenga miradi ya umwagiliaji ya kutosha, kujenga vituo vya masoko kila kata,kupelekea umeme vijijini kwa ajili ya kuboresha kilimo; na

(x) Uhamasishaji wa watanzania kwa ajili ya kilimo: Hii ilikuwa ni pamoja na kuhamasisha shule na vyuo kushiriki kwenye kampeni ya kilimo kwanza, viongozi wa ngazi zote kushiriki katika kilimo binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inataka kupata majibu ya kina juu ya utekelezaji wa nguzo hizi 10 za kilimo kwanza na hasa

ikizingatiwa kuwa huu ni mwaka 2013 na kwa maana hiyo, imebaki miaka miwili tu ili utekelezaji wa nguzo hizi uwe umekamilika.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha shughuli za Kilimo, Serikali ilikuwa na mpango wa kuanzisha Benki ya Kilimo, ambapo kulikuwa kunahitajika mtaji wa Shilingi bilioni 750 kwa ajili ya kuanzisha Benki hiyo.

Hata hivyo, mpango huu umekuwa ukisuasua na matokeo yake Benki hiyo imekuja kuanzishwa na mtaji wa Shilingi bilioni 60 kinyume na mpango wa awali wa mtaji wa Shilingi bilioni 750.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu ya kina kama fedha hizi zitatosha kulingana na mpango wa utekelezaji. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama mtaji huu wa Shilingi bilioni 60 ni sehemu ya marejesho ya fedha za *EPA* kama Bunge lilivyokuwa limeelezwa kuwa fedha za *EPA* zitaelekezwa kwenye Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1996 hadi 2012 uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kati ya asilimia 3.5 hadi 7.8, na kwa kipindi cha mwaka 2012 inaonyesha kuwa uchumi ulikuwa kwa asilimia 6.5.

Aidha, Kasi ya ukuaji katika Sekta ya Kilimo ambayo inaajiri takribani asilimia 75 ya nguvukazi nchini ilipungua, kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 hadi 3.6 mwaka 2011. Ni ukweli uliowazi kuwa taarifa hiyo ya ukuaji wa uchumi haiendani na hali halisi ya maisha ya wananchi. Mafanikio yanayotajwa yameshindwa kuondoa umasikini kwa wananchi hasa wale wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara ina jumla ya eneo la hekta milioni 29.4 linaloweza kufanya uzalishaji kwa umwagiliaji, lakini ni karibu eneo la hekta 330,000 tu (sawa na 1.1% tu ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji) ndilo kwa sasa linafanya uzalishaji kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kilimo ni biashara kama zilivyo biashara nyingine, hivyo ili kiweze kupiga hatua ni lazima mazingira ya kufanyia biashara hiyo ya kilimo yaboreshwe ili wakulima wadogo na wale ambao wasiojihusisha na kilimo wavutiwe kufanya biashara hiyo.

Katika mazingira ya nchi yetu, wakulima wadogo ndio wadau wakubwa wa kilimo, hivyo basi, changamoto za kuongeza tija ndiyo kikwazo cha kuifanya sekta hiyo kukua na kuondoa au kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei unauhusiano wa moja kwa moja na maisha ya watanzania wengi. Kupanda kwa bei za vyakula kwa zaidi ya asilimia 50% maana yake ni kushuka kwa uwezo wa manunuzi(Kipato) kwa wananchi masikini waishio mijini kwa asilimia 25%(Kwa kutilia maanani kuwa familia hizo hazizalishi chakula).

Sambamba na hilo ni kuwa kipato kikubwa kwa kipindi hicho kinatakiwa kiende kwa wakulima wazalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa kwa kilimo ni jinsi ya kuongeza tija kwa eneo dogo la ardhi inayotumiwa na wakulima wadogo kwa kulinganisha na nguvu kazi inayojihusisha katika kilimo. Changamoto hii inaweza kuondolewa kirahisi kama mahitaji muhimu katika kufanikisha kilimo yatapatikana yakiwa na ubora na kwa wakati. Mahitaji hayo ni huduma za ushauri, pembejeo bora (mbegu, madawa) miundombinu ya umwagiliaji, huduma za kibenki, masoko ya uhakika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya CCM inajua kwamba bila kuwekeza kikamilifu katika Kilimo, umasikini utaendelea kulitafuna Taifa hili, lakini bado sioni dhamira ya dhati ya Serikali kuwekeza katika Kilimo. Nasema hivi kwa sababu mwezi Agosti, 2010, aliyekuwa Waziri wa kilimo wakati huo, Mheshimiwa Stephen Masatu Wassira, alisema kwamba; “Msingi wa maudhui ya azma ya Kilimo Kwanza ni kukiri kwamba, haiwezekani kukuza uchumi wa Tanzania na

kiwango cha kupunguza umaskini kwa Watanzania walio wengi bila kuwekeza kwa kiwango cha kuridhisha katika Sekta ya Kilimo.*"*

Mheshimiwa Spika, nikumbushe Bunge hili kuwa Tanzania iliridhia na kujiunga na mpango wa maendeleo kusini mwa Afrika, *CAADP*, tangu ulipoasisiwa mwaka 2003. Pamoja na malengo mengine, mpango huu ulilenga kuongezwa kwa bajeti kwa Sekta ya Kilimo hadi 10% ya Pato ghafi la Taifa *(GDP).* Hii inajulikana zaidi kama Azimio la Maputo-Msumbiji, ambalo lilizitaka nchi zote mwanachama wa *African Union (AU)* kutenga asilima 10 ya bajeti zao kila mwaka kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa na mipango mingi ya kilimo na kwa sasa tayari kuna mpango mpya uitwao *TAFSIP- (Tanzania Agriculture Food Security Investment Plan)* ambao ni Mpango wa miaka 10 ijayo wenye lengo la kukifanya kilimo kiweze kuchangia katika ukuaji wa uchumi, kuongeza pato la mkulima na Taifa kwa ujumla na kuhakikisha kwamba Taifa linajitosheleza kwa chakula na lishe**.**

Mheshimiwa Spika, Mpango huo umeandaliwa kwa kuzingatia yaliyomo katika miongozo na mifumo ya kutekeleza Dira ya Maendeleo, yaani *Vision* 2020 na 2025, Programu za kitaifa yaani MKUKUTA, Kilimo Kwanza, *ASDP* na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012- 2015/2016).

Mheshimiwa Spika, *TAFSIP* imeainisha maeneo makuu saba (7) ya uwekezaji ili kufikia lengo la asilimia 6 ya ukuaji wa sekta kila mwaka na kwamba Serikali itaongeza bajeti yake hadi kufikia asilimia 10 kama Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Barani Afrika yaani *Comprehensive Africa Agriculture Development Programme (CAADP)* inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, gharama za kutekeleza mpango kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 – 2015/2016 ni shilingi za kitanzania trilioni 8.7 au

dola za kimarekani bilioni 5.3. Wastani wa mahitaji ya fedha kwa mwaka ni Shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihamasisha na kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi katika kilimo na kujenga dhana ya kibiashara biashara kama ilivyoainishwa katika nguzo ya pili ya Kilimo Kwanza ambayo pia umeanza kutekelezwa kupitia Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)*.

Mpango huo unalenga zaidi kuvutia uwekezaji katika kilimo kwa ushirikiano baina ya wakulima wakubwa na wadogo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wowote ambao unalenga kuondoa njaa bila ya kuondoa umasikini kwa wakulima, huo ni mpango mwingine wa kutuharibia ardhi yetu na unatakiwa ukaribishwe kwa tahadhari kubwa katika nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji katika kilimo unatakiwa ufanywe kwa wakulima wadogo na wa kati, kwani ndiyo sehemu kubwa ya jamii inayojihusisha na kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwekeza zaidi kwenye kada hizo mbili za wakulima. Aidha, tunaitaka Serikali kuchagua aina ya kilimo kitakachoharakisha kuondoa umasikini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ujio wa *SAGCOT* hapa nchini unapata uhamasishaji mkubwa kutoka ndani na nje, kwa dhana kuwa ndiyo mkombozi wa tatizo la njaa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ujio huo unakuja pia na washirika wake ambao ni Makampuni makubwa Duniani yanayozalisha mbolea na mbegu pamoja na madawa yakiwa kama washirika katika mpango huo wa uwekezaji mkubwa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, Makampuni hayo washirika katika mpango huo, sio kwamba itakuwa ni mara ya kwanza hapa

Tanzania bali washirika hao wamefanyakazi mataifa mengi hapa Duniani. Moja ya nchi hizo ni India.

Maandiko na taarifa mbalimbali kuhusiana na mpango kama huu wa *SAGCOT* kwenye nchi ya India zinaonyesha kuwa wakulima wadogo na wakati wamekuwa ni mahanga wakubwa wa makampuni hayo yanayozalisha mbegu, madawa na kutoa mbolea. Makampuni ya mbegu hasa za pamba yamesababisha wakulima kujiua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo nchini India iliishauri Serikali ya nchi hiyo kusitisha uuzwaji wa mbegu za pamba aina ya Bt-*Cotton* zilizokuwa zinazalishwa na kusambazwa na Kampuni ya Monsanto, ambayo ilitumia fedha nyingi kuwashawishi wakulima kuachana na mbegu zao za asili na kutumia mbegu zilizokuwa zinazalishwa na Kampuni hiyo.

Mbegu hizo zilionyesha ni ghali sana kwa asilimia 100 kulinganisha na mbegu za asili za Pamba. Mbali ya ughali huo mbegu hizo, zilionekana kuwa hazina uwezo wa kuota katika msimu unaofuata, jambo ambalo linazidisha kuongeza matatizo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, ukweli uliotolewa na Wizara ya Kilimo ya India ni kwamba zaidi ya wakulima wadogo 1,000 wanajiua kila mwezi kutokana na kukithiri kwa madeni yanayolimbikizwa kutokana na mbegu zizalishwazo na Monsanto. Hilo limepelekea wakulima wadogo zaidi ya 125,000 kujiua.

Mheshimiwa Spika, kitendo chochote kitakachopelekea wakulima wadogo kununua mbegu ambazo haziwezi kutunzwa na kuoteshwa zaidi ya msimu mmoja, Kambi Rasmi ya Upinzani inauweza kukiita kitendo hiki kuwa ni hujuma.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inaendelea kusema kuwa uzalishaji mkubwa ni kwa miaka mitano ya mwanzo tu,

na baada ya kipindi hicho maafa yanafuatia. Hii ni kuzidi kumdidimiza mkulima kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusu ujio wa Makampuni hayo ya mbegu kwani kwa historia na maandishi niliyoyaweka hapo juu ni kwamba kuyaruhusu Makampuni hayo kufanya biashara hapa nchini ni sawa na kuruhusu janga lingine linalokuja kwa wakulima wadogo na kilimo chetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mpango huo ni maeneo gani ambayo yako wazi kwa ajili ya uwekezaji zaidi ya kunyang'anya wakulima wadogo mashamba yao *(land grabbing)* ambayo ndipo tunapoelekea. Aidha, Wizara ya kilimo imekuwa ikihamasisha uwekezaji katika kilimo kupitia vijarida vyake vikiainisha maeneo yenye fursa ya kilimo *(Investment potential and opportunities in agriculture).*

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa na kuidhinishwa mwaka jana kwa ajili ya *SAGCOT* ni Shilingi bilioni 6.567. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa kwa ajili ya uendeshaji wa mradi huo ni Shilingi bilioni 3.827, hizi sio za uwekezaji na ni fedha za ndani. Hoja ni kwanini fedha hizi za ndani zimetengwa kidogo kwa kulinganisha na mwaka 2012 ? Jambo linalotia mashaka kwa mpango huu wa *SAGCOT* ni kipaumbele kwa Taifa.

Je, ni kweli Mradi huo ni kipaumbele cha Taifa kama inavyodaiwa ? Mwaka wa fedha unaomalizika fedha zilizotolewa na Hazina ni Shilingi bilioni 1.75 lakini zilizotumika hadi Machi 2013 ni asilimia 77 tu. Je, na hizo zilitumika katika uendeshaji badala ya uwekezaji? Wakulima wadogo na wa kati wamenufaika vipi katika mgawo wa awamu ya kwanza ya fedha hizo za *SAGCOT*?

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuelewa ni maeneo gani yaliyoainishwa yako wazi na hayatumiki kwa shughuli nyingine zaidi ya kilimo, kwani tumekuwa tukiambiwa Serikali inaandaa land bank? Kambi inataka kujua ni maeneo gani yaliyoainishwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo, mifugo na makazi kuondokana na migogoro inayoendelea hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, mjumuiko wa asasi za kiraia ulikaa na kutoa ushauri kwa Serikali katika kutekeleza Mpango wa SAGCOT ili vijiji vinavyotoa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa mpango huo vinufaike na uwekezaji huo katika chapisho lao. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka wazi jinsi gani upatikanaji wa ardhi na mchakato mzima wa uwekezaji na jinsi wazalishaji wadogo na wa kati wanaozunguka maeneo ya uwekezaji watakavyopata mitaji.

(ii) Matumizi bora ya ardhi katika vijiji ambavyo vitatoa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa *SAGCOT* yawekwe chini ya uangalizi huru ili kuepuka mgongano wa kimaslahi.

(iii) Eneo la ardhi ya vijiji litakalotolewa kwa msingi wa uwekezaji wa *SAGCOT* libaki kama eneo la vijiji kwani baada ya mradi kumalizika lirudi katika umiliki wa vijiji badala ya eneo hilo kutwaliwa na Serikali kuu.

(iv) Vijiji vinavyotoa ardhi ya uwekezaji ni lazima vipatiwe washauri waelekezi ambao ni huru ili watoe tathmini huru isiyoegemea upande wowote.

(v) Mpango mkubwa wa uwekezaji wa *SAGCOT* katika umwagiliaji ni lazima ulazimike kutoa huduma hiyo kwa jamii za wakulima wanaozunguka mradi huo.

(vi) Umwagiliaji ujikite katika kuhakikisha makubaliano ya matumizi bora ya maji na ufuatiliaji wa mara kwa mara unafanyika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge na Watanzania wote utekelezwaji wa ushauri huo wa Asasi za Kiraia hadi sasa umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano unaonyesha kuwa kipaumbele cha pili ni kuwekeza katika Sekta ya Kilimo kwa tafsiri pana ambayo inajumuisha Sekta ya Kilimo cha mazao ya chakula na biashara, Sekta ya Mifugo, Uvuvi, Ufugaji wa Nyuki na Rasilimali za Misitu. Shabaha Kuu ya kuendeleza Kilimo ni kuleta Mapinduzi ya haraka ya Kilimo yatakayotuwezesha kuongeza uzalishaji na tija ili kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada nje.

Mheshimiwa Spika, Kiwango cha ukuaji katika kilimo hakijafikia lengo lililowekwa na serikali la kufikia ukuaji wa asilimia kumi kwa mwaka kuanzia 2008 – 2015; na ukosefu wa chakula bado ni tatizo kwa watu wengi. Kiasi kikubwa cha kaya zisizokuwa na chakula cha kutosha zipo vijijini ambapo kilimo kinategemewa sana kama chanzo cha kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Bwana Philipe Egger kwenye Jarida la *ILO* la mwezi Februari,2013 inaonesha kuwa Afrika inaagiza chakula chenye thamani ya karibu dolla za kimarekani bilioni 50 kwa kila mwaka kwa ajili ya kulisha wakaazi wa miji inayokuwa kwa haraka sana. Inakisiwa kiasi hiki ni karibu sawa na misaada ya maendeleo inayotolewa na nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania uingizaji mkubwa wa chakula kutoka nje hufanywa si kwa sababu Tanzania haina chakula cha kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi bali ni mkakati unaotumiwa na baadhi ya watendaji kuhakikisha kuwa nguvu za wakulima hazitoi matunda na wakulima wazidi kuwa masikini. Mfano mzuri ni uingizaji wa mchele kutoka Thailand wakati wakulima wa mikoa ya Morogoro na Mbeya wakikosa soko la kuuza mchele wao. Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni hujuma kwa wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wakulima ni kwa nini inatoa vibali vya kuingiza nchini mchele wakati mchele upo mwingi kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu sehemu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango) ya mwaka 2012/2013 aliyoitoa hapa Bungeni: "Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mfumuko wa bei, Serikali ilichukua hatua zifuatazo: kuhakikisha usambazaji wa chakula katika maeneo yenye uhaba wa chakula; kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula; kuendelea kuimarisha hifadhi ya chakula kwa kuongeza ununuzi wa mazao ya chakula. ..." Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni wapi inapozalishia chakula! Hoja ni kwamba hata chakula kilichonunuliwa kutoka kwa wakulima, kilinunuliwa kwa mkopo, mfano ni wakulima wa Halmashauri ya Nkasi mkoani Rukwa ambao wanaidai wakala ya Hifadhi ya chakula ya Taifa zaidi ya shs milioni 500.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwa masikitiko makubwa ni kwamba, bado tatizo kubwa la ukosefu wa chakula limeripotiwa kutokea katika wilaya mbalimbali za nchi yetu kutokana na kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usambazaji wa chakula kutoka kinapozalishwa kwa wingi. Baadhi ya wilaya hizo ni Kilindi, Meatu, Iringa na Handeni. Kati ya Agosti hadi Februari, 2013, zaidi ya kaya 780 wilayani humo zilikabiliwa na njaa. Kwa kipindi hicho, Wananchi wapatao 81,769 wa Kata 12, Wilaya ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro, walihitaji chakula cha msaada tani 14,634.6 ili kukabiliana na tatizo la njaa ambalo limeonekana kuathiri shughuli nyingi za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya chakula nchini siyo nzuri na Serikali haionekani kuchukua hatua stahiki kumaliza tatizo hilo, kutokana na ukweli kwamba, mamlaka zilizopewa jukumu la kuhakikisha wahanga wanapewa msaada wa dharura haraka, badala yake mamlaka hizo zinafanya kazi hiyo kwa kuangalia itikadi za wanasiasa katika

maeneo ya wahanga. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa mamlaka husika zisiingiliwe na watendaji wa kisiasa, jambo linalopelekea mamlaka hiyo kupoteza uhalali wa kuitwa Kitengo cha Maafa.

Mheshimiwa Spika, uhusiano Kati ya Mgawo wa Bajeti na Uhaba wa Chakula Nchini. Kwa nchi zilizo makini na mipango yake, suala la mgawanyo wa rasilimali za nchi hasa zihusuzo chakula ni lazima ujikite kwenye maeneo ambayo yanaathirika mara kwa mara na tatizo la njaa. Utafiti ulioendeshwa na *Food Security Information Team (FSIT),* uligundua kuwa jumla ya mikoa kumi ndiyo inayokumbwa na tatizo la uhaba wa chakula mara kwa mara. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mwanza, Mtwara, Shinyanga, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa kuona kama mikoa hiyo inapata kipaumbele cha kupata zaidi katika mgawo wa fedha za *DADG* au la; matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa, kwa mwaka wa fedha 2009, mikoa hiyo kumi ambayo inaidadi ya watu asilimia 46.2 (karibu asilimia 50) ya watu wote hapa nchini *(National Bureau of Statistics (NBS)* – Mikoa hiyo ilipatiwa asilimia 30.2 ya fedha zote za bajeti ya *DADP* kwa 2009/10.

Mheshimimiwa Spika, kwa ushahidi huo inaonesha kuwa mipango ya Serikali mbali na kufanya tafiti haipangwi kutatua matatizo yanayojirudia rudia, badala yake inaonekana kuwa matatizo hayo ni neema kwa watendaji ambao hutumia vipindi vya maafa kujinufaisha wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza inakuwaje mikoa yenye idadi karibu nusu ya watanzania wote, inakabiliwa na uhaba wa chakula mara nyingi na Serikali inaelewa lakini haipewi kipaumbele katika kuhakikisha tatizo la ukosefu wa chakula linaisha au kwa ufupi ni kuwa mgawanyo wa bajeti ya kilimo haiangalii maeneo yenye uhaba wa chakula, Watawala wamechoka kutawala! Hivyo, walalahoi hawathaminiwi tena katika mipango yao.

Mheshimiwa Spika, Mgawo wa Bajeti ya *DADG* kwa

Mikoa yenye uhaba wa chakula Tanzania. Katika taarifa ya Serikali kwenye Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi mwezi Januari, 2013, Serikali ilisema inauza mahindi kwa wafanyabiashara binafsi toka katika Hifadhi ya Taifa ya Chakula (labda kwa bei ya chini kuliko ile ya soko). Wafanyabiashara binafsi wanasaga na kuuza kwa Wananchi hizo nafaka walizozinunua, lakini wafanyabiashara hao hao hulangua wanunuzi wa mahindi au unga kwa kutengeneza vocha mbili na kuwasainisha wanunuzi bei tofauti kwa sababu hawaelewi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania inadhibiti vipi bei ya unga au mahindi yanaouzwa na wafanyabishara walionunua mahindi toka katika Hifadhi ya Chakula kwa bei ya chini, ukilinganisha na bei ya soko ambayo ni wafanyabishara walionunua unga toka sehemu nyingine? Ni namna gani bei za soko zitaratibiwa kiasi kwamba wafanyabiashara waliopewa vibali vya kununua mahindi toka Hifadhi ya Chakula kuuza unga na mahindi kwa bei ya chini kuliko bei ilivyo sokoni?

Mheshimiwa Spika, pembejeo za kilimo. Ili kilimo kiendane na sera yake ya mwaka 1997 ya kuwa endelevu, chenye tija na cha kibiashara, ni lazima kubadili zana zilizokuwa zinatumika hapo kale. Takwimu zinaonesha kuwa, maksai wanaotumika katika kilimo wamekuwa wanaongezeka kutoka 320,000 mwaka 1970 hadi kufikia 1,542,000 mwaka 2010, ambapo majembe ya kukokotwa na maksai yameongezeka kutoka 140,000 hadi kufikia 620,000 katika kipindi hicho. Kwa mwaka 1960 nchi ilikuwa na matrekta makubwa 2,580 yaliyotumika katika kilimo na mwaka 2010 yameongezeka hadi kufikia 7,825. Aidha, kwa mwaka 2010 idadi ya matrekta ya mkono ilikuwa 4,571.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi ni kwamba, zana za kijadi za kilimo zinaongezeka kwa kasi kubwa kuliko ongezeko la zana za kisasa. Tafsiri yake jambo hili ni kwamba, kuna hatari kubwa ya kurejea kwenye kilimo kinachoendeshwa kwa misingi ya kijadi kuliko kilimo ambacho ndicho kinakusudiwa kumkomboa mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuangalia takwimu hizo za zana za kilimo, inaonesha wazi itachukua kipindi kirefu sana kukibadilisha kilimo, kwani ongezeko la maksai na majembe ya kukokotwa na maksai hayaendani na ongezeko la matrekta, licha ya uwepo wa mipango na mikakati mingi ya kuinua kilimo. Hizo zinaonesha kuwa ni ngonjera za muda mrefu ambazo zinaendelea hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mbegu bora, mbolea, dawa za mimea na dawa za kuulia wadudu yanayokwamishwa na upatikanaji mdogo na bei za juu za pembejeo. Umbali toka kijijini hadi maduka ya pembejeo nalo ni changamoto. Wananchi husafiri umbali wa takribani kilomita 25 hadi 56 katika Wilaya ya Lindi Vijijini, na kati ya kilomita 25 hadi 70 katika Wilaya za Mtwara Vijijini na Iringa Vijijini na kati ya kilomita 12 hadi 80 katika Wilaya ya Hanang' kufuata huduma ya pembejeo. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupeleka pembejeo katika maeneo ambayo wakulima wanaishi. Hizi siyo pembejeo zinazogawanywa bali ni zile pembejeo ambazo zinatolewa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya pembejeo za kilimo na udhibiti wa ubora wa pembejeo hasa mbegu, mbolea na viuatilifu. Kambi ya Upinzani inapenda kujua Serikali imechukua hatua gani kuhusu malalamiko ya wakulima wengi kuhusu mbegu wanazouziwa kutoota, mbolea kutokuwa na tija yoyote kwenye mazao na viuatilifu kushindwa kuua visumbufu vya mimea na mazao. Aidha, pamoja na Serikali kuajiri Maafisa Ugani wengi, lakini bado wakulima hawapati huduma hiyo hasa kuhusu matumizi bora ya pembejeo za kilimo na kilimo biashara *(farming as business).*

Mheshimiwa Spika, mgawo wa shilingi bilioni 75 kwa ajili ya vocha za pembejeo, mbolea na mbegu. Kutokana na hali halisi ilivyo, fedha hizi zinaweza kutumika kifisadi kama ambavyo imekuwa kwa miaka ya nyuma. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupeleka fedha hizi katika

Idara ya Umwagiliaji ili kuondoa adha ya ukame ambayo imekuwa kikwazo kikubwa cha uzalishaji. Kilimo cha kutegemea mvua kumeleta hasara na umaskini kwa wakulima hata wale wanaopatiwa pembejeo za ruzuku kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, fursa ya kujihusisha na kilimo cha umwagiliaji Tanzania ni ya pili katika Bara la Afrika nyuma ya Nchi ya DRC kwa kuwa na hazina kubwa ya maji. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kati ya eneo lote lifaalo kwa kilimo cha umwagiliaji la hekta millioni 29.4 ni asilimia moja inayotumika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nchi yetu ina maeneo makubwa ya ardhi, yenye rutuba na mito mikubwa pamoja na maziwa makubwa kama vile Viktoria, Nyasa, Tanganyika na Rukwa bila ya kusahau mabonde makubwa ya mito. Hii asilimia moja siyo kwamba ni ukosefu wa maji ya umwagiliaji ila ni kukosekana kwa utashi wa kisiasa na jinsi tunavyopanga vipaumbele vyetu katika matumizi ya rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, fursa katika uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji ni kubwa mno hapa nchini, lakini kuna tatizo kubwa la raslimali watu, yenye ujuzi katika nyanja ya umwagiliaji kwenye ngazi ya Halmashauri kwa ajili utekelezaji kwenye uwekezaji huo. Nyaraka zinaonesha kuwa, kikundi kazi kilichoundwa mwaka 2010, Agosti na *The Basket Fund Steering Committee* ili kuchunguza chanzo cha fedha nyingi za miradi ya umwagiliaji kupelekwa mwaka wa fedha unaofuata, kiligundua kuwa, kati ya Halmashauri 132, kuna mainjinia 32 tu na mafundi mchundo wa umwagiliaji *(Irrigation Technicians)* 107. Katika ngazi ya mkoa, kuna mainjinia wa umwagiliaji 17 tu. Baya zaidi ni kwamba, hata wale mafundi mchundo waliopo hawana vitendea kazi. La mwisho, lakini la umuhimu ni ukiritimba uliokithiri katika Halmashauri zetu ambao ni kikwazo kikubwa katika uwekezaji wa miradi kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, shabaha kuu ya Vyama vya Ushirika vilipoanzishwa, ilikuwa kuuza mazao ya wanachama

kwa bei nzuri na wakati huohuo kuondoa unyonyaji wa wafanyabiashara ambao walikuwa wakinunua mazao hayo kwa bei ya chini na kuuza kwa bei ya juu na pia kutayarisha mazao kusudi yawe katika hali bora inayotakiwa na wanunuzi. Aidha, kukusanya mazao kutoka kwa wakulima na kufanya mipango ya kusafirisha mazao hayo toka kwa wakulima hadi mikononi mwa Halmashauri za Mazao au mpaka katika Masoko ya Dunia. Pia Vyama vya Ushirika vikiwemo vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* na vile vya kilimo na masoko *(AMCOS)* vimedhihirisha kuwa nguzo muhimu katika kuwapatia maisha bora Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Ushirika unaoneshwa kuwa ni njia mojawapo ya kuboresha maisha ya Wananchi wa Tanzania walio wanyonge kiuchumi. Hoja ni kuwa kweli maisha bora yaliyokusudiwa wakati wa uanzishwaji wa vyama hivyo yanaweza kupatikana wakati bei kwa mkulima anaambiwa ni nguvu za ushindani wa soko?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tathmini ya utendaji mzima wa *AMCOS* na imesaidia vipi hizo *AMCOS* kupata mikopo kutoka taasisi za fedha kwa maendeleo ya wakulima?

Mheshimiwa Spika, nafaka ni mazao makuu ya chakula ambayo hutumiwa na Watanzania wote waishio mijini na vijijini. Nafaka zinaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu kuliko mazao mengine ya chakula na mara nyingi nafaka huzalishwa mara moja au mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, ili iweze kupatikana na kutumika kwa wakati wote ni lazima kuhifadhi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuweza kuwa na bidhaa zenye thamani ni lazima kusindika. Jitihada zimekuwa zikifanywa na Serikali kuongeza tija na uzalishaji wa mazao hayo. Uzalishaji wa mazao ya nafaka unakadiriwa kufikia wastani wa tani 3,897,500 kwa mwaka. Pamoja na ongezeko la uzalishaji, teknolojia zinazotumika katika uvunaji, utayarishaji na hifadhi ni duni na husababisha upotevu mkubwa wa

mazao hayo. Wastani wa tani 1,559,000 za mazao ya nafaka hupotea kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili ya kuanzisha chombo hiki ilikuwa ni kwa ajili ya kuwapatia wakulima huduma muhimu ikiwemo kuwapatia bei nzuri itakayokidhi gharama za uzalishaji mazao yao ambayo hayana chombo maalum ya kuyasimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa ni kwamba, chombo hiki kimeshindwa kabisa kuwasaidia wakulima kuwahakikishia ununuzi wa mazao yao kwa bei inayoweza kurejesha gharama za uzalishaji, mbali na bodi yenyewe kuingia katika mchakato wa ununuzi wa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kadiri Serikali inavyochelewa kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria zilizopo, mkulima anazidi kuwa fukara na kilimo kinazidi kukosa tija kwa mkulima na pale pale mfanyabiashara anazidi kuneemeka na kilimo hicho; hivyo, mnyororo wa biashara isiyoakisi hali halisi baina ya pande mbili husika inazidi kushamiri, jambo ambalo ni hatari na linapingana na Sera yetu ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa, muda umefika sasa kwa mkulima na kilimo kuonekana kuwa siyo chaguo la mwisho katika orodha ya kazi za ajira kwa vijana wa nchi hii. Jambo hili linaweza kufikiwa siyo kwa mikakati iliyo kwenye makaratasi na kufungiwa makabatini bali kwa kuangalia gharama halisi ya utoaji ruzuku na gharama halisi kama mkulima akipatiwa bei dira inayoweza kufuta gharama za uzalishaji. Aidha, ruzuku ikaingizwa kwenye uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani za mazao.

Mheshimiwa Spika, zao la muhogo ambalo linalimwa karibu na wakulima wote hapa nchini, linachangia takriban asilimia 15 kwenye kapu la uzalishaji wa chakula hapa nchini. Ni zao la pili nyuma ya mahindi ambalo ni zao kuu la chakula hapa nchini. Mikoa inayolima muhogo ni Mtwara, Pwani, Mwanza, Kigoma, Tanga, Morogoro, Mara, Ruvuma,

Shinyanga na Lindi. Ila kiwango cha kilimo cha zao hilo ndicho kinachotofautiana kati ya mkoa na mkoa. Kitendo kilichofanywa na Serikali kwa wakulima wa zao la muhogo wa Mtwara Mikindani la kuwalipa shilingi 130 kwa shina, ni kitendo cha kudhalilisha mkulima na kilimo kwa ujumla wake. Wakulima wa Mtwara Mikindani kwa nyakati tofauti walilamikia kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali itoe maelezo, kwa njia hii ya uthamanishaji wa shina la muhogo kwa shilingi 130; je, kilimo kinaweza tumika kama nyenzo ya kuondoa umaskini au hiki ni kiini macho kwa wakulima?

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizo za uzalishaji wa muhogo hapa nchini na umuhimu za zao hilo katika uchangiaji kwenye kapu la chakula hapa nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Wananchi ni mkakati gani uliopo wa kuhakikisha kuwa kilimo cha mihogo hapa nchini kinaleta tija kwa Wananchi na Taifa katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi?

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa ngano kwa Tanzania siyo kipaumbele kwa maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Hii inatokana na ukweli kwamba, zao la ngano halina sera wala halimo kwenye vipaumbele vya kuliendeleza (masoko na viwanda vya kuongeza thamani).

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania, matumizi ya ngano katika orodha ya vyakula ni ya nne nyuma ya mahindi, muhogo na mchele. Hii inaonesha ni jinsi gani zao la ngano lilivyo na umuhimu kwa nchi yetu. Matumizi ya ngano kwa maeneo ya mijini ni takriban asilimia 83 na vijijini ni takriban asilimia 17.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya zao hili yameachwa mikononi mwa sekta binafsi iliyonunua mashamba makubwa na inamiliki viwanda vya usagishaji wa zao hilo. Jambo hili linapelekea wakulima wadogo ambao wametawanyika sana kumezwa na wafanyabiashara

wakubwa. Hata hivyo, Tanzania ina uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 164,000 kwa mwaka kama Serikali itaweka sera madhubuti ya kuhakikisha hata wakulima wadogo wanauza ngano yao kwa bei inayoweza kuwa na tija kwao, kama ilivyokuwa hapo awali wakati wakiuza kwa *NMC.*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ngano ya kawaida iliyopetwa kilo moja inauzwa kati ya shilingi 800 hadi 900, wakati bidhaa zitokanazo na ngano, mkate, chapati, keki, maandazi na kadhalika, bei zake zimekuwa zikipanda kila kukicha. Mkate wa gramu 500 unauzwa kati ya shilingi 1200 hadi 1700 na kwa upande wa chapati zinauzwa kati ya shilingi 200 hadi 500.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizi za ngano ni muhimu sana kwa Jamii ya Watanzania waishio mijini. Swali la msingi ni namna gani Serikali inahakikisha wakulima wadogo wa zao hilo na wao wananufaika na umuhimu wa zao hilo kwa jamii ziishizo mijini?

Mheshimiwa Spika, bei ya ngano kwa miaka miwili ya nyuma ilipanda kwa asilimia 65 kutokana na kutokuwepo kwa uhakika wa uzalishaji toka kwa nchi za Bulgaria, Georgia, Romania, Russia, Turkey na Ukraine *(Black Sea Countries).* Uagizaji wa ngano toka nje umeendelea kupanda na sasa inakadiriwa kuwa ni tani milioni moja wakati uzalishaji wa ngano kwa mwaka ni tani 100,000. Tofauti na uzalishaji na mahitaji ni kubwa sana na hii inaonesha ni jinsi gani fursa kwa wakulima wetu ilivyo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mbegu ya ngano kilo moja inauzwa kwa shilingi 5,000 na gunia la kilo 100 linauzwa kwa shilingi 500,000 na kwa kawaida kilo 100 za mbegu zinatosha kupanda hekta mbili tu. Hoja ni kwamba, kwa bei hiyo ya mbegu ni kweli mkulima mdogo ili aweze kunufaika na kilimo cha ngano alime hekta ngapi na bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko inafanya nini kwenye zao hili muhimu kusudi liongeze tija?

Mheshimiwa Spika, zao hili kwa muda mrefu

limeachwa na wakulima wake wameachwa kana kwamba wao hawazalishi zao lenye faida kubwa kwa Taifa hili na hasa katika kulipatia Taifa letu fedha nyingi za kigeni ambazo badala ya kuelekezwa kwenye kuimarisha viwanda vya kubangua korosho, vimeachwa vife na wakulima waendelee kuuza korosho ghafi nje ya nchi na hivyo hawapati faida kama ilivyotakiwa kuwa; mifano halisi ni kama ifuatavyo hapa chini ya viwanda vilivyouwawa:-

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya malalamiko au changamoto zinazotolewa na Bodi ya Korosho ni kuwa nanukuu: "Ukosefu wa bei ya uhakika ya kuuzia korosho ghafi; na utegemezi wa soko la nje la korosho ghafi. Zaidi ya asilimia 95 ya korosho ghafi tunayozalisha nchini inategemewa kununuliwa na nchi za nje. Zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi hununuliwa na wamiliki wa makampuni ya ubanguaji kutoka India, hivyo soko la korosho ghafi kuu kwa ujumla lina wanunuzi kutoka nchi moja wakati wauzaji ni wengi. Kwa sababu hiyo ni wazi kwamba, wanunuzi hao wana nafasi kubwa ya kukaa pamoja na kupanga bei. Kwa ujumla hakuna ushindani wa bei."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nukuu hiyo ya Bodi ya Korosho inaonesha kuwa, India imehodhi soko la korosho na hivyo wanapanga bei wao.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti nilizozifanya zinaonesha kuwa Vietnam nayo ni nchi inayonunua na kuuza Korosho ndani na nje. Kwa msimu wa mwaka 2011, ilinunua korosho ghafi takriban tani 450,000 na hizo zilitoka Afrika ya Mashariki, Afrika ya Magharibi na Indonesia, Australia, Uarabuni, Russia, Uchina na Nchi za Scandinavia.

Mheshimiwa Spika, kurudishwa kwa viwanda vya korosho vilivyouzwa na vikashindwa kufanya kazi iliyotarajiwa ndiyo ufumbuzi wa kudumu kwa Serikali kuingia kwenye masoko ya nchi wanunuzi nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mbali ya matatizo hayo ya soko, naomba kunukuu kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye

Taarifa Rasmi za Bunge ya tarehe 4 Februari, 2013, wakati akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage: "Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado korosho kwa kiasi kikubwa inabanguliwa India. Sasa tatizo tulilokuwa nalo ni kwamba, Korosho ya Tanzania ndiyo Korosho premium duniani, lakini hatujaifanyia branding kwa sababu kwenye hali ya kukandamiza hii hali ya Korosho kuna maslahi kwa watu wengi ambayo inawakandamiza wakulima."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili maslahi ya watu wengi ambayo yanawakandamiza wakulima. Tunaitaka Serikali iwataje watu hao ili Bunge liweze kuishauri Serikali vizuri jinsi ya kushughulika na kundi hilo linalokandamzia maslahi ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa mashamba, viwanda na mashirika ya umma hapa nchini hasa vilivyokuwa kwenye Sekta ya Kilimo vimekuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kuzalisha chini ya kiwango na kutoendelezea kabisa. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, mashamba yote hasa yale ya *NAFCO, BASOTU, KAPUNGA* na ya *CHAI-TUKUYU*, yaendeshwe chini ya ushirika kama ilivyo kwa maeneo mengine ya Mbarali na Mvomero, Wananchi kuondokana na umaskini na kupunguza idadi kubwa ya Watanzania wasiokuwa na ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30, 2010 kama ilivyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 17 Aprili, 2012 kuhusu tathmini ya viwanda vya korosho.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho cha Likombe kipo Mjini Mtwara na kilijengwa mwaka 1980 kwa kutumia teknolojia ya Kijapani. Kwa Mwaka 2004, kiwanda kiliuzwa kwa Kampuni ya *Micronix System Limited* kwa bei ya shilingi milioni 100 ambayo alikwishalipa.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda hakijawahi kuzalisha tangu kilipobinafsishwa mwaka 2004. Mwekezaji hajafanya

ukarabati wowote wa mashine zilizokuwepo kiwandani ila amenunua mashine nne mpya za upakiaji ambazo ni *mixing, packing, drying na humidifier machines.* Aidha, ilibainika kuwa mwekezaji amekodisha sehemu ya ghala kwa kampuni binafsi ambayo inaendesha zoezi la kutunza korosho kwa mtindo wa stakabadhi ghalani na pia amekodisha sehemu ya kiwanda kwa Kampuni ya Olum, ambayo inafanya shughuli za ubanguaji wa korosho kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho cha Mtama kipo Lindi Vijijini na kilijengwa mwaka 1978 kikiwa na uwezo wa kubangua tani 5,000 za korosho kwa mwaka. Kiwanda kiliuzwa kwa Kampuni ya *Lindi Farmers Company Limited* mwaka 2005 kwa bei ya shilingi milioni 30.0 ambayo amekwishalipa. Hadi kinabinafsishwa, kiwanda kilikuwa katika hali nzuri na kwamba yalihitajika matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho cha Lindi kipo Mjini Lindi na kilijengwa kuanzia mwaka 1977 kwa kutumia teknolojia ya Kitaliano na kilikuwa na uwezo wa kubangua tani 10,000 za korosho kwa mwaka. Kiwanda kilifanyiwa majaribio mwaka 1978 na kuendelea kufanya kazi hadi mwaka 1996, kiliposimama. Mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa Kampuni ya Bucco Investment Holdings Limited kwa bei ya shilingi milioni 50.0.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji alitakiwa kuwekeza kiasi cha Dola za Kimarekani 600,000 kwa ajili ya ukarabati wa kiwanda. Mwekezaji amefanya ukarabati kwa gharama ya shilingi milioni 250. Maeneo yaliyofanyiwa ukarabati ni boiler, mashine za kukatia korosho na grading. Kiwanda kimesimama kwa kukosa mtaji wa uendeshaji. Ni wazi kuwa, mwekezaji amevunja Mkataba wa Mauzo kwa kushindwa kufufua kiwanda.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho Newala II kipo Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara. Ujenzi wake ulianza mwaka 1977 na kukamilika mwaka 1980, kwa kutumia teknolojia ya Kijapani na kilikuwa na uwezo wa kubangua

tani 10,000 za korosho kwa mwaka. Kiwanda kilifanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na kisha kusimama kutokana na uhaba wa korosho ghafi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa Kampuni ya *Micronix Sytems Ltd.* kwa bei ya shilingi milioni 75.0. Mwekezaji alikwishalipa fedha zote na kukabidhiwa kiwanda. Hadi wakati kiwanda hiki kinabinafsishwa, sehemu kubwa ya kiwanda ilikuwa katika hali nzuri, ukiacha matengenezo ya sehemu kadhaa kutokana na kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na mpango wa uwekezaji, mnunuzi alitakiwa kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 3.64 katika ukarabati wa kiwanda kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2006 mpaka 2010 kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Mauzo. Mwekezaji alieleza kuwa amewekeza kiasi cha shilingi milioni 150 katika ukarabati wa kiwanda kwa kununua mashine za kutumia teknolojia ya mkono. Ukarabati huo ulifanyika mwaka 2009. Mashine za zamani zimekusanywa na kurundikwa sehemu moja kwa kile mwekezaji anachodai kuwa teknolojia yake imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho Newala I kipo Mjini Newala, Mkoa wa Mtwara, kilijengwa mwaka 1976 na kufanyiwa majaribio mwaka 1981 na hakikufanya kazi baada ya majaribio ya awali. Kiwanda hiki kilijengwa kwa mitambo ya teknolojia ya Kitaliano yenye uwezo wa kubangua tani 10,000 kwa mwaka. Aidha, kwa maelezo ya Uongozi wa Shirika Hodhi la yaliokuwa Mashirika ya Umma *(CHC),* mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa Kampuni ya Agrofocus Limited kwa bei ya shilingi milioni 75.0. Mwekezaji alikwisha kamilisha malipo. Hadi wakati kinabinafsishwa, mitambo na mashine ya kiwanda vilikuwa katika hali nzuri, ukiacha sehemu chache za umeme na mikanda ya kusafirishia korosho. Aidha, majengo ya kiwanda yalikuwa katika hali nzuri isipokuwa sehemu kadhaa za paa ambazo zilihitaji ukarabati ili kuzirejesha katika hali ya kawaida.

Mwekezaji amewekeza kiasi cha shilingi milioni 718.0 katika ukarabati wa kiwanda. Mashine zote zimekarabatiwa na zinafanya kazi. Kiwanda kipo katika hali nzuri, mazingira ni safi na majengo yote yamepakwa rangi. Mashine pia zipo katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya Tathmini, Kamati haijaridhishwa kabisa na zoezi la ubinafshishaji wa Mashirika ya Umma katika Sekta Ndogo ya Viwanda vya Korosho (Mamlaka ya Korosho). Viwanda vyote vya kubangua korosho vilivyojengwa kwa Mkopo wa Benki ya Dunia vyenye thamani ya Dola milioni 284 havifanyi kazi. Wawekezaji waliovinunua wamevigeuza kuwa maghala ya kuhifadhia korosho na nchi inaendelea kupata hasara kubwa kwa kusafirisha korosho ghafi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kutoa tathmini hiyo kama nilivyoinukuu, ilitoa mapendekezo yake ambayo Bunge hili liliridhia na baadaye kuwa ni Azimio rasmi la Bunge. Naomba kunukuu Azimio hilo la Bunge kama lilivyo kwenye Taarifa ya Kamati ya *POAC* ya tarehe 17 Aprili, 2012.

"Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika tathmini yake ya viwanda vilivyobinafsishwa vya ubanguaji korosho, imebainika kuwa baadhi ya wawekezaji wamekiuka kwa makusudi mikataba ya uendeshaji wa viwanda hivyo; na kwa kuwa kwa kufanya hivyo wamesababisha Taifa kuendelea kusafirisha korosho ghafi kwenda Nje ya Nchi na hivyo kuondoa fursa ya wakulima kupata faida ya kutosha na kupunguza ajira nchini; kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa Serikali ichukue uamuzi wa kuvirejesha viwanda vyote vya kubangua korosho vilivyobinafsishwa na wawekezaji wake kushindwa kuviendeleza ili kuona namna bora ya kuwekeza kwenye ubanguaji wa korosho ikiwa na pamoja na Serikali kusisitiza umuhimu wa kuuza korosho iliyobanguliwa nje ya nchi kwa kuwajengea uwezo wakulima wa kubangua Korosho."

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata

majibu utekelezaji wa Azimio hili umefikia wapi mpaka sasa kwani kutokutekelezwa kwa Azimio hili ni kuendelea kuwaumiza Wananchi wetu ambao ni wakulima na ambao hawapati pembejeo kwa wakati, dawa na sasa hata bei nzuri hawapati.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kahawa Tanzania *(TCB)* ni Taasisi ya Umma iliyoundwa kwa Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Bodi za Mazao Namba 23 ya mwaka 2001, pamoja na majukumu mengine lakini ya msingi yakiwa ni kusimamia Sekta ya Kahawa Tanzania; nakuishauri Serikali mambo ya msingi juu ya mikakati ya kuendeleza kilimo na biashara ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, dira ya bodi inasema kuwa; "Kuwezesha mazingira mwafaka kwa maendeleo endelevu ya Sekta ya Kahawa nchini Tanzania." Kwa kadiri iwezekanavyo, maendeleo endelevu katika Sekta ya Kahawa hayawezi kufikiwa ikiwa bei anayopata mkulima wa kahawa haiwezi kuzidi gharama za uzalishaji. Hii ni kudanganyana na kumfanya mkulima aendelee kuwa tegemezi na maendeleo endelevu kwa sekta hayawezi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa Bodi hii, zao hili la kahawa limeendelea kudidimia siku hadi siku kutokana na wakulima kukosa pembejeo kama madawa, mbegu bora na wataalamu wa kutosha. Aidha, viwanda vya kubangulia kahawa vilivyojengwa wakati wa utawala wa Mwalimu Nyerere leo hii viko hoi bin taabani.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuna mkakati gani na mpango gani endelevu wa kulifufua zao hili pamoja na viwanda vya kubangua na kusindika kahawa ili kuliwezesha Taifa kupata faida kutokana na kilimo cha zao hili.

Mheshimiwa Spika, pamba ni zao kuu la biashara na ni la pili kwa kuingiza fedha za kigeni baada ya kahawa. Pamba inachangia asilimia 24 ya mauzo yote ya bidhaa za

kilimo nje ya nchi na inachangia asilimia nne ya mauzo yote nje ya nchi. Takriban hekta 400,000 zinatumika kwa ajili ya kilimo cha pamba kwenye wilaya zaidi ya 40 za mikoa 13 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, uzalishaji wa zao la pamba nchini umeongezeka kutoka kilo milioni 168 msimu wa mwaka 2010/11 hadi kufikia kilo milioni 224 katika msimu wa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, wakati akiongea na wawekezaji kutoka Algeria ambao pia ni wafanyabiashara mashuhuri Duniani, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika wa wakati huo, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe alisema: "Msimu huu uzalishaji wa Pamba umeongezeka kwa kiasi kikubwa ambacho hakijawahi kutokea kwa kipindi cha miaka 50 iliyopita."

Kauli hiyo ya Waziri iliongezewa nguvu na Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba nchini, kwa kusema kuwa; "Ongezeko hilo limechangiwa na Serikali kwa kutoa ruzuku za pembejeo. Aidha, alisema pia kuyumba kwa bei ya pamba ambayo ni kati ya shilingi 1,100 mpaka shilingi 800 kwa kilo, kunachangia wakulima kutoongeza bidii ya kilimo cha zao hilo."

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kuwa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa cha pamba kuliko nchi nyingine zilizopo Kusini na Mashariki mwa Bara la Afrika. Hivi sasa asilimia 70 ya pamba, inauzwa nje huku viwanda vya ndani vikitumia asilimia 30 na matumizi haya ya asilimia 30 siyo kwa ajili ya kutengeneza nguo bali ni kwa ajili ya kusokota nyuzi kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi. Huu ni uzembe mkubwa au hujuma kwa Watanzania, jambo linalopelekea kuendelea kuagiza mitumba toka nje na kuwa nchi ya wachuuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wakulima wetu kujitahidi kuzalisha kwa wingi kiasi hicho ambacho kimevunja rekodi ya uzalishaji kwa miaka 50, ila bado bei ya Pamba imekuwa ni ndogo sana ukilinganisha na uhalisia wa gharama

halisi za uzalishaji kama vile mbegu, madawa na gharama nyingine za uzalishaji wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha mkataba kimekuwa ni sumu kubwa sana kwa wakulima wa pamba na hivyo kupelekea wakulima kuona kuwa ni afadhali waachane na kilimo wajihusishe na shughuli zingine. Ili kilimo hiki kiwe na manufaa kwa mkulima, inabidi uzalishaji kwa hekari uongezeke. Katika kufikia hilo, *ginneries* ndizo ziwe na jukumu la kuhakikisha kuwa matatizo ya mkulima yanatatuliwa, lakini mkataba huo wa mkulima na hizo ginneries umwache huru kuuza pamba yake kwa mnunuzi yeyote atakayetoa bei nzuri, ila imlazimu mkulima kulipa gharama zote zilizotumiwa na ginneries katika kumfanya azalishe.

Mheshimiwa Spika, katika kuwekeana mikataba inabidi bei dira iwekwe katika mkataba na pia ielezwe kuwa uwepo uthamanishaji halisi ya nguvu za mkulima katika mchakato mzima wa uzalishaji. Katika hali hiyo mkataba uwe sawa kwa wakulima walioko kwenye maeneo au wilaya moja.

Mheshimiwa Spika, wote ni mashuhuda katika mdororo wa uchumi, hasara iliyotokea iliangukia kwa mkulima na mfanyabiashara alipata fidia toka Serikalini. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pale hasara inapotokea, mkulima awe wa kwanza kupatiwa fidia badala ya mfanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, hoja siyo kuendelea kuongeza ruzuku za pembejeo au bei za malighafi, ukifanya *marginal analysis (price - unit cost)* ya mazao uliyoorodhesha, utakuta kwamba mkulima anapata kama asilimia 12 ya total margin katika *value chain* wakati mwenye kiwanda anapata zaidi ya asilimia 50. Kwa mazao ambayo hayaendi viwandani, mkulima hupata kama asilimia 30 na mfanyabiashara hupata zaidi ya asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano: Leo mkulima wa kule Mwanza anauza kilo moja ya pamba kwa shilingi 600. Kilo hii

inatoa mashati manne na kila shati moja la pamba halisi likiuzwa kwa dola 50 ni sawa na shilingi 80,000. Hivyo, kwa kilo moja ni sawa na shilingi 320,000. Mwenye kiwanda (Mzungu) anatumia shilingi 10,000 tu kwa kilo kama gharama za ununuzi, usafirishaji (kupeleka pamba Ulaya na kurudisha shati Mwanza) na uchakataji kiwandani. Faida yake ni shilingi 310,000 kwa kilo moja. Hata kama angechukua shilingi 10,000 zingine akatupatia "msaada" wa kutujengea barabara kutoka Dodoma hadi Mwanza ili akunyonye vizuri zaidi kwa kupunguza gharama za usafirishaji, bado ana faida ya shilingi 300,000.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, tunaitaka Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Pamba kujenga kiwanda cha Pamba katika mojawapo ya mikoa inayolima Pamba ambacho kitakuwa na jukumu la kuongeza thamani ya Pamba yetu.

Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu ya kina kuwa Serikali ina mpango gani wa kuinua wakulima wa zao hili muhimu hapa nchini na hasa katika kuwapatia bei nzuri ya Pamba inayoendana na gharama halisi za uzalishaji wa kilo moja ambayo sasa imekuwa kubwa sana, wakati inatafakari uanzishwaji wa kiwanda cha Pamba.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji unaotakiwa kufanyika katika Mpango wa *SAGCOT* ni katika Sekta ya Sukari au ulimaji wa miwa. Kilimo cha miwa kimetawaliwa na kuhodhiwa kwa kiasi kikubwa na viwanda vinavyozalisha sukari, kwani viwanda hivyo ndivyo vinavyopanga bei na muda wa kununua miwa toka kwa wakulima wanaozunguka viwanda hivyo. Katika mchakato huo wa kikiritimba, anayeumia ni mkulima. Hoja ni kwa vipi tunamnasua mkulima katika mtego huo wa wenye viwanda? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufumbuzi wa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kanuni zinazowataka wakulima wanaozunguka kiwanda cha sukari waliondani ya kilometa 40 kutoka kilipo kiwanda cha sukari wanalazimishwa kuuza miwa yao kwenye kiwanda, japokuwa kanuni hiyo walidhani

wanamsaidia mkulima kusafirisha miwa yake kufika kiwandani, lakini ukweli ni kwamba ni ujanja wa kuvilinda viwanda na ushindani unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kanuni hii inazidisha ukiritimba kwa viwanda na kuwanyima haki ya msingi wakulima ambao kwa kutumia ushirika wao, wana uwezo wa kuanzisha kiwanda kikubwa au kidogo cha kutengeneza sukari. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya kanuni hiyo ili iendane na mazingira yaliyopo sasa. Aidha, tunaitaka Serikali kupitia *SIDO* kuanzisha viwanda vidogo ambavyo vitakuwa na ubia na wazalishaji wadogo wadogo (cane outgrowers) katika maeneo mbalimbali yazalishayo miwa hapa nchini. Hii itaondoa tatizo kubwa la sukari linaloikabili nchi yetu na pia ni njia mojawapo ya kuondoa umaskini wa kipato kwa wakulima na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, licha ya mabadiliko yaliyotokea katika mfumo wa uchumi katika miaka ya karibuni ambapo Sekta za Madini, Utalii na Huduma zimekua kwa kasi, Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia ajira Watanzania zaidi ya asilimia 70 na inachangia wastani wa asilimia 95 ya chakula kinachohitajika nchini. Katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo ilikua kwa wastani wa asilimia nne na ilichangia asilimia 26 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, toka mwaka 2001/2002, bajeti ya kilimo imekuwa ikiongezeka taratibu, mwaka huo mgawo ulikuwa shilingi bilioni 52.1, ambayo ilikuwa sawa na asilimia 3.0 ya bajeti ya mwaka 2001/2002, toka hapo bajeti imekua mara dufu hadi kufikia asilimia 7.8 ya bajeti kwa mwaka 2010/2011, lakini kwa mwaka 2011/2012 ilishuka na kuwa asilimia 6.9.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi hicho cha 2001/2002 - 2012/2013, kumekuwa na uhusiano usiorodhisha kati ya bajeti ya maendeleo na bajeti ya matumizi ya kawaida. Bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa ikiongezeka wakati ile ya maendeleo imekuwa ikishuka; kwa mfano, kwa mwaka 2001/2002 bajeti ya

matumizi ya kawaida ilikuwa asilimia 39.5 ya bajeti nzima ya wizara na mwaka 2008/2009 ilipanda hadi kufikia asilimia 82.4 na mwaka 2011/2012 ilipungua na kuwa asilimia 59.0. Wakati bajeti ya maendeleo mwaka 2001/2002 ilikuwa asilimia 60.5 na mwaka 2011/2012 ilishuka hadi kufikia asilimia41.0.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa tafakuri ya takwimu hizo, inaona ni wazi kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kuwekeza katika kilimo kwani hata bajeti inayokwenda kwenye wizara sehemu kubwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu.

Mheshimiwa Spika, mbali na kupanda na kushuka kwa bajeti inayotengwa kwa kilimo hapa nchini, bado kuna tatizo la utoaji wa fedha pungufu kulinganisha na zile zinazopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, takwimu zinaonesha kwamba, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, kwa upande wa fedha za *ASDP,* Hazina ilitoa Shilingi bilioni 107.1 kwa wizara zinazojihusisha na kilimo (Agriculture Sector Lead Ministries), kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Kati ya fedha hizo, ni kiasi cha shilingi bilioni 77.9 (asilimia 72.8) ndizo zilizotumika hadi mwisho wa mwaka huo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake nini kwa nchi ambayo mara zote taarifa zinatolewa kuwa Miradi imekwama kutokana na ukosefu wa fedha, ni dhahiri kuwa inawezekana tatizo la utoaji wa fedha za miradi nje ya muda bado linaendelea pia uwezo mdogo wa watendaji katika utumiaji wa fedha. Ujumla wa haya yote ni kukifanya kilimo kuendelea kudumaa na kushindwa kutoa tija inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inasema kama mipango hiyo ipo tayari kwenye makaratasi tatizo ni utekelezaji. Serikali ya CCM haiwezi kutekeleza mipango hiyo kwani imekuwa ikifanya hivyo siku zote. Naomba kunukuu kauli

iliyokwishatolewa hapa Bungeni kwamba, *insanity is keeping doing the same thing expecting different results.*

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa miji kimekuwa ni kichocheo kikubwa cha mchakato wa maendeleo kutokana na uwepo wa forward and backward linkages kwa bidhaa nyingi za kilimo na viwandani. Njia hii imekuwa na mafanikio makubwa kwa nchi nyingi hasa zile zilizoendelea ikiwemo China na Korea ya Kusini na nyingine kama vile India, Thailand, zimejikwamua kutoka kwenye umaskini wa kipato kupitia ukuaji wa miji midogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya Sera ya Kilimo ili iweke mazingira wezeshi kwa wakulima wadogo waweze kunufaika na kukua na kuwa wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*), yalikubaliwa na Wakuu wa Nchi mbalimbali Duniani Septemba mwaka 2000 kwamba, mwaka 2015 ni tarehe ya mwisho ya kufikiwa kwa malengo nane ambayo pamoja na mambo mengine, yanalenga katika kuondosha umaskini wa kipato na njaa. Lengo linalohusu moja kwa moja Sekta hii ya Kilimo. Ukweli ni kwamba, hata kipindi cha kukamilika kwa Malengo ya Maendeleo kingeongezwa, ni dhahiri tusingeweza kuondoa umaskini wa kipato na njaa kutokana na kushindwa kutambua kiini hasa cha matatizo ya wakulima na kilimo.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Nchi ya Thailand katika kupambana na kuushinda umaskini halikuwa jambo rahisi na la siku moja, bali ni matokeo ya uwekezaji makini na nia thabiti ya kisiasa ambayo ilichangiwa na mambo mengi ikiwemo uwekezaji wa nishati vijijini. Asilimia 97 ya Wananchi waishio vijijini Thailand, wanapata umeme wa uhakika, jambo hili linaenda sambamba na uzalishaji kwenye Sekta ya Kilimo wenye tija.

Mheshimiwa Spika, ni kwa namna gani Tanzania tunaweza kufanya ulinganisho na wenzetu hao? Takwimu za

bajeti ya kazi toleo la mwaka 2007 zinaonesha kuwa ni asilimia 2.5 tu ya Watanzania waishio vijijini ndiyo waliounganishwa na Gridi ya Taifa. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wakati alipokuwa anazungumza na Watanzania waishio Nchini Uingereza alisema kuwa: “Asilimia 18.4 ndiyo wanaotumia umeme hapa Tanzania na kati ya hao ni asilimia 6.6 tu wako vijijini.”

Sambamba na hilo, kwa mujibu wa mtandao wa Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuwa: “Hapa nchini takriban asilimia 14 tu ya Watanzania ndiyo wanaotumia nishati ya umeme na kwamba hali ni mbaya zaidi vijijini wanakoishi takriban asilimia 80 ya Watanzania, ambapo ni asilimia 2.5 tu ndiyo wanaotumia umeme kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Wananchi wakati upatikanaji wa nishati hizo nao hautoshelezi.”

Mheshimiwa Spika, akiwasilisha bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 yenye kaulimbiu “KILIMO KWANZA”, Waziri wa Fedha wa wakati huo, Mheshiniwa Mustafa Haidi Mkullo alisema: “Misingi na shabaha ya bajeti hii umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ambayo inalenga kuwa Tanzania iwe ni nchi yenye kiwango cha kati cha mapato... na hali bora ya maisha kwa Wananchi, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, MKUKUTA, Mpango Maalum wa Maendeleo Tanzania na Malengo ya Maendeleo ya Milenia.” alisema Waziri Mkullo: “Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kuwa kilimo kinapatiwa rasilimali zaidi ikiwemo pembejeo na zana za kilimo”.

Mheshimiwa Spika, Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA ambayo ni mwendelezo wa Sera ya Kilimo ya mwaka 1997 imeonesha na inaelekea kushindwa kukidhi malengo kutokana na ukweli kama ulivyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa *SAGCOT* katika mahojiano yake na Gazeti la Kiingereza la Business Times kuhusiana na mada ya faida na hasara za KILIMO KWANZA alisema nanukuu: *“It is true the KILIMO KWANZA initiative will bring fundamental changes in Tanzania, but this cannot happen overnight; there is a need to wait for other developments to support it, such as*

*infrastructure, rural electrification and construction of enough warehouses, good market system for agricultural products."* Kwa tafisiri isiyo rasmi kuwa ni ukweli kwamba, mpango wa KILIMO KWANZA utaleta mabadiliko ya msingi hapa Tanzania, lakini jambo hili halitatokea ghafla; hivyo, ni muhimu kuwa na maendeleo mengine ya kusaidia mpango huu kama vile miundombinu, nishati ya umeme vijijini, ujenzi wa nyumba za kutosha, mifumo mizuri ya masoko kwa ajili ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo huo na ukweli huo, hadi kupatikane maendeleo kwenye sekta hizo wezeshi itatuchukua miaka mingine mingapi?

Mheshimiwa Spika, toka wakati huo hadi sasa Watanzania hawaoni tofauti katika kilimo na kuna wanaoona kwamba kilimo kimeshuka kwa kulinganisha na miaka ya nyuma. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuangalia jinsi ya kuendeleza shughuli mbalimbali zisizokuwa za kilimo *(non farm activities)* zinazofanywa na wakazi wa vijijini, ili kusaidia kukuza hali ya kibiashara katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na fadhila, kwa kunijalia uhai, afya njema na kwa upendo wake anaotujalia kila mmoja wetu kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Chama makini cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Makamanda wenzangu wote, kwa mchakato wa mwanzo wa kuifungua nchi yetu kwa kurudisha madaraka ya kiutendaji kwa Wananchi kupitia *M4C.*

Mheshimiwa Spika, kama sitawashukuru Wananchi wa Wilaya ya Hanang', nitakuwa sijawatendea haki kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kuhakikisha Wilaya yetu inakuwa kiongozi katika kupambana na ufisadi katika Miradi ya Maji na ile ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu hasa wanangu; Emiliana na Linus. Nasema tuendelee kuvumiliana kwa kipindi chote nitakachokuwa kwenye uhamasishaji wa *M4C.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji lakini kwa asubuhi naweza kuwa nao wachangiaji sita. Naomba kueleza kwamba, zile fomu mlizoleta mkaleta priority yenu, ukiondoa Wizara tulizomaliza nyingine mnaweza kuja kuomba kubadilisha kama hamkuona, lakini siyo kuja kuniomba mimi, nikishaweka hapa nakwenda na priority ya kwanza, ya pili na sifanyi vinginevyo.

Kwa hiyo, kwa Wizara ambazo hazijaingia mnaweza kubadilisha, zilizoingia ndiyo majina yatakayofuata. Kwa hiyo, mchangiaji wetu wa kwanza sasa atakuwa Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Nkumba. Mheshimiwa Chibulunje ajiandae, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu ajiandae, Mheshimiwa Engineer Ramo Makani ajiandae, Mheshimiwa Susan Kiwanga ajiandae, Mheshimiwa Jerome Bwanausi ajiandae, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka ajiandae, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda ajiandae, Mheshimiwa Titus Kamani ajiandae, Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae na wengine nitawataja baadaye.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare interest;* niko humu ndani siku ya leo kama Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kahama na kwa misingi hiyo, nitakayoyasema, hoja nitakazoziweka mbele ya Bunge lako Tukufu, zinatokana na

Wananchi walionifanya niingie ndani ya Bunge hili na si vinginevyo. Baada ya kusema hayo na kuwa nimeifuatilia kwa karibu sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nasema siungi mkono hoja. Nimefuatilia Hotuba ya Waziri, sijaona mahali ambapo amekuja na maelezo ya msingi ya kutatua matatizo ya wakulima hapa nchini. Ni ukurasa wa 50 tu ambapo amezungumzia Serikali kuwa imekamilisha rasimu ya mapendekezo ya kuanzisha Mfuko Maalum wa kulinda bei ya mazao basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine kwa kweli ni nadharia na yanawaacha wakulima hapa nchini kote katika mazingira magumu sana, mazingira ya kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii kwa sababu kule Kahama wakulima wa pamba, wakulima wa tumbaku ...

**SPIKA:** Naomba uendelee kuongea na mimi. Amesemaje sikusikia?

**TAARIFA**

**MHE. APHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Lembeli kwamba, katika ukurasa huo wa 50 anaosema kwamba Wizara imekuja na majibu kwamba kuna rasimu juu ya kutatua matatizo ya bei ya wakulima wa pamba. Nilikuwa naomba nimpe taarifa kwamba, hiyo taarifa siyo sahihi kwa sababu kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, hakuzungumzia kuwepo kwa rasimu hiyo. Kwa hiyo, inaonekana wazi, nimpe taarifa kwamba, hiyo taarifa ya Waziri wa Kilimo anatudanganya hapa kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema haipo.

**SPIKA:** Naomba utulie chini wala siyo taarifa kwa mtu yeyote na wala haina maana yoyote. Naomba Mheshimiwa Lembeli endelea.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika zangu uzilinde. Mimi nilikuwa nasema katika ukurasa huu wa 50 nilichoweza kukiona ni taarifa njema kwa wakulima, ni maelezo haya kwamba, Serikali imekamilisha rasimu ya mapendekezo ya kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia bei ya mazao. Hii ni taarifa njema, sasa whether ni kweli au siyo kweli, tutayaona baada ya muda mfupi.

Kweli nitakuwa siwatendei haki wakulima wa mazao hususan ya tumbaku na pamba wa Jimbo la Kahama na Wilaya ya Kahama, ambako ni wazalishaji wakubwa. Wakulima wa Zao la Pamba nchini kwa miaka mitatu sasa bei ya Zao hilo imekuwa ikiteremka. Miaka mitatu mfululizo, hawa watu ni maskini, akilima heka moja ya pamba kipato chake hakizidi shilingi laki mbili; amejitahidi sana. Sasa leo mwaka wa tatu Serikali inasema imekuja na rasimu, inakamilisha; haya maneno ni maneno ya ku...

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka hapo Serikali itakaposema mwaka huu, kwa mfano, imejiandaa vipi endapo bei ya zao la pamba itakuwa imeteremka kuhakikisha kwamba wakulima wanafidia jasho lao. Hawa wanashinda vijijini, wanalima mashambani na dakika ya mwisho wanaletewa bei ambayo haina mbele wala nyuma. Kwa misingi hiyo, nasema siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwa Zao la Tumbaku. Katika Jimbo langu la Kahama kuna Kata zisizopungua tano wanazalisha tumbaku. Tumbaku nzuri na wanaliingizia Taifa wao wenyewe takriban shilingi bilioni 15 kila mwaka. Wananchi hawa nimepiga kelele sana, Mkuu wa Wilaya ya Kahama amezunguka amepiga kelele sana, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, wote wamefanya kazi nzuri kusikiliza kero za Wananchi lakini Serikali haisikii. Wakulima wa Tumbaku wa Jimbo langu wanaibiwa kimachomacho. Wakulima wa TUMBAKU wanabambikiziwa madeni, matokeo yake mwisho wa mwaka hawalipwi. Tumepiga kelele, nimemwomba ndugu yangu Mheshimiwa Waziri aje atembelee maeneo hayo; sijui ameweka nini kwenye masikio yake! Matokeo yake Viongozi wa Serikali na mimi niseme tu hapa; Afisa Ushirika

wa Wilaya ya Kahama yupo pale kwa maslahi ya nani? Huyu ndiye kinara wa kuchonga wizi, ndiye anayepitisha malipo yote ya wakulima wa vyama vya msingi, ndiye anayepitisha viongozi wabovu ambao kazi yao kila siku ni kuwaibia wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko kimya; kwa nini niunge mkono hoja? Najua maneno haya kuna wengine wataudhika lakini siyo kazi yangu, ukizingatia niko hapa kuzungumzia yale ambayo yanawasibu. Nitataja baadhi ya Vyama vya Msingi katika Jimbo la Kahama ambapo Wananchi kwa miaka miwili mfululizo wamelipa tumbaku, wameuza hawajalipwa mpaka leo.

Niko tayari kesho twende Kahama nimpeleke kwenye Vyama vya Msingi, wamelima miaka miwili iliyopita mpaka leo hawajalipwa na wale ambao wamelipwa mwaka huu tumbaku yao mwakani hawawezi kulipwa kwa sababu Viongozi wa Vyama vya Msingi wamekwenda kukopa fedha benki ili kulipa mauzo ya mazao ya msimu huu. Kwa maana nyingine, tumbaku iliyoko shambani sasa hivi imelipwa kwa mkopo.

Mheshimiwa Spika, hivi hii nchi tunataka tuipeleke wapi; na kwa nini watu wanapoteza pesa kuzunguka vijijini kuhimiza watu walime halafu matokeo yake mkulima analima anatoka jasho hawezi kufanya shughuli nyingine hata zile za jioni kwa sababu amechoka kuchoma tumbaku and then Serikali haiwasaidii. Naomba niseme baadhi ya Vyama vya Msingi ambavyo vimetapeliwa, vimeibiwa na hivi ninavyovisema vingine vya kijijini kwangu Kata ninayotoka ya Mtaganya, Kata ya Namatutu, Kata ya Migamba, Kata ya Mweli, vyote katika Kata ninayotoka mimi ya Bulungwa. Lakini vipo vingine vya Twende na Wakati, Kata ya Uloa, Nsungansabi, Kata Uyogo, Kidana, Ushetu, Nyenyera Ushitu, Mihama Ushetu, Wananchi kule wameibiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye zao hili la tumbaku; hivi ni kwa nini mkulima tumbaku yake inanunuliwa kwa dola, pembejeo anakopeswa kwa dola, malipo

analipwa kwa shilingi? Hii ni biashara ya wapi? Ni wizi mtupu, mkulima hajui thamani kama tumbaku yake inauzwa kwa dola 1.26, senti sita ni shilingi ngapi? Mkulima wa kawaida kule kijijini anajua? Mimi najiuliza kama kweli Serikali iko tayari kuwasaidia; mimi nina *account* ya dola kwa nini huyu mkulima huyu wa tumbaku asiruhusiwe kufungua *account* mbili; moja ya dola ambako malipo yake yote yatapelekwa akitaka kubadilisha siku anayotaka na kwa *exchange rate* iliyo nzuri abadilishe na hela iingie kwenye akaunti yake ya shilingi. Sasa wizi, wakulima kule wako hoi, sisi tumo humu ndani tunazungumza na viyoyozi, wao wanaungua na jua hakuna mtu wa kuwatetea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siwezi kuunga mkono hoja hii mpaka haya niliyoyasema yatolewe maelezo ambayo yataniridhisha mimi na wakulima wa tumbaku kule vijijini. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi nizungumzie Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Naomba niseme bila kutafuna maneno kwamba, kwa hakika kabisa sitakubaliana na bajeti hii kwa lugha ya kawaida tuliyoizoea, ni kwamba, siungi mkono hoja hii. Ninasema hivyo nikikubaliana sana na hoja zilizotolewa na kaka yangu Mheshimiwa Lembeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu asiyejua nchi hii kwamba, Wilaya au Mkoa ambao una njaa kuliko Wilaya zote au Mikoa yote ni Mkoa wa Shinyanga. Njaa ya Mkoa wa Shinyanga imekuwa ni ya historia, lakini kwa kifupi hakuna kinachofanyika cha kukabiliana na tatizo hili. Watu wa Shinyanga tumewafanya kuwa ni watu wa kupokea msaada wa chakula kila wakati na mbaya zaidi kutokana na kuharibika kwa mazingira kwao, lakini pia kutokana na ukosefu wa ardhi na ni wachapakazi wazuri, wakiwa ni wakulima na wafugaji, wanapohama kutoka Mkoa wa Shinyanga wakiwa na mifugo yao kwenda kuishi na kulima sehemu zingine nako wanakataliwa kupokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika matendo ya namna hiyo,

sitarajii Mbunge wa Mkoa wa Shinyanga au mtu yeyote anayetoka Mkoa wa Shinyanga, anaweza akakubaliana na mipango ya Serikali iliyowasilishwa hapa. Kwa hakika tunajua kwamba, Mkoa wa Shinyanga una njaa na mvua zinanyesha, inawezekana kabisa ya kuwa na mipango mizuri ya kuondokana na tatizo la njaa kwenye mkoa huu na jibu la uhakika ni kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabonde mazuri yapo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika na amefika kwenye bonde zuri sana linalitwa Chela, lakini pia Waziri wa Kilimo ni rafiki yangu, tumekuwa tukizungumza naye mara kwa mara. Naamini kwa hapa tulipofika, Wananchi wa Shinyanga ni marafiki zangu zaidi kuliko Mheshimiwa Waziri. Hatuwezi tukaendelea na hali tuliyonayo, hakuna skimu hata moja ya umwagiliaji Shinyanga huku tukijua kwamba, mvua zinanyesha.

Juzi mmemsikia Mheshimiwa Opolukwa, Mbunge wa Meatu, ambao ni Mkoa dada; mvua zimenyesha mafuriko yametokea, maji yamekwenda, hakuna kilichofanyika cha kuyatunza yale maji. Inawezekana kabisa maji yale yakatunzwa, kilimo cha umwagiliaji kikafanyika, tuna mabonde mazuri, Jimbo la Msalala na Jimbo la Solwa, kuna bonde zuri kabisa ambalo linaweza likawa sawa na Mbarali. Mpunga unaozalishwa Mbarali ni kidogo sana ukilinganishwa na ule unaozalishwa Solwa, Salawe, Mwakitolyo, Chelya, Bulige, Kinaga, Isakajana na sehemu zingine kama Segese. *0*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya ambayo tunaona kabisa kwamba kilichofanyika ni kutokujali kilio cha Wananchi wa Shinyanga kuhusu matatizo yao. Katika mazingira haya, mimi nikiwa Mbunge wa eneo hilo, niseme kwamba sikubaliani. Uchumi wa Mkoa wa Shinyanga unalindwa kwa kilimo cha pamba kama zao la biashara. Tumeangalia mipango ya Serikali kwenye zao hili, hakuna ambacho kimefanyika kinachoendana na uzito wa tatizo hili. Kilimo cha pamba kinaendesha maisha ya Wananchi zaidi ya milioni 14 wa Mkoa wa Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na Mikoa mingine. Tatizo kubwa la wakulima wa

pamba limekuwa ni bei ya mazao yao, lakini kubwa zaidi ni hasara wanazozipata baada ya bei kuwa imeporomoka na inakuwa inaporomoka kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitegemea na tulizungumza mwaka juzi, baada ya bei ya pamba kushuka kutoka bei tarajiwa ya shilingi 1100 kwa kilo ikaenda hadi shilingi 600. Tulitegemea yangefanyika mambo mawili makubwa kwa zao hili. Kwanza, tulitegemea katika bajeti hii kungekuja mpango wa kuwa na mfuko kwa ajili ya kufanya uhimili wa bei. Tunaita price stabilization fund. Ni suala ambalo Wataalam wa Kilimo wanalijua, Waziri analijua na Serikali inajua, lakini hakuna Mfuko huo. Kwa maana hiyo, mwaka huu pia kwa sababu hatujui bei itakuwaje, ikija kuporomoka watakula hasara nyingine tena.

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuhimili au kwa kutokuweka mipango ambayo itaweza kusaidia kuhimili kwa bei ya pamba, kwa vyovyote vile lazima Wananchi wataendelea kuteseka. Jibu lingine ambalo lingeweza kupatikana kutokana na tatizo la pamba ni kutafuta soko la uhakika na soko la uhakika ni kuweka viwanda. Mwaka jana tuliondoa tozo mbalimbali kwenye mazao ya kilimo na kwenye viwanda au kwenye ku-process mafuta ili kuongeza angalau bei. Kwa upande wa Serikali nini kimefanyika? Viwanda vya nguo ambavyo ndiyo vingeweza kuchakata pamba havijafanyiwa chochote. Viwanda vingi vimebinafsishwa na vingine vimetelekezwa. Katika mazingira hayo ambayo hatuweki mipango ya kuhakikisha tunakuwa na uhakika wa bei ya wakulima wetu tena wakulima wa pamba, sikubaliani na kwa hakika sidhani kama Wananchi wa Shinyanga pia nao wanaweza wakakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili nikubaliane na bajeti hii, kwa upande wa pamba ninategemea mambo matatu: La kwanza, nategemea nione fedha zimetengwa kwa ajili ya price stabilization fund; la pili, nategemea nione mkakati wa kutosha na uhakika kwa ajili ya kufufua angalau viwanda vya kuchakata pamba; na la mwisho ninategemea kuona mipango madhubuti ya kutangaza na kusaidia wakulima wa

pamba ili kuongeza tija kwenye kilimo cha pamba. Sasa hivi productivity ni ndogo na kwa maana hiyo wanalima kwa gharama kubwa, wanapata kidogo na mwisho wa yote wanakuja kuuza kwa bei ambayo ni chini ya matarajio waliyokuwa nayo wakati wanalima. Kwa upande wa pamba, kama haya hayatakuwepo au majibu kwenye maeneo yao hayatakuwepo, hakika hatutakubaliana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la chakula cha njaa. Mmetufanya tumekuwa watu wa kutulisha, tupeni sasa chakula. Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Shinyanga, tulitegemea kupata angalau tani 3,500 za mahindi. Tulizoletewa kwenye hesabu zilizokubalika kwenye Wizara ni tani 1,821 na hizi tani zilitakiwa ziletwe kati ya mwezi Oktoba na Desemba. Hizi tani zimeletwa 1,000 na zimeletwa mwezi Februari. Tunawaambia Watanzania kwamba, hakuna mtu atakayekufa kwa njaa, unampelekea chakula mwezi Februari kwa njaa ya mwezi wa Oktoba. Kwa hakika hatuna mipango ya kuendana na hiyo kauli ambayo ni matumaini tunawapa Wananchi lakini utekelezaji wake unakuwa haupo.

Kwa hiyo, tunaomba sana, kuna tani 700 zimebaki ambazo hazijapelekwa, tunategemea zingepelekwa mwezi wa kumi. Chakula hicho ambacho bado kilitakiwa kiwe kimepelekwa hakijapelekwa. Kwa hiyo, kitendo cha kucheleweshа kuleta chakula huku tukijua watu wale wana njaa na tuliwaahidi kwamba tutawaletea chakula watakapopata njaa, ni kuwaweka katika mazingira ambayo wanaishi kwa kudra za Mungu. Mimi kama Mbunge wao, kwa sasa tunajua hali ya chakula tuliyonayo, nimetoka juzi Kata ya Chela, wamelima mazao hawajavuna hata kitu. Chakula walichokitegemea wangevuna wakati wanalima mwezi wa kumi hakijafika mpaka sasa na hiki walichopata, hizi tani 1,000 zimeenda kwenye robo ya vijiji tulivyotarajia. Katika mazingira kama hayo, watu hawa tuseme tu kwamba, mtaishi kwa matumaini kwa nguvu za Mungu, kwa nguvu za Roho Mtakatifu, lakini si kwa mipango ya Serikali ya kuhakikisha kwamba hamfi kwa njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuzingatia muda

nilionao, naomba niseme kwa uhakika kabisa kwamba, katika mazingira haya, bajeti hii sikubaliani nayo na ninaamini Wananchi wa Shinyanga hawatakubaliana nayo. Kwa hiyo, naomba kutamka kwamba sitakubaliana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi. Ninaomba uniruhusu nianze na nukuu ya Profesa Issa Shivji anasema: "Ardhi kwa Wananchi wa kawaida hasa wanavijiji ni kielelezo cha uhai wao, kielelezo cha utamaduni wao, kielelezo cha ubinadamu wao pamoja na tegemeo lao la kuishi maisha ya kujitegemea na heshima." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, sitaki kuamini kwamba, Watanzania hawawezi kujitosheleza kujilimia chakula mpaka wapate msaada wa Wajomba kutoka Ulaya kuja kutulimia chakula. Ninaamini kabisa kuwa, Watanzania kama Serikali itakuwa na nia na utashi wa kuwasaidia, wakulima wetu wadogowadogo ambao wamekuwa wakililisha Taifa hili kwa miaka 50 iliyopita, wakitumia nyenzo duni na mbegu za asili wameweza kuzalisha chakula na kulifanya Taifa hili lisiwe ombaomba katika chakula isipokuwa katika vipindi vile ambavyo tulipata ukame.

Ninaamini kama kuna nia ya kweli na utashi wa kuwasaidia wakulima wetu wadogowadogo kuwapatia nyenzo za kisasa zilizo bora na pembejeo kwa wakati, nina uhakika kabisa kuwa, watazalisha chakula cha kutosha na ziada. Serikali yetu mara kadhaa hata kupitia Wizara hii ya Kilimo, imekuwa ikielezea uwepo wa ardhi kubwa katika nchi hii. Dhana ya kuwepo kwa ardhi kubwa ni ya kufikirika, hatuwezi kuwa na uhakika wa ardhi tuliyonayo na matumizi yake kama hatujaipima ardhi yenyewe, ni watu wanafikiria kuwa ardhi ipo lakini ardhi hiyo inamilikiwa na vijiji na ile ambayo mnaiona haitumiki, wanavijiji hawa wanaitumia kama maeneo ya malisho ya mifugo yao, hakuna ardhi ambayo haitumiki.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwatolee mfano mdogo tu, ninayo document hapa ambayo iliwasilishwa kwenye

tathmini ya uwekezaji katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika iliyowasilishwa na Dkt. Abunuwasi Mwami wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama kielelezo cha kuifanya Serikali itafakari kwa kina, nikitolea mfano wa Wilaya ya Mpanda. Wilaya ya Mpanda ina eneo la ardhi la square metre 47,527, ambayo ni sawa na hekta milioni nne laki sana na elfu hamsini na mbili na mia saba, lakini ardhi hii ambayo inatumika kwa ajili ya kilimo na ufugaji pamoja na kuishi wanadamu ni asilimia 19. Asilimia 18 ni mapori ya wanyama, (game reserves), asilimia 19 ni akiba ya misitu na asilimia nne ni maeneo ambayo yana maji.

Kwa maana hiyo, Wilaya ya Mpanda mwaka 1967 ilikuwa na wakazi 51,200 ambao walikuwa wanaishi katika eneo hilohilo ambalo ni chini ya hekta 100,000. Leo katika sensa ya mwaka 2002, Wakazi wa Mpanda walikuwa laki nne na elfu kumi katika eneo hilo hilo dogo ambalo Serikali inafikiri kwamba lipo eneo kubwa. Leo idadi ya watu imeongezeka mara dufu na inakaribia laki sita, maana yake ni nini? Ni kwamba, watu wanatafakari kuwa kule Mpanda wakiona yale mapori wanadhani tuna ardhi, mapori haya yanamilikiwa na Serikali. Serikali sasa ioneshe utayari wa kupunguza Hifadhi zake ili ziendeleze kilimo kama wanahitaji maendeleo ya kilimo.

Mbaya zaidi, ardhi hiyo hiyo, wakulima hawa na Wananchi hawa wa Mpanda, wanaendelea kupokonywa ardhi yao na kuongeza Hifadhi za *Wildlife Management Areas (WMA).* Inapokonya ardhi ya vijiji, kwa maana hiyo watu wanapunguziwa maeneo ya kilimo, idadi ya watu inaongezeka kwa kasi na hakuna uwiano. Ili tuweze kufanya mipango madhubuti juu ya hili ni lazima Serikali sasa ipime ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pembejeo; kama Kambi ya Upinzani ilivyokuwa imeeleza, bado ninaungana nayo mkono, ni kwamba, Wizara na Serikali kwa ujumla imekuwa ikifanya kazi ya kubahatisha, yaani *try and error.* Mpaka hivi sasa hawajaja na mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa pembejeo kwa utaratibu wowote ule

zitawafikia wakulima wetu kwa wakati mwafaka na kwa kiasi kinachohitajika. Hatuwezi kusema kuwa tunawasaidia wakulima. Nitoe mfano, Kijiji ambacho kina Kaya 1,000 wanapelekewa kilo 350 za mbegu, kwa maana ni Kaya 35 katika Kaya 1,000 ambazo watapata mbegu bora. Tuna nia madhubuti ya kusaidia wakulima wetu, kama hatuwezi kuwafikishia pembejeo kwa wakati bado tutakuwa na tatizo kubwa katika eneo hili la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Kilimo cha Umwagiliaji na nisikitike, sitaunga mkono Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri mpaka nipate maelezo juu ya *Kikese Irrigation Scheme.* Nimepitia kitabu chako, nimeona umeainisha *Irrigation Scheme* ya Ugala na hakuna taarifa zozote kuhusu Kakese Irrigation Scheme, ambayo iko katika Jimbo langu. Fedha iliyotumwa katika msimu uliopita ni milioni 187,500,000 zimekuwa zikionekanika kwenye mtandao hazijafika katika Halmashauri yetu na Mradi ule umeendelea kusimama.

Kulikuwa na soko la tumbaku, bila kuzungumzia tumbaku nitakuwa sijawatendea haki Wananchi wa Mpanda. Mpanda inazalisha tumbaku, ni moja ya eneo ambalo linazalisha tumbaku kwa wingi hapa nchini. Nilikuwa ninataka kuishauri Serikali, pamoja na jitihada zilizofanywa kuhusu zao hili la tumbaku, soko kubwa limepatikana China, makampuni yanayonunua tumbaku nchini ni ya Kimarekani, soko lao liko Ulaya. Sasa Serikali hii isikae ikangojea hawa Wamarekani waje kununua tumbaku ya wakulima wetu, waende wakauze China. Ni sisi wenyewe kupitia Serikali yetu, kupitia Vyama vyetu vya Ushirika na kupitia wakulima wetu, tuanze kutengeneza mpango madhubuti wa kulipata soko la China kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika wa tumbaku tulivyonavyo.

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na kiwanda cha kusindika tumbaku, tusifanye makosa kama tuliyofanya mara ya kwanza, wakaenda kujenga kiwanda Morogoro. Kiwanda cha kusindika tumbaku kijengwe Tabora, baada ya kujenga kwa ubia na wale ambao tutaenda kuwauzia hususan masoko haya ya China, nina uhakika kabisa kuwa

tutawasaidia wakulima wetu na watakuwa wamepata bei nzuri katika kuuza tumbaku yao.

Nimalizie na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Moja ya nia thabiti ya Serikali ilikuwa ni kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nianze kwa kusema kuwa, uongozi ni changamoto na kuongoza nchi siyo jambo jepesi. Kwa maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba kusema kuwa, nimetumwa na Wananchi wa Sikonge na haya yaliyoko mbele yangu hapa na mbele yao ni changamoto. Kazi yangu ya kwanza ni kuona yale muhimu ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekwishayafanya na kuyaunga mkono, lakini zile changamoto ambazo zipo ni kuendelea kuziboresha.

Ninaomba nitofautiane kabisa na wenzangu waliotangulia, mimi ninaomba niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

Kilimo ndiyo tegemeo kubwa la Wananchi, karibia asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, kwa hiyo, kwa namna yoyote ile Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiweza kuwawezesha Wananchi wanaoishi katika maeneo ya vijijini na wale wa mijini katika suala zima la kilimo, utakuwa umekomboa kwa kiasi kikubwa sana Wananchi katika suala zima la kuondokana na umaskini. Mimi nina uhakika kabisa kuwa, haya maelezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameyasema kuwa bajeti ya Serikali hii ni ndogo katika kilimo na kuwa hatujaamua kwa kiasi kikubwa kuwekeza katika kilimo, hii ni hoja ya msingi na ni lazima Waheshimiwa Wabunge wote tuiunge mkono.

Mheshimiwa Spika, kule Maputo kulifanyika Azimio la kuelekeza kuwa, nchi zote ambazo zinaishi katika Ukanda huu wa *SADC* zihakikishe kuwa, tunafikia angalau kuwekeza bajeti karibia asilimia kumi kwa mapato ya ndani ya Serikali. Naiomba Serikali kwa sababu nilikuwa ninaangalia uwekezaji

wa Serikali kwenye bajeti, kwa maana ya fedha zinazotengwa kwenye Bajeti ya Serikali toka mwaka 2008/ 2009, 2010/2011, 2012/2013 na mwaka wa 2013/2014, hatujawahi kufikia asilimia nane. Kwa hiyo, tuko nyuma katika Azimio hili, ninaiomba sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ione umuhimu wa kuwekeza kwa kiwango hiki ambacho tuliazimia ili tuweze kufikia malengo ya kuleta mapinduzi katika kilimo.

Jambo lingine muhimu sana ni suala la matumizi kwa maana ya pembejeo na mbolea. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inakuwa na gharama kubwa sana ambazo inazitoa kwa ajili ya usambaji wa pembejeo; kwa mfano, kuna huu utaratibu wa kusambaza mbolea hizi zinazoitwa mbolea za ruzuku, lakini kama tungekuwa na viwanda vyetu humu nchini, nina hakika kabisa kuwa, kungekuwa na gharama ndogo na wakulima wangeweza kupata pembejeo hizi kwa gharama nafuu. Sasa niiombe Serikali na kwa bahati nzuri tumeshapata phosphate, tumeshapata gesi asilia na hizi ni sehemu ya pembejeo ambazo zinaweza kusaidia katika kuanzisha viwanda na baadaye kuanza kuzalisha mbolea humu nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, siyo vizuri Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kujiondoa katika kila kitu, tuliamua muda mrefu sana kuwa viwanda vya mbolea nchini ni muhimu, tunaendelea kusubiri wawekezaji siku hadi siku; wawekezaji wasipokuja kuwekeza katika suala la mbolea Wananchi wetu wataendelea kubaki katika hali hii mpaka lini? Nilikuwa ninaomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ione umuhimu wa kuanza kuwekeza aidha yenyewe au ubia na vyombo vingine ambavyo vinaweza kusaidia katika kuendeleza jitihada za kuondoa tatizo la mbolea kwa wakulima wetu hapa nchini.

Wenzangu wamezungumza suala la mazao makuu ya biashara, ni kweli ukiangalia mazao yetu Makuu mengi sana yameanza kwenda chini niiombe sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Yako mambo ambayo Serikali yenyewe inaweza kusaidia kuboresha; kwa mfano, wakulima

wengi wa biashara wanategemea Sekta ya Ushirika katika kuendelea kusimamia, lakini ushirika wetu katika maeneo mengi ukiangalia ushirika wa zamani, Ushirika wa *SHIRECU,* Ushirika wa NYANZA, Ushirika wa *KNCU* ulivyokuwa na nguvu, ushirika wa leo hii sasa umekuwa na matatizo makubwa ya ubadhirifu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, nimefurahi sana kusikia kuwa, kutakuwa na hoja hapa, tutakuwa na Muswada mpya hapa wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushirika. Mimi ninaomba sana Sheria ile ya Ushirika tutoe meno kwa wabadhirifu wote, wanaowanyonya wakulima, wanaowaibia wanaushirika, Sheria iwe na meno ya kuwashughulikia na kuwachukulia hatua kali sana wale wanaopatikana na hatia hizi. Mazao yetu ya biashara kama korosho, tumbaku, kahawa, chai, pareto na mkonge, yana changamoto ambazo ziko tofauti; kule Kusini yako malalamiko makubwa sana juu ya mfumo huu wa stakabadhi ghalani. Ni vizuri Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwa sikivu sasa na kuweza kusikiliza kilo hiki cha Wananchi wa Mikoa hiyo ya Kusini na kuona kuna tatizo gani huko na kufuatilia ili kuona kama tunaweza kurekebisha kwa maslahi ya wakulima wetu wa korosho.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wakulima wa tumbaku, mimi ninataka kusema kuwa, katika kipindi hiki yako mambo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri kubaini maeneo ambayo yana ubadhirifu hasa maeneo ya Sekta ya Ushirika. Hatua zinaendelea kuchukuliwa na katika jambo hili kwa kweli ninaomba niipongeze sana Serikali, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla na Mkuu wa Mkoa wa Tabora - Mama Fatma Mwasa, kwa jinsi alivyoshughulikia suala hili kikamilifu. Mimi nina hakika, tutafika mahali Wananchi wetu, wakulima wetu, wataendelea kupata haki yao vizuri zaidi na niipongeze sana Serikali katika jambo hili muhimu kwa kupatikana kwa soko hili la wakulima wa tumbaku kwa maana ya soko la China.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie; ili ulete ukombozi wa kweli nchini, ni vizuri ukawekeza kwa wale watu

ambao wanafanya kazi za kila siku mijini na vijijini. Ukiwekeza kwenye kilimo kwa vijana, ukawekeza kwenye kilimo kwa wanawake, utakuwa umeleta ukombozi mkubwa sana. Serikali lazima ijielekeze katika makundi haya kuhakikisha akina mama na vijana wanapewa mitaji, wanawezeshwa zana za kuleta mabadiliko katika kilimo na mambo haya yanawezekana. Nipongeze sana katika maeneo mbalimbali katika Mikoa mbalimbali, jambo hili limeanza. Nipongeze katika Mkoa wa Tabora kule Igunga, vijana wamejiunga wanakwenda vizuri na Mheshimiwa Rais amekuja pale amewapa msaada mkubwa. Sikonge tumeanzisha jambo hili muhimu, vijana karibu 70 wako kambini wanaendelea na kazi hii muhimu ya kujiajiri.

Tukiendeleza jambo hili, vijana wakatoka wakapata ufundi, wakapata ujuzi wa kilimo, watarudi na watafanya kazi nzuri za kuendelea kujiajiri. Ninaomba nirudie kuunga mkono hoja na ninaomba niseme kwamba, changamoto zilizopo sisi kama Viongozi ni lazima tukabiliane nazo katika kuwasaidia Wananchi ambao tunawahudumia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza, ninataka niikumbushe Serikali ya kwamba, bila ukaguzi imara au bila kuimarisha kada ya ukaguzi wa Vyama Vya Ushirika, jitihada zetu zote tunazozifanya juu ya kufufua au kuimarisha ushirika hazitazaa Ushirika wenye matumaini na kwa hiyo, hatutapata Ushirika endelevu.

Ninapenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ya kwamba, tulishaanzisha mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ningeomba mchakato huu uharakishwe ili kupitia Tume hiyo basi, Kada ya Ukaguzi wa Vyama Vya Ushirika iimarishwe kuondoa mwanya wa wizi na ubadhirifu katika Vyama Vya Ushirika, ambao unafanywa bila woga kutokana na kukosekana kwa ukaguzi wa mara kwa mara kwa Vyama vya Ushirika.

La pili, niongelee Zao la Zabibu. Mkoa wetu wa Dodoma hatuna zao la kudumu la biashara, lakini ninaishukuru sana Serikali ilituanzishia Mradi Chinangali wa Zao la Zabibu kwa kilimo cha umwagiliaji wa matone. Kilimo kile kinakwenda vizuri isipokuwa tatizo lililopo ni soko la zabibu zinazozalishwa pale. Nilishamwandikia Mheshimiwa Waziri kumweleza tatizo hili kwa kirefu na hivi sasa yule mnunuzi mmoja wa Kiwanda cha *CENTAWICO* kutoka Hombolo anatumia nafasi yake ya ukiritimba kutoa masharti anayoyataka, kutoa bei ndogo na wakulima sasa wameshaanza kuonesha dalili za kukata tamaa na sisi tusingependa tufike huko, ningeomba sana Serikali iingilie kati kuhakikisha kuwa angalau tunapata uhakika wa kuuza Zao la Zabibu kwa sababu ndiyo zao pekee la biashara la uhakika hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumeomba pengine ingekuwa ni vizuri Serikali iwasaidie wakulima kuanzisha kiwanda cha kusindika zabibu ili ziweze kuuzwa zikiwa katika hali ya usindikwaji, kwa kuuza juisi badala ya kuuza yale matunda ambayo yanaharibika haraka. Ninadhani tukifanya hivyo, tutakuwa tumewanusuru wakulima ambao wanalitegemea sana zao hili. Kinyume cha hivyo, ninaogopa kusema kuwa Mradi wetu ule mkubwa muda siyo mrefu, unaweza kuwa katika mashaka makubwa sana.

Nijielekeze katika suala la kilimo Mkoani Dodoma. Mkoa wetu wa Dodoma ni kati ya Mikoa kame na kilimo cha kutegemea mvua katika Mikoa kame kama huu wa Dodoma ni cha kubahatisha sana. Mimi nilitegemea kuwa Serikali ijielekeze na kuweka mkazo mkubwa sana katika kilimo cha umwagiliaji katika maeneo haya ambayo ni kame na kipindi fulani Wizara ilitangaza kuwa inakusudia kuanzisha Tume ya Umwagiliaji miaka miwili iliyopita. Nimepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, sijaona maelezo yanayoeleza namna ambavyo mchakato huo unaendelea. Pengine mchakato huo ungeharakishwa, ungeweza kutusaidia sisi wakulima katika sehemu kame, kuhakikisha kuwa tunapata kilimo cha umwagiliaji kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua ambacho ni cha kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, lakini niharakishe tu kusema kuwa, katika eneo hilo la umwagiliaji, ziko skimu za zamani ambazo zilikuwa zimeanzishwa miaka ya nyuma na baadhi yake bado zina miundombinu ambayo ni imara.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijitahidi kufufua skimu hizo na hapa nataka nilete ombi mahususi kuangalia skimu ya Bwawa la Ikoa pale Chalinze, ambapo hivi sasa kwa kutumia fedha za Maendeleo za Wilaya, tumeshaanza kufufua ile mifereji. Nilikuwa nafikiria kwamba, ni vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kutoa fedha za kutosha kuweza kulifufua lile Bwawa la Ikoa ili kuwe na uhakika wa umwagiliaji mwaka mzima, ambapo itakuwa sasa ni ukombozi wa wakulima wetu katika eneo la Ikoa na Chalinze na wakulima wote wa Mkoa wa Dodoma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa chakula ambalo wenzangu wamelizungumzia, linatukabili sisi pia katika maeneo yetu mbalimbali. Kwenye Jimbo langu la Chilonwa kuna Kata kadhaa zikiwemo Kata ya Msamalo, Ikoa, Manchali, Bugiri, Msanga na Majereko, tumepata upungufu wa chakula kutokana na ukame ulioyakumba maeneo haya kwa miaka miwili mfululizo. Naishukuru Serikali kwamba, katika hatua za mwanzo imeshaanza kutoa chakula japokuwa ni kidogo, lakini nihimize kwamba, tatizo bado ni kubwa, kwa hiyo, Wananchi bado wanahitaji msaada ule. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuendelea kutoa chakula cha msaada katika maeneo yale ili tuweze kuondokana na tatizo hili la njaa ambalo linawakabili Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, katika Mkoa wetu wa Dodoma, tunayo mabonde ambayo ni mengi. Moja ya mabonde hayo ni lile nililosema la Ikoa, lakini liko Bonde la Mto Farkwa ambalo linatusaidia kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yetu ya Wilaya za Bahi, pamoja na Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Chemba, kwa upande wa Kondoa. Bwawa lile likiimarishwa vizuri na Waziri analijua sana, nadhani litakuwa ni ukombozi mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba, Wananchi wetu wanaondokana na

tatizo la njaa inayotukabili kutokana na ukame unaotupata wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusisitiza suala la ushirika, wenzangu wameshaeleza kwamba kuna ubadhirifu mwingi katika Vyama vya Ushirika, lakini tatizo moja ambalo ninaliona, ukiacha lile la ukaguzi ni kutokuwa na elimu ya kutosha kwa wanachama wetu, japokuwa sheria ya sasa inaeleza jinsi ambavyo wanachama wanatakiwa wapate elimu. Vilevile kuna Programu ya Uboreshaji wa Ushirika *(Cooperative Reforms),* lakini naona kwa fedha zilizotengwa katika Kitengo hiki cha Idara ya Ushirika pengine zinaweza zisitosheleze sana katika kusimamia shughuli zote hizi ambazo zimetengwa katika kutekeleza shughuli za ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa nisisitize kwamba, haya niliyoyasema Serikali ikiyatilia maanani itakuwa imetusaidia sana sisi Wakulima wa Mkoa wa Dodoma; na ili yaweze kutekelezwa haya, mimi sina sababu ya kukataa bajeti ya Waziri, ninaiunga mkono ili haya yote niliyoyasema yaweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, ninakushukuru sana, naomba haya yote niliyoyasema yaweze kuzingatiwa. *(Makofi)*

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Kabaka, naomba urudi unakotoka.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Hotuba ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa mara nyingine tena kwa kuja na mkakati wa kuona kilimo tutakiendeleza vipi hapa nchini. Nasema hivyo kwa sababu kama kuna kada ambayo Watanzania tulitakiwa tuwe

wataalam zaidi na tuwe na mchango mkubwa katika *International System* ni kilimo. Tumekuwa wakulima tangu asili, wakati wenzetu wamejaliwa na barafu kule hawawezi kulima, sisi tumelima. Katika miaka yote hii, kasi ya kilimo vile tunavyotaka iende pamoja na jitihada nzuri za Serikali, inaonekana haiendi barabara. Hili linanikumbusha Dkt. Kleruu wakati mmoja akajaribu kutofautisha wakulima akasema Tanzania tuna *peasants* hatuna *farmers,* ilibidi atumie maneno ya Kiingereza ili kulionesha hilo, hadi leo bado Tanzania tuna peasants, sasa hili ndiyo suala ambalo inabidi tujiulize. Kwa nini watu ambao tuna ardhi nzuri, tulikuwa na vyanzo vizuri vya maji, hali ya hewa nzuri, tuwe bado tuna peasants mpaka leo?

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita niliongelea suala la vitendea kazi, nikatofautisha kati ya ukulima mwanzo wa kilimo na baada ya kilimo. Nilitegemea suala hilo liwe limeangaliwa katika bajeti ya mwaka huu, lakini ninapoangalia pamoja na kusifu jitihada nzuri za kupata matrekta kutoka India, bado tunaongelea kukopa matrekta kutoka India.

Sasa kilimo ambacho ndiyo msingi wa maendeleo yetu, ikiwa tunajikita tu katika kulima bila ya kuwa na nyenzo za kuwezesha kilimo kifanyike vizuri, sidhani kama tutapiga hatua vizuri. Tutakopa matrekta kutoka India kwa miaka mingapi, baada ya hapo tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, wakati tunafanya hivyo, Wahindi na matrekta yao wanayoyatengeneza wanazidi kujiimarisha katika nyenzo za ukulima, wanazidi kujiimarisha katika kilimo, itafika wakati Wananchi wetu watashindwa kununua matrekta hata ya bei nafuu kwa sababu hata matrekta yaliyonunuliwa sasa hivi yametumika; kuna vifaa ambavyo ni vya bei kubwa sana zaidi ya milioni mbili, kikiharibika inabidi usubiri hicho kifaa, kwa hiyo, msimu wa mvua unapokuja ambao unakuja kwa shida sana sasa hivi, inakuwa huwezi kufanya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda kuwa

viunganishwe na chachu kubwa ya maendeleo yetu kama kilimo ni la muhimu. Viwanda vya mbolea kabla hatujalima, viwanda vya matrekta vya *power tiller* na baada ya kilimo, lakini naona sana tunajikita baada ya kilimo tunaanza ku-process mazao vipi, lakini huku mwanzo hakuna msukumo mkubwa ambao tumeuweka. Ningeomba hilo Wizara iliangalie.

Mheshimiwa Spika, kazi yetu hapa sisi ni kuangalia Wizara imekuja na bajeti gani na tujaribu kuiboresha, ninyi mnajaribu kuondoka kwenye kubadilisha Bunge liwe debating club, yaani unapinga tu kwa sababu unataka kupinga, hapo inabidi tuelezane ni nini cha kufanya na tunaomba Serikali tunaposema hivyo watilie maanani na wafanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye Jimbo ambalo ni Wilaya ya Tanga. Siyo siri, Tanga ilikuwa mhimili wa uchumi wa nchi hii na kilichoifanya iwe mhimili ni ukulima wa minazi, ukulima wa matunda na hasa zaidi ukulima wa mkonge. Tanga ile ambayo ilikuwa imeshikilia uchumi wa nchi hii kwa kuwa na vitu vyote hivyo na kwa kujitolea ardhi yote itumike hivyo, Tanga leo inaonekana kama siyo sehemu ya ukulima. Sijaona chochote ambacho kimesema kuwa zile sehemu ambazo hazikupata matrekta ya kutosha kinawekewa miakakati mingapi na vipi ili iweze kupata matrekta. Wilaya ya Tanga mpaka sasa ina matrekta 21 tu. Matrekta 21 yahudumie kaya za ukulima 15,129, matrekta 21 yalime hekta za wakulima 35,000 haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, Tanga ina power tiller kumi tu pamoja na kuwa Wilaya nyingine zina power tiller mpaka 50. Sasa mtalimaje hivyo, hakuna hata wazo la kuweka mabwawa Tanga pamoja na kuwa mvua sasa hivi zimekuwa adimu. Hakuna ruzuku, si ya mbolea, si ya nini kule, ni jambo geni kabisa hakujatolewa ruzuku hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, sasa naangalia mahali hapa ambapo palishikilia uchumi wa nchi kwa kilimo leo pamerudi mpaka imekuwa kiasi hicho; tatizo ni nini? Zao la Mkonge

linaongelewa tu humu lakini uhakika hasa linatakiwa lirudi katika hadhi yake ya zamani. Zao la Mnazi ambalo lilikuwa limefanya Tanga kuwa mji wa viwanda vya sabuni na mafuta na vinginevyo, minazi imekufa, jitihada za madhubuti za kuifufua hazionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningesema kama ningelipata fursa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, labda hili la kuwa Tanga ni Jiji nalo lina matatizo yake, kwa sababu hata unapokuja kwenye suala la ardhi sehemu za ukulima ambazo zingeweza kuenziwa kwa ajili hiyo sasa hivi zinapimwa viwanja.

Wananchi wale sehemu zao za kilimo zinakuwa hazipatikani na hata zile ambazo zinawekwa kwa ajili ya kufanya shughuli maalum kama za *EPZ,* unakuta mpaka leo wameacha kulima, lakini hawalipwi wamekaa wanavumilia tu kungoja mwisho utakuwa nini. Labda suala hilo lingefikiriwa tena, warudishiwe maeneo yao waendelee na kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, kubwa ni lile la kutenganisha kama zilivyo sehemu zingine ili ieleweke kabisa Tanga siyo Jiji, Tanga ina Kata kumi za Vijijini ambazo ni za kilimo. Ninapoambiwa Tanga ni Jiji, nadhani ndiyo inaleta athari hii ya kuwa yanapokuja mambo ya kilimo, yanapokuja mambo ya maji vijijini, Tanga inakuwa imewekwa kando. Tutaleta ombi letu Wilaya ya Tanga iwe na Halmashauri mbili; Halmashauri ya Jiji na Halmashauri ya Vijiji na ningeomba tuungwe mkono tutakapofanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kitu kimoja ambacho kimetajwa mara nyingi hata katika hotuba ya leo; ubadhirifu, rushwa, utendaji kazi wa kigoigoi. Kama tunavyosema kilimo ndiyo kipaumbele chetu cha kwanza, kwa sababu ndiyo kilichopo na ndiyo tunaweza kufanya vizuri na rushwa nayo ndiyo adui yetu wa kwanza nchi hii. Rushwa ndiyo adui wa kwanza na wa pekee itabidi ashughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Nami nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu katika mjadala huu wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kukumbusha tu kwamba, ukijua tatizo au ukijua nini kinakusumbua kinagaubaga, unakuwa tayari umeshapiga hatua katika kutatua jambo hilo. Kwa kuanzia tu, niwakumbushe wenzangu kwamba, kama Taifa tulishajiwekea lengo kwamba tunataka kuondoka katika kundi la nchi ambazo zina uchumi wa chini *(the low income countries)* kwenda kwenye kundi la nchi ambazo zina uchumi wa kati (the middle income countries) kadiri ya vigezo vya Benki vya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa vigezo vinavyotumika na Benki ya Dunia ni Pato la Taifa *(GDP per Capita)* ambayo kwa sasa ili ufike kwenye the lower middle income country, ule upande wa chini wa middle income country unatakiwa uwe angalau una Dola za Kimarekani 1,025. Kama Tanzania mpaka sasa tupo si mbali sana ya nusu ya kile kiwango ambacho ni cha chini kabisa, kwa hiyo, kusudio letu la kufika kwenye middle income country bado liko mbali sana. Sasa inavyochangia kwenye pato pamoja na mengine yote, kwa sababu ya muda nitasema tu kitu kimoja ambacho ni kilimo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 25 wa Taarifa ya Benki Kuu ya mwaka huu 2011/12, inaonesha kwamba, korosho iko nyuma tu ya tumbaku. Tukiacha tumbaku, miongoni mwa mazao makuu ya biashara, korosho ni sambamba na bidhaa za samaki na samaki wenyewe. Hii nilikuwa naisema ili nioneshe umuhimu wa zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa korosho zinatakiwa kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye Pato la Taifa, yapo maeneo ambayo nitayasema leo hii na nitajikita kwenye korosho tu peke yake, kwa sababu ya muda mchache, lakini pia kwa sababu ya umuhimu wa zao hilo, siyo tu kwa uchumi wa Taifa lakini pia kwa uchumi wa Wanatunduru kule ambako wamenituma nikaingia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Zao la Korosho licha ya umuhimu wake katika Taifa, lina changamoto kubwa lakini ambazo kwa bahati nzuri nimeona kabisa Waziri akiwa anaeleza hapa kama hayo yangefanyiwa kazi, tungeweza kuondoka hapo tulipo.

Nataka kuiasa Serikali kwamba, yale yote yaliyoidhinishwa ambayo nitayapitia moja baada ya linguine, yafanyiwe kazi ili tuweze kuondokana na hali tuliyonayo sasa ya mazao ya biashara kwa ujumla wake hususan korosho, kwa sababu ndiyo nalipa kipaumbele kwa leo yafanyiwe kazi ili tuweze kuondoka hapa tulipo na tuweze kupiga hatua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Zao la Korosho, moja linalosumbua kubwa ni masoko. Katika suala la masoko, nataka niseme dhana ya masoko hiki kitu kinaitwa Soko la Dunia inatakiwa kweli elimu ifanyike tupambanue, tuelezane vizuri zaidi. Kuna mchezo unatumika kusingizia tuna changamoto kwenye Soko la Dunia ilihali kuna watu wanafanya michezo ambayo inasababisha mazao haya yauzwe kiujanja ujanja katika bei zisizofaa.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kupata soko vizuri unatakiwa uwe umefanya utafiti. Naona kwamba, Wizara yenyewe pamoja na Bodi ya Korosho, pamoja na chombo kile kinachotakiwa kuendeleza zao la korosho *(CDTF),* bado hawajafanya kazi yao sawasawa. Hapa panatakiwa kufanyika kazi ili tuweze kuboresha bei ya korosho ghafi kwanza kama zilivyo, wakati tukiwa tunafanya kazi ya kufanya utafiti wa viwanda ili tuweze kuongeza thamani, tuweze kupata bei nzuri katika korosho ambazo zitakuwa si ghafi, zile zilizokwishabanguliwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la pembejeo, ambalo ningetakiwa kuanza nalo kwa sababu hapo ndipo

mahali ambapo unazalisha korosho. Kwenye pembejeo tuna matatizo makubwa ya wakulima kupelekewa pembejeo zisizofaa, kupelekewa pembejeo zikiwa zimechelewa na kupelekewa pembejeo zikiwa na bei kubwa kupita hata ule uhalisia.

Ningekuwa na muda wa kutosha ningeweza kutoa takwimu kwa sababu ninazo. Niseme tu kwamba, kuna haja ya kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo kwa bei, kwa ubora wa pembejeo na upatikanaji kwa wakati ni eneo ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi na Wizara ya Kilimo au na Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni lile la utendaji wa chombo hiki muhimu kabisa cha ushirika. Kuna sarakasi nyingi sana kwenye ushirika. Nafurahi kwamba, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna hatua inazungumziwa ya kupitia upya Sheria ya Ushirika, lakini kama alivyosema mzungumzaji mwingine aliyetangulia, hayo ni maneno mazuri sana, lakini sasa tunataka kuona kwa vitendo hilo likitokea. Kweli Sheria ya ushirika inatakiwa ipitiwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mfupi, wakati tukiwa tunasubiri mapitio ya sheria, kwa sababu huo ni mchakato mrefu sana, zichukuliwe hatua haraka hivi sasa za kupitia upya mahesabu ya ushirika, kukagua ushirika, kupitia watendaji wa shirika wote, kuangalia sifa zao, ili tuweze kuchukua hatua za haraka katika kuboresha eneo hili la ushirika.

Natoa rai yangu kwamba, kati ya sasa na msimu ujao wa korosho, wala si muda mrefu ni muda mfupi sana, naishauri Serikali yaliyotokea Tunduru, yaliyotokea mahali pengine popote ambapo korosho ni zao muhimu kama ilivyo kwa Tunduru, yasirudie tena mwaka huu. Msimu ujao wa korosho, tunataka kuona korosho za wakulima zinanunuliwa kwa bei ya Soko la Dunia kweli siyo ile ya ujanja ujanja ya uchakachuaji wa watu wa kati.

Mheshimiwa Spika, pili; katika msimu ujao tunataka kuona wakulima wakiuza korosho zao wapewe pesa zao taslimu. Tunataka kuona pia wakulima hawakopwi tena na Vyama vya Ushirika au na mtu mwingine yeyote yule.

Kukopa Wakulima ni kuwadhulumu. Licha ya kukopa, lakini pia hata katika pesa wanayopewa wanakatwa makato mengi sana ambayo hata hayaelezeki.

Naomba Serikali katika msimu ujao, makato yasiyokuwa na maelezo ya msingi kwa wakulima yasiwepo. Naomba uwazi katika utekelezaji wa haya, maana tunafika mahali wakulima hawana hata mtu wa kumwuliza; si Bodi ya Korosho, si Vyama vya Ushirika na wala si Wizara yenyewe inayojitokeza mbele ya wakulima na kuwapa maelezo juu ya yaliyojiri katika masuala ya masoko ya mazao yao, makato yao, pamoja na mambo mengine yasiyofaa katika mtiririko mzima.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na suala la stakabadhi ghalani. Mimi naamini kama Serikali inasema kwamba, mpango wa stakabadhi ghalani unafaa na ni mzuri, rai hiyo inatakiwa iwashirikishe wakulima pia, ikiwa Serikali inasema ni mpango mzuri lakini wakulima wanasema si mpango mzuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nitaunga mkono hoja baada ya ufafanuzi wa maelezo haya.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli yetu kwa kipindi hiki cha jioni lakini kabla sijamruhusu Katibu atupe Mwongozo, ninasimama hapa kuwashukuru sana kwa imani mliyokuwanayo kwangu na kunirudisha tena kuwa Mwenyekiti wa Bunge, nikimsaidia Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, katika shughuli hizi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, naomba niwashukuru sana. Namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie lakini awasaidie na ninyi Wabunge wenzangu, ili Bunge hili liweze kwenda sambamba na matakwa ya Watanzania na baadaye Watanzania waone kwamba kilichotuleta ndani ya Bunge ni kwa faida ya nchi yetu na kwa faida ya Watanzania wote. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na hoja iliyoko mbele yetu ni Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni hii kwa mujibu wa orodha niliyonayo Mezani, atakuwa Dokta Lucy Nkya na atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi. Sasa naomba nimwite Dokta Lucy Nkya, simuoni, basi nitamwita Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Jerome Bwanausi ajiandae na Mheshimiwa Dokta Hadji Hussein Mponda na yeye ajiandae. Mheshimiwa Susan!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii Wizara ya Kilimo na Chakula, nina masuala kadhaa ya kuchangia ya Kitaifa na hususan Mkoa wa Morogoro na Majimbo ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kilimo, ni suala mtambuka yaani Tanzania ukisema kuhusu kilimo ina maana unawazungumzia Watanzania 80% ambao wanaishi vijijini ndio wanashughulika na kilimo. Hali halisi ni kwamba, Wabunge, tunapotoka hapa tunaenda *Canteen,* yale mazao pale tunayopata afya yanatokana na kilimo. Naomba sasa nipate taarifa tu ya awali ya kichokonozi kwamba, hivi huu mchele tunaokula hapa *Canteen* ambao sasa hivi hauna ladha unatoka wapi? Ndio huo uliotoka Thailand au umetoka wapi? Maana mimi ninashangaa kwetu Kilombero mchale mtamu upo, Mbeya upo, Shinyanga upo, lakini tunapikiwa mchele gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninajenga hoja yangu kuanzia hapa kwa sababu gani? Nchi yetu, Wizara hii na Serikali kwa ujumla, wamefanya kitu kikubwa sana. Mkoa wa Morogoro ni ghala la chakula, kuna Wilaya kabisa zimetambuliwa huko ndiko kutakakotoka chakula na kitazalishwa kwa wingi. Mfano, mmojawapo ni katika Wilaya ya Kilombero, ghala la chakula, lakini ukiliangalia hilo ghala la chakula Serikali, inafanyaje kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye mradi wa kuzalisha mpunga *(KPL),* mradi mkubwa kabisa; mpunga umezalishwa, Serikali imemwambia Mwekezaji afundishe na wale wanaowazunguka wapate elimu ili na wao wazalishe mpunga kwa wingi. Wamefanya hivyo, wakulima wamefundishwa, mpunga umezalishwa mwaka jana, huwezi amini, mpaka hivi ninavyosema, kilio. Kama kuna watu wanalia basi nenda kajifunze Wilaya ya Kilombero, kule Mngeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ile ya Kilombero kule Mngeta, Mwekezaji amezalisha, hata Mwekezaji ukimuuliza leo anashangaa Serikali yetu. Wamezalisha mpunga, wakulima wamezalisha, Serikali bila aibu wameagiza mchele kutoka Thailand wamejaza sokoni. Leo ni kilio, ingawaje pale anacheka, lakini hicho sio kicheko hicho ni kilio Naibu Waziri, hali ya mpunga ni mbaya katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo debe la mpunga, nenda kanunue kule Kilombero, Mngeta, debe la mpunga mpaka 2,000/=. Wale watu wamekopa kwenye Benki za *NMB,* hawajui watalipa vipi hiyo mikopo. Mpaka Benki ya *NMB,* nimeonana na Afisa mmoja pale Kilombero, anasema wakulima tena hawatakopesheka kwa sababu hawana uwezo wa kulipa tena madeni yao kwa sababu, mpunga wanao hawana soko; mnatufanyia nini Serikali ya Tanzania? Kwa nini mnadhalilisha wakulima? Tatizo liko wapi? Mna mkataba gani na watu wanaoleta mchele kutoka nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo langu, ninaitaka Serikali, itoe majibu kwa wakulima wa Kilombero na wa Mikoa mingine inayozalisha mpunga, ni namna gani watawakwamua hawa wakulima katika kununua yale mazao ambayo yamelundikana kwenye maghala, hawajui watauza wapi; mtupe majibu. Huko ni kwenye kilimo cha mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye kilimo cha miwa, kilimo cha miwa, Sheria au Kanuni inasema kwamba, katika mzunguko wa kilometa 40 katika kiwanda cha sukari, wanatakiwa wasianzishe viwanda vidogovidogo. Wakati inatungwa Sheria hiyo na hizo Kanuni wakulima walikuwa wachache sana katika maeneo hayo. Leo wakulima wamekuwa wengi, hiyo Sheria bado inawakataza wakulima kuanzisha viwanda vya sukari, matokeo yake ni nini? Matokeo yake wakulima wanalima miwa, kiwandani wakienda kuuza miwa mingine inakatwa, ikikaa wiki moja Mwekezaji hataki kuinunua anasema imechacha, mkulima amepata hasara, miwa inatupwa, tunamsaidia vipi huyu mkulima? Kiwanda cha Kilombero iko hivyo, mikataba ya ajabuajabu, *K1* na *K2.* Sasa naitaka Serikali, iende ikafanye mambo mapya, ikawasaidie wakulima na wawekezaji, iende ikawasaidie wakulima ni namna gani wataanzisha viwanda vidogovidogo kwa kushirikiana na *SIDO,* ili waanzishe viwanda vya sukari, waweze kusaga miwa yao na wauze sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ahadi za Rais, kule

Mtibwa, leo tunasikia Viongozi wa Kisiasa wanaenda huko wanawadanganya watu, ooh tutashughulikia; ameshindwa Rais na kwenye ahadi yake pale Mtibwa, utaweza wewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali, itoe majibu kwa wafanyakazi wa kiwanda cha Mtibwa, ni namna gani watapata stahili zao. Ni namna gani watapata stahili na haki zao na kwenye viwanda vyote vya miwa, Serikali ije na majibu wana mpango gani wa kuwasaidia wakulima wadogowadogo na wafanyakazi katika viwanda vya sukari. Hali ni mbaya, watu wanahangaika, hawajui cha kufanya. Naomba mje na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hilo halitoshi, twende katika masuala ya ushirika. Leo tunasema ushirika-ushirika; ushirika wa zamani uko wapi? Serikali, naomba mlete majibu. Waliokuwa wanachama wa ushirika Mkoa wa Morogoro ambapo Serikali mlisema mnachukua mali, mkiziuza mtawarudishia, mtawalipa stahili zao. Tangu mwaka 1984 kuna wanaushirika takribani 200 hawajui watapata wapi stahili zao. Naomba Serikali ije na majibu, wawaambie wananchi wa Morogoro wasiopungua 200 waliokuwa wanaushirika Mkoa wa Morogoro, watalipwa lini stahili zao? Nataka majibu ya Serikali ya kwelikweli, msiruke hizo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya katika masuala ya pembejeo. Pembejeo imekuwa kizungumkuti, hali ni mbaya kuliko matokeo. Leo mkulima anaandaa shamba mwezi wa 11, pembejeo inakuja mwezi Januari; hii pembejeo mnamplekea nani? Mje na utaratibu, lini pembejeo zitawafikia wakulima? Hebu someni mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kilombero kulikuwa na miradi nya umwagiliaji. Kuna mradi uko Zinginali, naomba Serikali ije na majibu;

umetumia karibu shilingi milioni mia tatu na *point,* lakini mpaka leo ule mradi ni kizungumkuti, hauendi mbele wala haurudi nyuma, umesimama. Mradi wa Njagi, unazidi kutengewa hela, lakini ule mradi kuna watu wawili wamefanya kazi kwenye ule mradi na yote iko kwenye kiwango cha chini. Nataka nipate majibu ya Serikali, kwa nini miradi ya umwagiliaji haileti tija katika Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kibaya zaidi watumishi wa Kilimo Wilaya ya Kilombero, hawajatengewa hela za ufuatiliaji. Hivi mnategemea nini kama Wagani, hamuwatengei hela za ufuatiliaji? Mnategemea ni kilimo gani kitaenda kule kwa wananchi wa kawaida? Nataka majibu ya Serikali na je, bajeti ya mwaka huu inasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukichukulia suala la kuboresha kilimo pamoja na miundombinu, katika tarafa ya Mngeta yenye Kata tano, hakuna umeme. Mnaongea vipi na watu hawa wa umeme? Watu wanashindwa kukoboa mipunga yao, wanashindwa kuweka mashine za kukoboa na kusaga. Barabara mmesema mtatengeneza kilometa 103, kutoka wapi mpaka wapi? Naomba ufafanuzi kutoka Serikalini kuhusu miundombinu Wilaya ya Kilombero. Maana ninavyojua, barabara kuanzia Kidatu, ambapo ni mbaya, mpaka Mngeta kwenye uwekezaji mkubwa hazipungui kilometa karibuni 160, lakini leo, mmesema mtatengeneza 103, zitaishia wapi? Kuanzia wapi mpaka wapi mpaka tufike katika eneo la uwekezaji? Sasa ni vema Serikali ikaja na majibu na wananchi wakajijua wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi bado wana kilio kikubwa. Chonde ninaomba na naitaka Serikali, ilete majibu ya kina, ili wananchi waelewe wanakwenda wapi. Haiwezekani Serikali, muwahujumu wakulima. Mmewahamasisha walime, wamelima, halafu ninyi mnaingiza mchele sokoni wao wanakosa soko, haiwezekani, ni lazima tupate majibu hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Susan Kiwanga kwa mchango wako. Tunaendelea na mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Jerome Bwanausi sijamwona ndani ya ukumbi wa Bunge, nitampa nafasi Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani na Mheshimiwa Jitu Soni wajiandae.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kuwa wazi, naunga mkono bajeti ya Wizara hii kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, ukisoma hotuba ya Waziri, katika utangulizi wake ameeleza na wengi tunafahamu kwamba sekta hii ya kilimo ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya Watanzania, inachukua 75% ya shughuli ambazo wanajishughulisha Watanzania na 95% ya chakula tunachokula, kinatokana na sekta hii ya kilimo. Sasa wale ambao, nawashauri, wanafikia hatua kwamba hawakubaliani na bajeti hii tuwaulize, wanaitakia mema nchi hii, si wanatuletea janga la chakula hao? Maana msipopitisha hela hii, hii sekta haitaweza kuendelezwa kwa msimu wa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hotuba ya Waziri, ukurasa wa 65 - 72, wameeleza namna gani vilevile nje ya jitihada ya Serikali, lakini wanahusisha na sekta binafsi ambayo, Mbunge aliyepita, ameelezea yanayofanyika. Tayari Serikali imeshaanza kufanya hivyo na hata bajeti hii

wataendelea zaidi kushirikisha sekta binafsi kuboresha kilimo chetu; kwa mfano ile *SAGCOT.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna programu ya vijana katika kilimo. Je, vijana hawa wanaomaliza shule, ajira zinakuwa ni ngumu, Serikali wamefikiria namna gani ya kuweza kuwasaidia vijana hawa. Kwa hiyo, hii bajeti ninavyoiona kabisa inatoa majibu ya ajira na majibu ya uhaba wa chakula katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze sasa kujikita katika mchango wangu, nitaulekeza katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni Kanuni za Kilimo Bora. Sehemu ya pili, kilimo cha umwagiliaji. Sehemu ya tatu, soko la uhakika la mazao ya shambani na sehemu ya nne ni utafiti wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada na mikakati ambayo Serikali tunaishukuru inafanya, lakini bado wanatakiwa waongeze zaidi. Kilimo chetu bado ni duni miongoni mwa wakulima wadogowadogo, bado wengi mpaka leo hawajui Kanuni bora za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna changamoto, elimu na uwezeshaji wa kufikisha huduma hizo. Kwa mfano, matumizi ya mbegu bora; wakulima wangu, nikiwemo na mimi mwenyewe Ulanga kule, bado kilimo chetu cha mpunga tunabahatisha mbegu bora. Tunabahatisha vimbegu hivi ndio matokeo yake wastani wa mapato inafikia gunia nane mpaka magunia 10 kwa hekta moja, ambapo kama tungeletewa mbegu bora za *Salo Five,* zingeweza kuzalisha mpaka magunia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna tatizo la mbolea na pembejeo na niliiomba Serikali katika swali langu moja ambalo nimeiuliza Wizara hii kwamba, basi hii mbegu bora waiingize katika ruzuku ya pembejeo. Naiomba Serikali, katika bajeti hii nayo waangalie vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji ndio itakuwa mkombozi katika kilimo chetu. Wengi

wamezungumza na mimi ninaomba nisisitize zaidi, hasa nikirejea kwa sehemu ambayo ninaijua vizuri sana na hiyo sehemu kama tutaiwezesha, Bonde la Mto Kilombero ambalo lina Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Kilombero, tutaweza kutatua kwa kiasi kikubwa sana tatizo la chakula nchi hii ambao ni mchele na sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ulanga, wana hekta ambazo zimekaa kiumwagiliaji, hekta 30,000, lakini mpaka leo haifiki hata hekta 1,000. Maoni na maombi yangu kwa Serikali, tafadhali hebu elekezeni nguvu za uwekezaji katika maeneo yale kwa sababu yako maeneo 12 ambayo yakiwezeshwa yanaweza yakaleta tija kubwa sana, lakini mpaka leo ni *scheme* tatu tu ndio zimewezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la uhakika la mazao yetu, kilio cha wengi na wengi tunashuhudia. Sio mpunga tu, ukienda korosho, ukienda tumbaku, ukienda pamba, kila zao ni tatizo la soko. Mimi nilivyoliona ni kwamba, lingine linalochangia ni mfumo huru wa soko, bado haliwasaidii wakulima sanasana linawasaidia hawa wachuuzi wa katikati. Sasa tuangalie ni namna gani tutatengeneza utaratibu wa kuweza kumsaidia mkulima huyu badala ya kuliachia tu kuwa soko huria kama walivyosema wajumbe waliopita kwamba hii ukweli haiwezi kuleta tija, haiwezi kutatua tatizo la soko la wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali nafikiri inahitaji kujenga vituo vya kurahisisha biashara hii ya mazao. Kwa mfano, vituo viwe pale mipakani, kama mahitaji yametosha katika nchi hii bado nchi za jirani wanahitaji. Wenzetu wa Kenya, wameshatupiga mabao, wanachukua mchele wetu, wanachukua sukari yetu wanapeleka Darfur. Sasa sisi ni kwa nini tusitengeneze mazingira ya vituo kama hivi mipakani kuwezesha biashara hii iwe rafiki na iwe rahisi zaidi kumsaidia huyu mkulima wa kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha soko, vilevile inatakiwa upatikanaji wa taarifa za masoko. Watu wa Shinyanga, wanalalamika hawana mahindi, lakini watu

wa Songea wanalalamika hawana mahali pa kuuzia hayo mahindi. Sasa hilo ni suala la utaratibu tu Serikali wapatie taarifa hawa wahusika wakulima, wapi kuna soko, wao wenyewe wataleta jitihada mpaka kufikisha huko kwenye masoko. Kwa hiyo, hakuna kila siku tunatoa kilio cha njaa wakati sehemu nyingine wana vyakula vya ziada mpaka vinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa nimalizie maelezo yangu, mchango wangu, kuhusu utafiti wa kilimo. Hela zilizotengwa ni kidogo sana tena chini ya 1% zimetengwa katika bajeti nzima ya Serikali, kwa ajili ya utafiti pamoja na kilimo. Hela hizi jamani ni kidogo sana, suala la utafiti ni muhimu sana ndio linatoa majibu na takwimu za kisayansi ambazo zinaweza zikatusaidia sisi watunga Sera, zitawasaidia na watendaji namna gani ya kutatua matatizo ambayo yanawakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, suala la zao mpunga; kuna kilio kwa wakulima wa mpunga, kuna ugonjwa unaoitwa *rice yellow mottling virus desease,* kule nyumbani wakulima wa mpunga wanaojua tunaita kimyanga. Hili suala sasa hivi lina mwaka wa 10 hakuna jibu. Mimi nawashauri Serikali, wenzetu wa China wameshafanya tafiti kama hizo katika mazingira ya Kiafrika na wametoa majibu. Serikali, hebu muwasiliane na hawa Watafiti wa Kichina na mnaweza vilevile yale majibu mkayatumia yakaweza kutatua tatizo hili. Huu ugonjwa unawaathiri sana wakulima wa mpunga ni kwamba, mmea wa mpunga unakuwa rangi ya njano, unadumaa na unaathiri sana uzalishaji kwa mkulima wa kawaida na mkulima wa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watafiti, wanafanya utafiti mwingi lakini unaishia tu kwenye majarida, kwenye *publication* tu, wanapata *PhD,* wanapata na vitu vingine. Je, ni lini sasa mtawawezeshe watafiti hawa watoe taarifa hizi kwa wale wahusika zaidi? Watoe taarifa hizi kwa wakulima kwa njia rafiki zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda. Waheshimiwa Wabunge, nilisema mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Titus Kamani lakini simwoni ndani ya ukumbi wa Bunge, basi naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Jitu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nishukuru kwa kupata nafasi hii. Mimi kwanza ningependa kuishauri Serikali kwamba yale yote ambayo Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo imeshauri izingatie ushauri huo kwa sababu tumefanya kwa niaba ya Wabunge wote na kwa niaba ya Watanzania wote wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarudia mengi yale ambayo tayari Kamati imeshashauri lakini muhimu kuliko yote Serikali iangalie namna ya mtiririko wa ile fedha ambayo inatolewa hasa fedha ya maendeleo. Kama mwaka jana inaonyesha kwamba imetolewa asilimia 19 tu na katika ile asilimia 19 ni asilimia 49 ndiyo imetumika kwa ajili ya Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo ni vizuri sisi kama Wabunge wote tujikite tuangalie namna ya kubadilisha ile Sheria ya Manunuzi. Ile Sheria ya Manunuzi ndiyo inaua nchi hii, ndiyo inamaliza uchumi wetu, ni vizuri tukiangalia upya na tuiboreshe ili tuweze kuendelea na Taifa letu liweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa tofauti kidogo na baadhi ya wachangiaji, mimi nasema kwamba sisi kazi yetu ni kuishauri Serikali na kuisimamia. Wote tukiwa walalamikaji bila kutoa ushauri kwamba tufanye nini majibu yatapatikana? Tunapochangia basi tuikosoe Serikali lakini pia tuiambie kwamba tunategemea wafanye nini ili Serikali iweze kurekebisha na tuweze kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kilimo Kwanza, mimi nilikuwa nashauri kwamba moja katika nguzo ni ardhi lakini katika Wizara ambazo zipo katika *lead ministries,* zile Wizara

mstari wa mbele katika kilimo Wizara ya Ardhi haimo. Ningeomba safari hii mtuhakikishie na leo wakati wa kutoa majibu au kesho mtuambie kwamba Wizara ya Ardhi pia sasa mmeshaiweka katika moja ya hizo Wizara ambayo itakuwa mstari wa mbele kwa sababu bila ardhi hakuna kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningeshauri Serikali wakati wa kuandaa miradi mbalimbali, wa kuibua na wakati wanakaa na kuweka mipangilio Wizara zote husika zingeshirikishwa. Leo malalamiko yote haya ambayo yanatokea hapa ni kutokana na kutokuwa na ushirikiano baina ya idara moja na nyingine au Wizara moja na nyingine na utafiti mbalimbali ambao umefanywa pia unaonyesha kwamba Wizara hazishirikiani na ndiyo maana unakuta miradi mingi inakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba kuishauri Serikali kwamba iangalie upya mambo ya tozo na kodi mbalimbali ambazo zipo katika sekta ya kilimo ni mzigo kwa mkulima. Wanasema kwamba hizo tozo na kodi mbalimbali zinatakiwa kulipwa na wafanyabiashara lakini si kweli mbebaji wa mwisho wa mzigo huo ni mkulima. Kwa mfano, hata hizi kodi ambazo tumeshaondoa mwaka jana kwenye *Finance Bill* kwa mfano matela ya trekta, matairi , vipuli vya matrekta, hiyo yote pamoja na kuondolewa na ni sheria bado zinaendelea kutozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeomba Wabunge wote tushirikiane kipindi cha *Finance Bill* mwaka huu hayo majibu yapatikane na Serikali itoe majibu kwa nini bado inaendelea kutoza. Wakitaka mfano yale yaliyoondolewa hata mwaka huu kwa mfano kwenye matela tunazo risiti ambazo watu wamelipia kodi bila hivyo zilikuwa haziruhusiwi kutoka bandarini lakini pia kodi ya ardhi na kodi nyingine nyingi. Tuiangalie vizuri wakati wa *Finance Bill* wote tuchangie tuhakikishe hizo kodi zote tunaziondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nashauri kwamba Serikali iangalie Sheria ya Manunuzi kama

nilivyosema awali. Bila kubadilisha Sheria ya Manunuzi hatutasonga mbele katika idara yoyote ile iwe kilimo, iwe mifugo, iwe katika mambo ya barabara, ni sheria ambayo lazima tuiangalie kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningeshauri Serikali katika mfumo wa vocha, umekuwa na malalamiko mengi. Kabla ya kuanza huo mfumo mpya kama Kamati ilivyoshauri, ningeomba wajipange vizuri na kama ni hili suala la kukopeshwa bila kwanza kuleta Sheria ya *VICOBA* kutambulika kisheria hapa, wananchi wetu wengi wako kwenye vikundi vya *VICOBA* haviko kisheria, je watakopeshekaje? Je, ardhi yote imeshapimwa? Huyo mkulima ataweka nini rehani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri huu mfumo mpya usitumike kwanza, tuendelee na mfumo huu, tuangalie namna ya kuboresha na mjipange vizuri kabla ya kuleta mfumo huo wa kukopesha kwa kupitia mabenki lakini pia hizo taasisi za kifedha na mabenki, je, huko vijijini yapo? Kwa hiyo, utafiti wa kina ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kuishauri Serikali suala la kulinda ardhi ya kilimo, ni muhimu hiyo sheria iletwe mapema na ardhi za kilimo zilindwe kwa sababu leo hii sehemu nyingi unakuta ardhi za kilimo zinageuzwa kuwa maeneo ya makazi, viwanda na zinabadilishwa matumizi. Tusipochunga, itafika mahali ardhi zote zile zenye rutuba itakuwa zimeshaondolewa, zimejengewa makazi na hatutakuwa na maeneo ya kilimo. Mfano mzuri ni pale Babati eneo lote lile la Babati linalozunguka Bonga lilikuwa lizinazalisha mbaazi ambayo inasifika duniani leo hii mashamba yote yamegeuzwa kuwa makazi. Arusha pale, Burka ukiangalia shamba kwa mfano la Gomba *Estate* kule Arusha na maeneo yote yale yamekuwa makazi wakati mji wa Arusha ungeweza kutanuka kuelekea Gisongo au kule Orjoro. Sasa hiyo sheria isipoletwa ninaamini kwamba itafika mahali hatutakuwa na maeneo ya kulima ambayo yana rutuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wakati wa kubinafsisha mashirika ya umma, mashirika mbalimbali, mashamba na pia ranchi iangalie nani wa kuwapa. Kuna watu ambao ni wazalendo wa humuhumu ndani nchini ambapo uwezo wanao, nia wanayo isipokuwa labda hawana ule ufahamu. Wangeboreshwa, wawekwe kwenye vikundi na ndiyo wapewe kipaumbele kupewa hayo mashirika au hayo mashamba na ranchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iweke mazingira rafiki katika uwekezaji katika kilimo, miundombinu mbalimbali kwa mfano barabara, umeme, maji katika maeneo ya vijijini. Watu wengi leo wanahamia mijini kwa sababu maendeleo hakuna vijijini, hivi vitu kule vijijini ni tatizo. Mkipeleka mahitaji muhimu vijijini, watu wataendelea kubaki kule na wataendelea kuwekeza katika sekta hizo na mazingira rafiki yataendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la Mfuko wa Pembejeo. Mimi ningeshauri Serikali, ni mfuko ambao umesaidia wakulima wengi sana, ungeendelea kuboreshwa. Kuanzia umeanzishwa mpaka leo umepewa shilingi bilioni 22 tu, ni vizuri Serikali ingeangalia namna ya kuuongezea mfuko huo fedha lakini pia uwezo wa *TIB* na Benki ya Kilimo ije mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upande wa Chuo Kikuu chetu cha *SUA*. Ni vizuri Serikali iangalie namna ya kuboresha Chuo hicho kwa sababu pesa ya maendeleo pia inakuja kwa mtiririko ambao siyo sahihi lakini vifaa vingi hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu ni suala la mazingira. Ni vizuri Wizara zote zikae pamoja ili suala la tabianchi na masuala ya mazingira yaweze kuboreshwa. Pia upande wa utafiti, ni vizuri Serikali ijikite kuongeza fedha katika vituo vyetu vya utafiti. Aidha, ruzuku zinazotolewa kwa ajili ya mbegu na mbolea, kwanza zipewe makampuni wanayozalisha hapahapa nchini badala ya kutoa hiyo ruzuku kwa makampuni ambayo yanaagiza kutoka nje. Ruzuku ibaki

nchini inufaishe Watanzania na vituo vyetu vya utafiti kwa vile ndivyo kwa sehemu kubwa vinazalisha hizo mbegu. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali izingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali iangalie namna pia kuwezesha Halmashauri zetu kuwa na uwezo wa kukopa. Mahali ambapo Serikali kwa ajili ya bajeti ndogo iweze kuiruhusu Halmashauri pia ikope iweze kuendeleza miradi mbalimbali badala ya kusubiri tu ruzuku na mapato kutoka Serikali Kuu. Halmashauri zetu pia zikope mahali wao wanaona wanakipaumbele ambapo hawajapewa pesa na Serikali Kuu pia waweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi unaosema ukimpa mtu samaki unamlisha kwa siku moja, mfundishe namna ya kuvua ili aweze kujilisha kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima anahitaji kupewa mikopo, awezeshwe ili aweze kujilisha yeye mwenyewe lakini aweze kulisha Taifa hili. Hahitaji kila siku kupewa misaada na wanasema kwamba *no farmer, no food, no life,* bila mkulima hakuna chakula, hakuna maisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Jitu, sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Kaihula.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa kilimo ni kitu kikubwa sana. Wananchi wote wanategemea kilimo, wakulima wote wanategemea kilimo na hasa wale ambao hawakai vijijini wanategemea kilimo. Asilimia 80 ya wanachi wote wanakaa vijijini na hawa wote wanategemea kilimo. Hata wale ambao wanakaa mjini wanategemea kilimo. Kwa hiyo, kilimo ni kitu kikubwa, hakuna uhai, hakuna kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa

Programu ya Maendeleo ya Kilimo (*DADPS).* Mpango huu ni mzuri sana, wananchi wengi wamenufaika kwa mpango huo wa *DADPS* hasa kwa upande wa umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo moja ni kuwa bado kuna hela nyingi huko kwenye Halmashauri zetu ambazo bado hazijatumika. Ni kwa nini? Tatizo ni kuwa hatuna wataalamu wa kutosha hasa wa umwagiliaji na hasa ma-*engineers* na *surveyors.* Kitu kingine ni mtiririko wa fedha kulingana na maombi ya mradi, fedha zinakuja kidogo kiasi kwamba huwezi kufanya kitu kufuatana na huo mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa upande wa Wizara na Serikali yangu, naomba sana iangalie kwa upande wa wataalamu, kuna Chuo cha Kilimo - SUA pamoja na Chuo cha Umwagiliaji – Mbegani, wanatoa wataalamu wa umwagiliaji tuweze kuomba kibali na waweze kutoa wataalam wengi kusudi waweze kusambazwa huko vijijini na kusimamia hii miradi ya *DADPS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni Programu ya Kuendeleza Shughuli za Kilimo Vijijini yaani shughuli za *SAGCOT***.** Sasa hivi *SAGCOT* imeshaanza tayari katika Mkoa wa Pwani pamoja na Mkoa wa Morogoro. *SAGCOT* imejikita kwenye mazao ya mpunga na miwa. Ninachowasihi wakulima hasa wakulima wadogo wadogo wa Morogoro ambao wananisikia pamoja na Mikoa mingine ambayo haijaanza, wajitayarishe kwenye mpango huu wa *SAGCOT* ambao utaweza kuwanufaisha kwa kuinua kipato chao pamoja na lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye bajeti, kila mmoja anajua anategemea kilimo, hata humu Wabunge wanategemea kilimo, hakuna mtu ambaye halimi hata tuta la mchicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Kilimo mpaka sasa hivi ni ndogo, kwa hiyo kwa miaka inayokuja, bajeti zinazokuja tuweze kuona kuwa tunaongeza fedha kwenye

bajeti hii ya Kilimo angalau iweze kufikia 10% ili iweze kutekeleza mipango yake kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Wabunge wote hapa wanalalamika sana kwa sababu ya chakula. Siyo kusema hawataki kulima kwa sababu ya tabia ya nchi, Mikoa mingi imekumbwa na ukame lakini kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi. Kwa hiyo, naiomba na nashauri Serikali yetu na Wizara tuweze kuona jinsi ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji hasa kwenye Mikoa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Mkoa wangu wa Morogoro, Mkoa wa Morogoro unaweza ukalisha nchi nzima kwa sababu una mito mingi, tatizo ni wataalam wa umwagiliaji na wagani. Tukipata wataalam wa umwagiliaji, naamini tunaweza kumwagilia na kulisha wananchi wengi. Kama tunavyofahamu, wakulima wengi ni wanawake, wakipewa zana za kilimo na wataalam, wanawake wa Morogoro ni wachapakazi, naamini wataendeleza vizuri kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Rais kwa msukumo wanaouweka kwenye upande wa kilimo na hasa kwa upande wa zana za kilimo. Wamesukuma suala la matrekta kiasi kwamba tumeweza kupata matrekta na wananchi wameweza kuyanunua. Kilimo cha jembe kila mmoja kila mtu anajua ni matatizo. Ombi langu kwa Serikali yangu, naomba ile sehemu ya pili ya matrekta ambapo mpango unapangwa ufanyiwe kazi haraka ili kusudi matrekta hayo yaweze kununuliwa na wananchi waweze kusambaziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu, naomba sana kupitia Wizara na Serikali, waiangalie Wakala wa Uzalishaji wa Mbegu kusudi waweze kupewa nyenzo hasa fedha za kutosha waweze kuzalisha mbegu za kutosha. Aidha, wanachi wanaowazunguka na wenyewe waweze kuwekwa kwenye mpango huo waweze kuzalisha mbegu. Mpaka sasa hivi tunatumia mbegu za nje. Hakuna sababu ya kutumia

mbegu za nje kama wananchi tunaweza kuzalisha mbegu za ndani. Serikali yangu naiomba mipango yote iwekwe kuweza kuzalisha mbegu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wakala wa Udhibiti wa Mbegu ambao ipo Morogoro, inafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, tukiwahimiza wananchi kulima mbegu, wanaweza tukazalisha mbegu tukapata mbegu za kutosha kuliko kupata mbegu za nje. Naomba niwahakikishie kuwa mbegu za nje nyingine zinakuja na magonjwa, tukiweza kutumia mbegu za kwetu tunaweza tukazalisha mazao ambayo hayana ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti, Chuo cha *SUA* pamoja na vyuo vingine, naomba waweze kupewa fedha za kutosha kusudi waweze kufanya utafiti. Taifa haliwezi kuendelea kama hakuna utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha matunda na mboga. Watu wengi sasa hivi wanakula *apples* lakini *apples* hizi zinatoka *South Africa.* Hakuna sababu ya kuendelea kula *apples* za *South Africa* kutokana na kilimo cha matunda na mboga, pamoja na utafiti uliokwishafanyika, ningeshauri tuzalishe *apples* zetu za kutosha. Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Tanga na Mikoa mingine inayozalisha matunda iweze kufaidi kwa kuzalisha matunda haya tusiweze kupata matunda ya kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachi wengine wanakunywa juisi za kutoka nje, hakuna sababu ya kunywa juisi ya kutoka nje ambayo hujui ubora wake. Tuhimize kula vitu vya humu nchini kusudi tuweze kuona afya zetu zinakwendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa upande wa kuthaminisha matunda, viwanda vingi vimeharibika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninarudia kusema, naunga mkono hoja asilimia 100.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Dkt. Ishengoma. Waheshimiwa Wabunge, ninaona hapa Kambi ya Upinzani bado wanaendelea kufanya *consultation,* kwa hiyo, nitamwacha Mheshimiwa Naomi Kaihula kwanza mpaka watakapoweza kuwa wamemaliza, kama anasimama ina maana wameshakubaliana kwa sababu una dakika tano tu za kuchangia kwa mujibu wa taarifa niliyonayo Mezani, huna dakika kumi una dakika tano tu. Kwa hiyo, kama una dakika tano na ziko sawasawa basi ukichangia ina maana mtu mwingine tena badala yako hataweza kuchangia. Kwa hiyo, kama ndivyo hivyo unaendelea basi nikupe nafasi uendelee na atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu ajiandae.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi napenda kuzungumzia masuala kama mawili, matatu kwa msisitizo kwa dakika tano, naomba Serikali iyazingatie sana masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kuhusu chakula, sielewi kwa nini mpaka leo tunakaa tunalia chakula, chakula wakati kusema ukweli Siasa ni Kilimo mwaka 1972 ilikuwa imetoa jibu la vitu kama hivi, kulikuwa na mashamba ya Taifa ya Chakula kwa mfano NAFCO, BASUTO na mengineyo. Haya mashamba yalikuwa yanaweza kuzalisha chakula vizuri pia yalikuwa yana-*save* kama mashamba darasa kwa watu wanaowazunguka. Kule kwetu Mbozi wale watu waliokuwa wanazunguka mashamba yale walikuwa wanaweza kujifunza mambo mengi, kilimo cha mahindi na kwa kweli chakula kilikuwa hakipunguki lakini kwa kitu kisichoeleweka kilekile ambacho Serikali yetu inafanya haya mashamba yamekufa na wala hayaonekani yako wapi. Kwa hiyo, naitaka Serikali ihakikishe haya mashamba inayafufua na iyawezeshe yafanye kazi badala ya kuwaleta wawekezaji kulima vyakula

ambavyo havina tija na mara nyingi vinakuwa kwa faida ya wale wanaokuja kuwekeza hapa, naomba tusiwe Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuzungumzia suala la *SAGCOT*, lakini katika *SAGCOT* naomba kuzungumzia zaidi wale mawakala wao wanaowatumia Monsanto. Sasa Monsanto tumekuwa tukizungumzia toka zamani, *actually* nikiwa mwanaharakati, tulikwishaeleweshwa madhara ya mbegu ambazo zinatolewa na hawa watu wa Monsanto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaomba, sisi kama Taifa, tunaolipenda Taifa letu ni lazima tuwe na *intelligence* yetu ya kilimo na uchumi. Kwa sababu, hapa wanaletwa watu ambao wanafanya nchi yetu iwategemee wao badala ya sisi kujitegemea. Hawa wanazalisha mbegu ambazo baada ya muda zinakufa na siyo hilo tu, pia hizo mbegu zina hasara sana kwa sababu zinaenea mahala pengi pakubwa. Kwa hiyo, ukisema zikianza kwa mfano Mbeya, zinaendelea kote, Mbozi wapi na Mikoa mingine, kwa hiyo tulikuwa tunaomba waweke hiyo *intelligence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoimba Serikali yetu hii, iwe inatenda mambo badala ya kuzungumza. Hawa watu wa *SAGCOT* wawekewe *intelligence* inayowafuatailia na tunaomba wakulima wetu watayarishwe wajue njinsi ya kuweka mbegu zao za asili ili kama zile za kwao zikifeli, zile zinazotokana na Monsanto; basi waweze kurudi kwenye mbegu zao za asili. Wenzetu kama walivyotueleza, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, India walikwishaachana nao watu hawa, walifanya utafiti na wakaona hawa jamaa wanafanya tu kusudi wao waendelee kuwa tegemezi wa kwenda kununua mbegu huko, msione hata kama ni nchi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ninalotaka kuzungumzia, ni suala la ubunifu. Sisi tunaweza kuwa na chakula pia kwa kufanya biashara, lakini biashara tukipata, pia tunakuja kununua chakula. Sasa mimi sielewi kwa nini vitu kama uzalishaji wa dawa lishe, vitu kama Alovera, vitu

kama michaichai, vitu hivyo siku hizi vinazalishwa pia, vinaweza vikawa faida...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa muda wako umepita. Sasanitamwita Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba Serikali izingatie masuala hayo mawili, matatu. *(Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kuchangia kwa huu muda wa dakika tano. Nitakwenda moja kwa moja kuzungumzia ushirika. Ushirika mimi nasema ni jambo zuri, uliundwa ili uweze kusaidia wakulima. Ushirika uliundwa ili kuweza kuhakikisha kwamba, kupitia kilimo wakulima wanapata bei nzuri, wakulima wanaweza kuendeleza maisha yao na wanaweza kusomesha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwamba, Serikali kwa kweli imedhoofisha ushirika kwa sababu ukitazama Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003, kuna Maafisa Ushirika, kuna Mrajisi wa Vyama, lakini kusema kweli, vyama vikuu vya ushirika vimekuwa ni kama machimbo kwa viongozi wanaoongoza ushirika huo. Kuna ubadhirifu mkubwa, kuna kuiba fedha za wakulima, kuna malalamiko mbalimbali ya wakulima ambayo yanatokana na ushirika kuongozwa vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa mfano kwa ushirika wa KCU, kule kwetu Mkoa wa Kagera. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana, kuhusu ubadhirifu na utendaji mbaya wa chama hicho. Malalamiko hayo, yako mbele ya meza ya Waziri wa Kilimo, lakini mpaka sasa hivi

hakuna kitu ambacho tumeshapata sisi katika Mkoa wetu, kuona kwamba Serikali inanyanyuka kuweza kusaidia au kufanya utafiti juu ya malalamiko hayo. Mambo haya siyo kwa Mkoa wetu tu na vyama vingine vya ushirika vinakufa, wakati Serikali inakaa na hata malalamiko yanapokuja haichukui hatua haraka. Sijui mnataka tusemeje, mpaka tuwalime makonzi vichwani ndiyo muamke ili kusudi muweze kusaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwaangalie Maafisa Ushirika. Hawa Maafisa Ushirika hawana hata ofisi nzuri za kufanyia kazi, hawana nyenzo, matokeo Mameneja Wakuu wa Vyama vya Ushirika ndiyo wanaowapangia kazi, ndiyo wanaowapa posho, mnachotegemea ni nini? Mnategemea kwamba hawa wanaweza kufanya kazi nzuri wakati hawana hata nyenzo za kufanyia kazi? Matokeo yake, wanazika na kuhakikisha kwamba hata malalamiko ambayo yanatokana na wakulima hawayafanyi kazi. Mimi naiomba Serikali iwangalie hawa Maafisa Ushirika. Nina uhakika kupitia hii sheria ambayo mnaileta sasa bila shaka itakuwa nzuri na itaiwezesha Serikali kuweza kuweka mkono wake, japokuwa Ushirika ni mali ya wakulima lakini Serikali ihakikishe, kwa sababu zile pesa ni za Watanzania, basi mhakikishe hata nyie mnasaidia kuhakikisha kwamba vyama hivi vinasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashauri Serikali itoe elimu ya ushirika kwa umma. Kwa sababu mpaka sasa hivi kizazi hiki kipya, hakielewi hata ushirika ni nini, hawaelewei haki zao za kimsingi katika ushirika. Unaweza kukuta hata wale wajumbe wa Mkutano Mkuu ambao wanawakilisha wenzao katika mikutano ya kutoa maamuzi, hawaelewi kinachoendelea, hawawezi kusomi mizani, hawawezi kufanya chochote. Kwa hiyo, wale Mameneja wanawatumia kutokana na kutoelewa mambo yao kuweza hata kupitisha mambo mbalimbali, kwa ku-*stamp* tu ili mradi wanapewa kitu kidogo wakati mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda

niongelee ukaguzi wa ushirika. Hata katika kitabu hiki wametuambia kwamba, ushirika unakaguliwa na vyombo mbalimbali lakini ninachotaka kusema, ni kwamba ukaguzi unaofanyika na wenyewe siyo sawasawa. Unaweza kukuta wale Wakaguzi na wenyewe wanapigwa kitu kidogo, basi wanafunika mambo mengine. Ninaomba sasa, ifike mahali hata *CAG* na yeye aweze kusaidia hata kukagua mahesabu hasa ya Vyama vya Ushirika Vikuu. Kwa sababu hesabu zinazotolewa zinakuja na mambo ambayo hayaeleweki, lakini Serikali bado haichukui hatua za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niongelee kuhusu Maafisa Ugani. Kama alivyotuambia katika kitabu chake, ni kweli mnataka kuajiri hawa watu. Hata mwaka jana mlitueleza hapa kwamba mnataka kuajiri Maafisa Ugani Tanzania lakini bado kuna vijana wengi ambao wamemaliza vyuo katika *grade* mbalimbali, Cheti, Stashahada, Shahada wako mitaani wamelalia taaluma hii wakati hawa watu wanahitajika sana ili kuweza kusaidia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele imelia?

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Conchesta. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na orodha yetu na kama tutakuwa na nafasi za kuchangia, tutazingatia majina ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba na majina yao yako kwenye orodha ya Meza ya Spika, kwa maana ya uwiano uleule ambao tumekubaliana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, naona Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu hayupo, basi nitampa nafasi sasa Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. AMINA A. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kudaiwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, tangu tupate Uhuru wa Taifa hili mpaka leo, kila mwaka bajeti ya Kilimo haizidi asilima nane (8% ) ya bajeti yote ya Serikali. Tanzania ni mwananchama wa *SADC* na walikaa Maputo na wakasaini Azimio la kiwango cha angalau asilimia kumi (10%) ya bajeti ya kilimo, katika bajeti nzima ya serikali lakini mpaka leo nadhani bajeti hii tunayo-*discuss* sasa hivi ni asilimia saba. Niombe Serikali kama kweli ina nia ya dhati kabisa ya kuwa na kilimo cha kisasa, ni lazima wazingatie hili, ni lazima bajeti iongezeke angalau ifikie hiyo asilimia kumi. Ningeomba sana kwa sababu tunaweza tukapiga kelele, lakini watendaji wakashindwa kutekeleza yale ambayo tunayaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikitike kidogo kwa sababu kilimo chetu kwa kweli ni duni, kwa muda mrefu sana kimekuwa hakina misingi thabiti. Kwa sababu Tanzania Mungu ametupenda, tuna ardhi kubwa na ina rutuba, tuna mito, tuna mabwawa makubwa kabisa, hakuna sababu yoyote ya kutolima chakula cha kutosha lakini inasikitisha sana mpaka leo bado tuko ombaomba. Ukiangalia maeneo mengine bado yanapewa chakula cha msaada, hii inasikitisha sana zaidi ya miaka hamsini ya uhuru sasa hivi mpaka leo bado tuko ombaomba. Hii ni dhahiri kuwa nchi yetu bado haijakuwa na sera. Imekosa sera ambayo ni muafaka kwa ajili ya kukuza kilimo na kuinua hali za maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata baadhi ya viongozi ambao wako katika Serikali hii, ambao ni wajasiri wanakiri kuwa hatujapiga hatua ya maana katika kubadilisha kilimo chetu. Mfano, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, ambaye wakati huo alikuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda

na Biashara Zanzibar, miaka minne nyuma iliyopita. Aliwahi kusema wakati anafungua warsha moja huko Zanzibar, naomba kumnukuu Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ruhusa yako.

*"Hivyo ni muhimu tukijiuliza kwa nini mapinduzi ya kilimo yanachukua muda mrefu kufikiwa Tanzania? Kitu gani hatujafanya sawa? Je, mfumo wetu wa kitaasisi unaunga mkono ukuaji wa kilimo? Je, wadau wanaelewa sawasawa matatizo ya msingi katika sekta ya kilimo nchini?". (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu maswali yake yalikuwa ni ya msingi kabisa, yalikuwa ni mazuri lakini sina uhakika kama mpaka leo hii yameweza kupata majibu, kwa sababu, ukiangalia sera zinabadilika siku hadi siku. Tulikuwa na Kilimo cha Kujitegemea, Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona na leo tuko kwenye Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niipongeze Serikali, wanajitahidi sana kwenye mipango yao mikakati kwa sababu kuna makabrasha kwa makabrasha ya mipango. Ukisoma katika kabrasha la Kilimo Kwanza, kwa kweli utashawishika kabisa, kusema na kuamini kuwa sasa tumepata muarobaini wa kilimo cha mapinduzi ya kijani lakini katika utekelezaji bado unasuasua, tatizo kubwa ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijawatendea haki ndugu zangu wa Tanga kama nitakuwa sikuiongelea Tanga. Mheshimiwa Waziri alipokuja hapa, alisema katika hotuba yake, ardhi ni rasilimali ya kwanza katika kilimo, ni kweli namuunga mkono asilimia 100%, kwa sababu tatizo kubwa tulilonalo Tanga, ni uhaba wa ardhi uliopo. Tanga *historically* ilikuwa ni *estate*. Kulikuwa na mashamba makubwa ya mkonge na baada ya ubinafsishaji, mengi yamechukuliwa na ndugu zetu wanaitwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Tanga Mjini,

nitatoa mfano, ndugu yangu Mheshimiwa Nundu asubuhi aligusia Tanga Mjini. Tanga ni Jiji lakini lina Vijiji ambavyo viko ndani ya Jiji. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na maeneo ya kilimo lakini hawana ardhi ya kutosha ya kuweza kulima, ni tatizo sugu, maeneo yale ni ya wawekezaji. Pia ukiangalia Wilaya ya Pangani, Mwera, Kimang'a, Kigombe na maeneo mengine, wanakabiliwa na tatizo hilohilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi karibuni alipofanya ziara yake Tanga, katika kufungua barabara ya Horohoro - Kisera pale katika Wilaya ya Mkinga, Mheshimiwa Rais katika *speech* yake aliligusia hili na aliahidi kuwa atashughulikia. Ningemwomba Mheshimiwa Rais kwa kweli ashughulikie suala hili na aharakishe kulishughulikia kwani wananchi wale wanateseka sana. Kwa sababu huwezi kukaa kijijini, hakuna kiwanda, hakuna kitu chochote, utafanya kazi wapi, ni lazima upate ardhi ili ulime. Ningemwomba Mheshimiwa Rais kwa busara zake suala hili aliharakishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nigusie kwenye suala la mfumo wa kusambaza pembejeo kwa kutumia vocha ambao ndio ulikuwa ni mfumo wa zamani. Sasa hivi Serikali imekuja na mapendekezo ya mfumo mpya wa kusambaza pembejeo kwa mikopo ya muda mfupi na yenye riba nafuu. Suala la kusambaza pembejeo kwa vocha, lilikuwa na changamoto nyingi sana kama alivyosema Waziri. Kwa kweli limeshindikana kwa sababu limewasumbua sana wakulima na ilikuwa ni *issue* kubwa. Pia katika hili suala la kusambaza pembejeo kwa hii mikopo, inaweza ikawa ni nia nzuri ya Serikali lakini kwa kweli kwanza linahitaji muda kwa ajili ya kulifanyia kazi ili kwanza wakulima waelewe suala hili. Je, dhamana itakuwa ni nini? Nina mashaka kama umefanyika utafiti wowote? Je, wakulima walishirikishwa na ushirikishwaji wake ni upi, kutoka chini kwenda juu au kutoka juu kwenda chini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. AMINA A. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina Mwidau, naomba uzime *microphone* yako. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Dunstan Mkapa, atafuatiwa na Mheshimiwa Shaffin A. Sumar.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu, ya Wizara ya Kilimo na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja (100%). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo. Asilima kubwa ya wananchi hapa Tanzania huwa wanashiriki katika kilimo lakini hivi karibuni nadhani mwaka jana, tumeanzisha dhana ya Kilimo Kwanza. Napenda nitoe masikitiko yangu makubwa kwamba Wilayani kwangu Nanyumbu, dhana hii ya Kilimo Kwanza bado haijatekelezwa kikamilifu. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, zana ya kilimo bado ni duni. Wananchi wa Nanyumbu wanatumia majembe ya zamani ya mkono. Wanaumia migongo hata hivyo tija yenyewe inakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, naomba sana Wizara hii ya Kilimo, itusaidie wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu katika sekta hii ya kilimo ili waweze kunufaika na dhana hii ya Kilimo Kwanza. Hatuna matrekta mengi, mbegu

hatupati, tunatumia bado mbegu duni zilezile za kienyeji. Vilevile kwa kweli wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu hawapati pembejeo kwa wakati. Kwa hiyo, hali hii inawafanya wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kuwa maskini, kipato chao ni kidogo, hawana mikopo, hivyo kuwapelekea hawa wananchi wa Nanyumbu kukosa hii dhana nzima ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika Wilayani Nanyumbu bado unasumbua wakulima. Hakuna kabisa ile dhana ya ushirika kwa maana ya ushirika hasa ule tuliouzoea miaka ya nyuma. Maafisa Ushirika wanadidimiza Ushirika badala ya kuendeleza ushirika. Wamekaa sana wengine miaka kumi, kumi na ngapi, sasa wanafanya kazi kwa mazoea. Kwa hiyo, naomba sana kama inabidi basi wahamishwe wapelekwe sehemu nyingine, pengine waje watu wengine waendeleze ushirika unaostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma Serikali ilifanya ushirika wa Mkoa wa Mtwara, ukopesheke kwa kulipa madeni yake, lakini hii leo tunazungumza bado kuna wakulima wa zao la korosho ambao hawajalipwa pesa zao, na Mheshimiwa Waziri mwenye zamana anajua hilo na nasikitika kwamba mpaka sasa wananchi wanalalamikia hii sheria ya stakabadhi ghalani. Sheria ya Stakabadhi Ghalani haiwanufaishi kabisa, ni matatizo makubwa, wanalalamika, watu wanashindwa kupeleka watoto wao shuleni, wanashindwa kupeleka watoto wao Hospital na kwingineko, kwa ajili ya huduma mbalimbali kwa sababu hawajalipwa fedha zao za korosho, hivi ni lini watalipwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao nayo ni tatizo. Kuna mazao mchanganyiko sana yanalimwa Wilayani Nanyumbu kwa mfano, choroko, mbaazi, ufuta, lakini bei anayopewa mkulima ni ndogo sana. Mathalani zao la choroko, mkulima analipwa shilingi 400, 500, imezidi sana 600, lakini ukienda Kariakoo sokoni choroko hiyohiyo iliyotoka Nanyumbu inauzwa 2500 kwa kilo. Hii ni dhuluma kubwa sana. Wizara hii ilituambia kwamba itaunda Bodi ya Mazao

Mchanganyiko, lakini mpaka sasa hivi sijaona faida na matokeo ya Bodi hii. Naomba sana Wizara hii iwasaidie wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu iwaletee angalau kipato kwa kuwaongezea bei za mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji, Wilaya ya Nanyumbu skimu za umwagiliaji hakuna kabisa. Tuna mto mkubwa sana, mto Ruvuma, unapitisha maji mengi kutoka kwako kule Mwenyekiti mpaka Bahari ya Hindi, lakini maji yale yanapita tu hivihivi yanakwenda mpaka huko mto Ruvuma hayafanyi kazi yoyote. Nchi nyingine maji yale yangeweza kutumika kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na za kibinadamu, lakini maji haya yanakwenda tu hivihivi, ni lini tutayatumia hayo maji? Ninaomba sana Wizara hii ilete miradi ya kuweza kuweka skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kwa wakulima wetu, ni fursa za upatikanaji wa dhana bora za kilimo. Nimezungumzia matrekta, lakini vilevile, vijana wetu wangeweza kuwezeshwa wakaanzisha angalau viwanda vidogovidogo kwa ajili ya kubangulia korosho, kwa sababu zile korosho walishakata tamaa sasa hivi, kwamba hazina bei, walionazo bado wanazo mpaka leo majumbazi mwao. Tungepatiwa angalau viwanda vidogovidogo kwa ajili ya vijana, ingeweza kuwasaidia angalau kupata kipato kidogo. Naomba sana tena sana, Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo, watupatie viwanda vidogovidogo kwa ajili ya kuwawezesha vijana waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yamepelekea uwiano wa maendeleo kuwa mdogo katika Wilaya na nchi nzima ya Tanzania. Kuna maeneo mengine maendeleo yamekuja kwa sababu wanawezeshwa kwa kilimo lakini maeneo ya Wilaya ya Nanyumbu niseme Kusini kule, maendeleo yetu ni duni kwa sababu uwezeshwaji nao ni duni. Tukumbuke kwamba Wilaya ya Nanyumbu ilikuwa ni eneo la wapiganaji enzi za ukombozi Kusini mwa Afirika, tuko nyuma kimaendeleo, tusisahauliwe na kilimo ndiyo uti wa mgogo. Naomba sana tena sana Serikali ituone kwa jicho la huruma, watu ni maskini, wanajitahidi kulima lakini kipato

chao ni kidogo kwa sababu ya kutokuwa na uwiano mzuri wa maendeleo kati ya Wilaya ya Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara na sehemu zinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Maafisa Ugani nao ni tatizo linguine Wilayani Nanyumbu, Maafisa Ugani hawapatikani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mkapa, nilisema baada ya Mheshimiwa Mkapa nitamwita Mheshimiwa Shaffin Sumar na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa ajiandae.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hai mpaka leo hii kwa sababu niliugua ghafla jambo ambalo lilipelekea kupelekwa India kwa matibabu. Aidha, niwashukuru Wabunge wenzangu kwa kunifariji na kunipa maneno ya kupona haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuru Serikali kwa kunipa msaada wa haraka na kunipeleka India kwa ajili ya matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru familia yangu kwa kuwa wavumilivu katika kipindi chote ambacho nilikuwa naumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawashukuru wapigakura wangu kwa kuwa na uvumilivu na kuniombea

dua ya kupona haraka. Nawahakikishia kwamba sasa hivi afya yangu ni njema, niko kazini naendelea kupambana na changamoto zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba nijielekeze kwenye hoja na kwa kuanzia, nianze na suala la tumbaku kwa sababu Wilaya ninayotokea, Wilaya ya Uyui, ni ya pili katika uzalishaji wa tumbaku kwenye Mkoa wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kufanya kazi nzuri ya kuvipatia dhamana Vyama vya Msingi, Vyama vya Ushirika ili vijitegemee kiuchumi, lakini bado wapo wachache ambao wamejipanga kabisa kuhujumu Vyama vya Msingi na kuwahujumu wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho huu unajidhihirisha pale ambapo Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Tabora *(WETCU)*, kukaguliwa na baadaye uongozi, Bodi nzima kujiudhuru. Ni jambo ambalo linatushtua sisi kwamba kuna ubadhirifu wa hali ya juu kwenye vyama vya ushirika. Pia nimpongeze Hassan Wakasuvi ambaye kapewa jukumu la kuongoza Bodi hiyo kwa muda mfupi. Tuna matumaini makubwa na Wakasuvi na tunaamini atafanya kazi nzuri lakini bado anahitaji msaada mkubwa sana kutoka Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Bodi kujiudhuru, nataka nipongeze juhudi za Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, mama Fatuma Mwasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wameonyesha ujasiri na wameonyesha kwamba tukiamua tunaweza. Nimwombee Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kwamba Serikali imwongezee ulinzi kwa sababu baada ya zoezi hili amekuwa

na maadui wengi sana kiasi ambacho maisha yake yako hatarini kwa sababu wale ambao walikuwa wamezoea kuchota fedha za wakulima, mianya yao yote sasa imekatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeanza kazi ya kusafisha, naishauri Serikali kwamba isiishie kwenye ngazi ya WETCU tu, iende juu iangalie mfumo mzima wa *APEX*, lakini pia ishuke chini iangalie Maafisa Ushirika jinsi wanavyotenda kazi na jinsi wanavyotuharibia kazi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakulima ambao wanakuwa na tabia ya kutorosha tumbaku, kitu ambacho kinawapelekea wakulima wengine waadilifu kukosa malipo yao. Pale ambapo hawa wakulima wanaotorosha tumbaku wakifikishwa kwenye vyombo vya dola, basi huachiwa kwa vielelezo kwamba hao ni wadaiwa, waendelee kudaiwa. Hili jambo linawavunja moyo sana wakulima ambao wanafanya kazi kwa kujituma. Naishauri Serikali iimarishe Sheria ya Ushirika ili hawa wote wenye tabia ya kutorosha tumbaku waache mara moja na hatua kali dhidi yao iweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubadhirifu mwingine unaofanyika kwenye ushirika, nao wanatumia ujanja wa kusema kwamba tunauza tumbaku kwa fedha za kigeni za dola, lakini wakulima hawapelekewi mahesabu sahihi yaani kwa maana ya *exchange rate* na hapo ndipo wakulima wanapoibiwa. Najua uchunguzi umefanyika na mpaka leo wakulima wanasubiri matokeo ya uchunguzi huo. Nataka Serikali itamke kwamba ni lini matokeo ya uchunguzi huo yataweza kutangazwa lakini pia nataka niseme kwa msisitizo mkubwa sana kwamba kwa kuwa ubadhirifu umebainika kwenye vyama vya msingi na *WETCU* basi katika msimu huu wa kilimo, wakulima wa tumbaku wote wale wanaodaiwa wasikatwe hata shilingi moja mpaka hapo uchunguzi utakapokamilika na kujua kwamba kiasi gani ni halali wakulima kulipa na kiasi gani ni cha kuibiwa. Narudia, wakulima wasikatwe hata shilingi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikathubutu kusema kwamba, katika huu wizi unaoendelea, hata Benki ya *CRDB Branch* ya Tabora, wamehusika kikamilifu katika kuibia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano na ushahidi ninao, katika msimu wa mwaka jana walikuja na mpango wa kuanza kujenga maghala ya tumbaku. Utaratibu waliotumia ni kuwalazimisha wakulima wakubali kujengewa kwa gharama juu, dola elfu 40. Mkandarasi aliyeletwa alikuwa ni ndugu yake na Afisa Masoko wa Benki ya *CRDB, BOQ* alijitengenezea mwenyewe, alijikagau mwenyewe na mbaya zaidi walijilipa wenyewe hata pale ambapo Vyama vya Ushirika vilikuwa havijaidhinisha malipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi, yale maghala yaliyojengwa ambayo yanakuwa na mlango mmoja na ile milango ukiiona imetengenezwa kwa mbao iliyooza, lakini wamewachaji shilingi milioni sita. Huu ni wizi mkubwa, wakulima hawawezi kubebeshwa mzigo kama huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia karatasi ya bei ya tumbaku ya msimu huu mwaka 2012/2013, kiwango cha kufanikisha ununuzi, kipengele namba tano, namba 10, wanataka kwamba, *Belo* litakalokuwa limetayarishwa kwa ajili ya kwenda sokoni, liwe na majani ya tumbaku ya *grade* moja kwa asilimia 100, jambo ambalo haliwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa wateuzi au hawa ma-*classifiers*, ndiyo wanapata mwanya wa kuomba rushwa kwa wakulima. Mimi nataka niiombe Serikali, kama inaweza, itoe *classifier* wake mmoja, aje kule Jimboni tumkabidhi *burn*, achome Tumbaku, a-*classify* mwenyewe tuone kama *Belo* moja ataweza kuweka majani ya aina moja kwa asilimia 100, hawezi! Sasa mkulima wa kijijini ambaye haelewi vizuri masuala ya ku-*grade*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ni kengele ya pili.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Mheshimiwa Dkt. Fetus Limbu ajiandae.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi ni mjumbe mwaminifu wa Kamati iliyochambua hoja hii. Tumewasilisha taarifa yetu leo asubuhi, tumeiunga mkono na mimi naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kwa ajira na uchumi wao. Hii ina maana kwamba kwa kila Watanzania watano, wanne, ngozo yao ya maisha ni kilimo. Kwa mujibu wa sensa tuliyoikamilisha mwaka jana, tuliambiwa Watanzania tuko milioni 45, ina maana Watanzania wanaotegemea kilimo ni takribani milioni 36. Pamoja na asilimia kubwa hiyo, mchango wa kilimo katika uchumi wa nchi hii, ni asilimia 26 tu! Tafsiri iliyo dhahiri hapa ni kwamba, kilimo chetu kwa ujumla wake hakiendeshwi kwa tija, ni kilimo duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wakulima wa Tanzania ni wakulima wadogo wadogo wanaoitwa *small holder farmers* au *peasants*, ambapo mashamba yao yana ukubwa mdogo sana, ni wastani wa hekta 0.9 -3 na wakulima wengi wa Kitanzania hawatumii teknolojia ya kisasa ama kwa sababu ya kukosa uelewa wa kilimo cha kisasa au kwa sababu wamekosa pembejeo stahiki.

Upatikanaji wa mbegu bora na mbolea ni tatizo na kwa kiasi kikubwa wakulima wetu wanategemea mvua kwa ajili ya kustawisha mazao yao. Dhana wanazotumia ni duni na zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni asilimia 10 tu ya wakulima wetu wanaotumia Matrekta. Asilimia 20 ndiyo wanatumia majembe ya kukokotwa na wanyama, waliobaki asilimia 70 wanategemea jembe. Tumeambiwa takwimu hizi zimepungua kidogo mpaka kufikia 64, lakini hata hivyo siyo za kujivunia kwamba theluthi mbili ya Watanzania wanategemea jembe kwa kilimo na kweli tukitaka kuwa *serious*, kuleta mageuzi ya kilimo, hatuwezi tukategemea jembe la mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi kwamba Wakoloni walipokuja hapa nchini, walitukuta tunatumia jembe kwa kilimo, walipoondoka wakatuacha tunatumia jembe la kilimo, tofauti ni kwamba walipokuja, hayo majembe tulikuwa tunatengeneza wenyewe lakini walipoondoka, tunaagiza kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa ni kulinganisha idadi ya wakulima na idadi ya Watanzania, nina mapendekezo na maangalizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii asilimia 80 ya Watanzania tunaosema wanategemea kilimo, tumeisikia kwa zaidi ya miaka 20. Mimi nadhani umefika wakati wa kupitia tena kwa sababu kumekuwa na mabadiliko mengi tena makubwa katika sekta ya kilimo, sekta ya kijamii, lakini pia kuna uhamiaji mkubwa sana wa vijana wetu kwenda mijini, huenda hii tarakimu imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mchango mdogo wa kilimo katika uchumi wa Taifa, ni ishara kwamba kilimo chetu kinahitaji elimu kutolewa kwa wakulima wetu na

vilevile zana za kisasa zipatikane ili kilimo chetu kiwe na tija. Mwananchi wa kawaida ukizungumza habari za kilimo, yeye anafikiria shamba, jembe, kupanda, kuvuna na kula, lakini tuweke msisitizo katika elimu kwa wakulima wetu, kwamba tuanzie kwenye ardhi iliyo bora na ulimaji ulio sahihi unaofuata misimu, mbegu bora, mbolea sahihi na ya kutosha, maghala, kuongeza thamani ya mazao mpaka kuwepo na soko la uhakika. Haya yakitimizwa matokeo yake tutapata mavuno makubwa na hii itamhamasisha mwananchi huyu mkulima kulima zaidi. Hakuna Taifa duniani ambalo limepiga hatua kubwa katika maendeleo kwa kutegemea kilimo pekee. Sisi Watanzania wanne kati ya watano ni wakulima, hao wakulima wakilima mazao ya chakula cha kutosha watamuuzia nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Uholanzi ambayo kwa eneo inaingia mara 22 katika Tanzania, ina wakulima 50,000 tu na *population* yao ni 16.6 milioni, kwa hiyo, idadi ya wakulima ni asilima tatu ya Waholanzi wote. Pamoja na uchache wao, wakulima hao mchango wa kilimo katika uchumi wa nchi hiyo ni asilima 10. Isitoshe Uholanzi ni nchi ya pili ulimwenguni kwa ku-*export* chakula na mazao ya kilimo, inafuata Marekani ndiyo wanakuja wao. Tuna mengi ya kujifunza kutoka Uholanzi. Nikumbushe nilichosema, ni kwamba wakulima wa Kiholanzi wako asilimia 50 na asilimia tatu ya Waholanzi wote wanachangia asilima 10 ya uchumi wa Taifa, wanalisha Taifa na kuuza nje. Kwa Watanzania, wakulima wako 36 milioni ambayo ni asilimia 80 ya Watanzania wote lakini wanachangia asilimia 26 tu katika uchumi wa Tanzania na hawawezi kulisha Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India ni nchi kubwa kwa eneo na kwa idadi ya watu, imedhamilia kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kutumia ujuzi na uzoefu wa hawa Waholanzi. Nchi hizo mbili zimekubaliana kuanzisha vituo 10 na tayari wameshavisambaza katika nchi yao, vinaitwa *Dutch Indo-Centers of excellence* ambavyo vitatoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima na wajasiriamali, wanataka kuchota mbinu wanazotumia Waholanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali ni kwamba, ipo haja kwa Serikali kufanya mageuzi makubwa katika mwelekeo wa sera zetu na lengo hapa ni kupunguza idadi ya wakulima hasa wakulima wadogo. Mikakati iwekwe itakayowawezesha wakulima wadogo kuwa wa kati na wakubwa na wakati huo huo viwanda vidogo na vikubwa vikiwemo vya kusindika mazao vianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ilianzishwa kwa madhumuni ya kutengeneza nyenzo na vifaa vya teknolojia nyepesi ambavyo vinaweza kununuliwa na wananchi, lakini nadhani *potential* yake hatujaitumia sawasawa. Nadhani tukiwekeza katika *SIDO* na tukaiimarisha wananchi wengi wanaweza wakapata vitu kama vya kusindika mafuta, nyuzi za Pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema naunga hoja mkono na bado naunga hoja mkono, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa kwa mchango wako na Waheshimiwa Wabunge sasa nitamwita Mheshimwa Dkt. Limbu atafuatiwa na Mheshimwa Josephine Genzabuke!

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Waziri wa Kilimo, Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia na pili naomba kuzungumzia kuhusu bajeti ya Wizara kuhusiana na utegemezi wa fedha za nje. Bajeti hii imekuwa tegemezi sana kwa fedha za nje kiasi kwamba bajeti hii ambayo inaendelea ina fedha za nje bilioni 52 ukilinganisha na fedha za ndani bilioni 15

Mheshimiwa Mwenyekiti, afadhali mwaka huu bajeti ambayo Waziri anaomba fedha, bajeti ya fedha za ndani imeongezeka kwa 45% kutoka bilioni 15 kwenda 24, lakini fedha za ndani nazo zimeongezeka japokuwa ni faraja

kwamba sasa angalau umuhimu umeonekana kwamba, tumeongeza fedha za ndani kwa ajili ya kuhudumia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo linaikumba sekta hii muhimu ambayo ni uti wa mgongo ni kwamba fedha zinazotolewa na Serikali zinatolewa kidogo mno na zinatoka polepole. Kwa mfano, mpaka tarehe 9 Machi kama Waziri alivyosema kwenye hotuba yake zimetoka 19% peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sekta muhimu na ya kipaumbele kama Kilimo kuitengea fedha kiasi kidogo namna hii hatuitendei haki. Ni matumaini yangu kwa miezi iliyobaki angalau kiasi hiki kitaongezeka kuzidi hata 50% ambayo inatia mashaka. Kama mpaka Machi imekwenda 19% peke yake kuna mashaka kwamba mpaka tunafika mwisho wa mwaka wa fedha zitakuwa zimetolewa hata nusu ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*declare interest* kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba mpaka kesho. Bodi ya Pamba katika mwaka wa fedha 2006/2007 iliidhinishiwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya shughuli za matumizi ya kawaida. Lakini fedha hizi zimekuwa zikipungua ama ruzuku imekuwa ikipungua kwa kiasi ambacho kinakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana fedha iliyokuwa imeombwa ilikuwa ni shilingi milioni 500 kwa ajili ya *OC,* lakini ikatengewa shilingi milioni 150. Mwaka huu hii shilingi milioni 150 imepunguzwa mpaka shilingi milioni 80. Shilingi milioni 80 utafanyia nini katika Sekta ya Pamba nchi nzima; mikoa 14 Halmashauri za Wilaya zaidi ya 30 na Watanzania wanaotegemea zao hili milioni 14, lakini unatenga shilingi milioni 80 ambazo zinatosha matumizi ya mwezi ya ofisi na huduma katika Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ilifikirie hili kwa makini ili angalau iweze kuongeza ruzuku kwa Bodi ya Pamba. Sijui kilitumika kigezo gani katika kugawa fedha

kwenye Bodi za Mazao kwa sababu nyingine nyingine zina fedha kwenye shilingi milioni 550, sasa unalipa zao moja shilingi milioni 350, zao lingine tena muhimu ambalo linaajiri watu wengi kama Pamba unalipa shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri alitazame hili tena ili aongeze kiasi hiki, tulikuwa tumeomba angalau kama Serikali ina matatizo ya fedha na kama Wizara imebanana basi angalau ingeiacha ruzuku katika kiasi kile cha mwaka jana cha shilingi milioni 150, angalau! Lakini mahitaji halisi yako kwenye shilingi milioni 500 ambayo tulikuwa tumepeleka kama ombi la ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tuhuma ambazo zina zaidi ya miaka minne sasa kwamba kuna fedha ambazo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa pamba kwenye bei zimeliwa, shilingi bilioni 2.4. Sasa huu ni mwaka wa nne. Kamati iliyokuwa ya *POAC* iliagiza Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG)* akague, Bodi ya Pamba wamemsubiri aje akague, lakini hajafika, ameandikiwa barua mara mbili aje akague lakini hajafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itolee maelezo hili suala ili lifike mwisho na Bodi ya Pamba iweze kusafishwa kama haina tuhuma na kama ina tuhuma, basi hatua ziweze kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya mkulima wa pamba; katika mazingira ya soko huria na ukweli kwamba bei ya pamba inatokana ama inategemea zaidi soko la dunia, kuyumba kwa bei katika soko la dunia kwa vyovyote vile bila kuwa na njia za kumsaidia mkulima ataendelea kupata shida. Njia mojawapo ni kama ile aliyoitaja Mheshimiwa Waziri ya kuanzisha Mfuko Maalum wa Kufidia Bei ya Mazao yaani *Price Stabilisation Fund.* Naomba Serikali iharakishe mchakato huu ili Mfuko huu uweze kuanzishwa kwa sababu utamsaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini njia nyingine tunauza pamba yetu 70% ikiwa ghafi, inakuwa *delighted,*

inaondolewa nyuzi na nyuzi ndiyo tunauza, lakini kwa kufanya hivyo tuna *export* ajira na tunampunguzia bei mkulima. Mpango aliousema Mheshimiwa Waziri kwamba, *NSSF* wametoa ofa au wamejitolea kuchangia 60% ili kuanzisha viwanda vya uchakataji, viwanda vya nyuzi na vya nguo, lakini inaonekana wafanyabiashara wa kutoa hii 40% hawapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, masharti ya Benki ni magumu, lakini naomba Serikali iingilie kati suala hili aidha, itoe 40% inayobaki baadaye itakuja kuuza hisa ama ichangie katika hii 40% ya sekta binafsi, Serikali ichangie 20% ili angalau tuanze kuwa na viwanda ambavyo vitachakata pamba na kumsaidia mkulima wa pamba ili bei ya zao hilo iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo zao la pamba tu bali hata zao la korosho, vile vile kwa nini Serikali inapata kigugumizi kuingia katika kuwekeza katika kuingia ubia na sekta binafsi maadamu tayari *NSSF* wameshajitolea, ameshatoa ofa siyo tu kwenye pamba bali hata kwenye korosho pia. Sekta binafsi ikiachiwa peke yake itachukua miaka mingi, hili suala lichukuliwe maamuzi ya haraka ili viwanda hivi viweze kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba wakulima wanahamasishwa waweze kulima, lakini wanapolima kunakuwa hakuna masoko. *CRDB* wametoa fedha kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha zabibu. Suala hili alilisema asubuhi Mheshimiwa Chibulunje, wameji-*organise* vizuri, wamelima vizuri kwa teknolojia ya kisasa, *drip irrigation,* lakini mazao hayana soko. Haiingii akilini! Kwa hiyo viwanda vianzishwe kama nilivyopendekeza kwenye zao la pamba na korosho lakini pia kwenye zabibu na mazao mengine, Serikali iingilie kati na isiachie soko huria ama sekta binafsi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ili tuweze kumsaidia mkulima wa pamba, kilimo cha mkataba ndiyo njia pekee ambayo itaweza kumsaidia. Kwa mfano, mwaka huu

pembejeo kwa maana ya viuadudu ambavyo vilikuwa vimeagizwa havikuweza kuuzwa, wananchi walikuwa hawana fedha za kununua kwa fedha taslimu na kwa hiyo matokeo yake kama kutakuwa na wadudu wengi watakaoshambulia zao, basi uzalishaji wa zao hilo utapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna matatizo na kilimo cha mkataba, basi matatizo hayo yarekebishwe, yaainishwe na hatua hiyo najua inaendelea, uainishwe upungufu uliopo kwenye utaratibu wa sasa......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili!

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Limbu. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata nilisema ni Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Clara Mwatuka.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa kuwa nchi nzuri yenye milima, mabonde, bahari, maziwa, mito mikubwa na mito mingi midogo midogo. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kutumia fursa hizo ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia iweze kujielekeza katika kilimo cha umwagiliaji, tukiweza kufanya hivyo tutaweza kuwasaidia wananchi wetu na wataweza kulima kilimo cha umwagiliaji na wataweza kukuza uchumi wao kwa kutumia kilimo hicho hatimaye kuweza kujipatia kipato na kuweza kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Wabunge wenzangu ambao wamelalamikia ukosefu wa masoko ya mchele na sukari. Wananchi wetu wanapokuwa wanalima wanakopa mikopo kwa ajili ya kununulia mbolea na hata madawa, hivyo wanategemea wanapokuwa wamevuna wakiuza mazao yao waweze kulipa madeni ambayo wamekopa kwa ajili ya kununua vifaa au pembejeo kwa ajili ya kutumia wakati wanapolima mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iwasaidie wakulima hawa ambao wameweka mchele kwenye maghala yao na mipunga ili kusudi waweze kupata soko ikiwa ni pamoja na kusitisha michele inayotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa kwamba, michele inayotoka nje pamoja na sukari haizuiliwi kuingia nchini, lakini tunaomba sasa wakati michele hiyo inaingia Tanzania, basi Serikali ijielekeze kutafuta soko la wananchi wa Tanzania au wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, mwezi uliopita kabla hatujaja hapa Dodoma tulitembea katika Mkoa wa Morogoro. Tulipofika Morogoro, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Bendera alitoa malalamiko kuhusu Sukari ambayo imerundikana katika Viwanda vya Sukari vya Mtibwa na Kilombero. Ma-*godown* yamejaa, sukari imejaa kwenye ma-*godown* lakini wananchi wanalalamika kwa sababu wananunua sukari kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wananchi wanaendelea kupunjika kwa kununua sukari kwa bei ya juu wakati viwanda vyetu vya ndani katika maghala yake kumejaa sukari? Naomba Waziri atafute dawa ya kuhakikisha sukari hiyo ambayo imerundikana katika ma-*godown* inapatiwa soko ili wananchi waweze kunufaika kwa kutumia sukari inayozalishwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu kuchelewa kwa mbolea kuwafikia wakulima. Kwa

mfano, katika Mkoa wa Kigoma, mbolea imekuja kufika mwezi wa kwanza wakati mvua za kwanza za mwezi wa Kumi na Kumi na Moja ni mvua za kupandia, sasa unapopeleka mbolea mwezi wa kwanza mbolea hiyo inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuwa na wasiwasi kwamba inawezekana kuna hata baadhi ya viongozi ambao wanahusika kabisa kukwamisha mbolea isiwafikie wakulima kwa sababu ambazo wao wanazifahamu. Kwa sababu, mbolea hizo zinachelewa haziwafikii wakulima, lakini ukienda baada ya kuwa zile mbolea zimefikishwa mwezi wa Kwanza katika maeneo husika hukuti mbolea na mbolea yote inakuwa imeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza na ikiwezekana hata Waziri atusaidie, ile mbolea ambayo inapelekwa mwezi wa Kwanza huwa inafanya kazi gani? Kama haifanyi kazi, tungejiridhisha tu siku moja kwa kwenda kukagua tuone mbolea ile kwa sababu haikufanya kazi, watuonyeshe imerundikwa katika magodown gani kwa sababu kuna ushahidi kabisa kwamba, mbolea ile haiwafikii wakulima, inacheleweshwa kwa makusudi mazima na ikishafika inafichwa. Matokeo yake inakwenda kuwanufaisha wananchi wa Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri atusaidie Watanzania wote kuhakikisha mbolea haichakachuliwi na inakuwa ni mbolea inayowasaidia Watanzania na siyo nchi jirani. Nchi jirani zinufaike kwa kununua mazao ambayo tumelima sisi Watanzania na tumetumia mbolea ya kwetu kupandia na kukuzia mazao yetu, hatimaye tukawauzie wananchi wa Burundi na siyo wao wafaidi mbolea, halafu sisi tusiweze kunufaika. Naomba kabisa hilo nalo litazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vil evile nawaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuwa kwenye Kamati zile zinazogawa mbolea. Waheshimiwa Wabunge ndiyo tunaoulizwa maswali tunapokwenda kwenye majukwaa. Ukisimama kwenye jukwaa wananchi wanakuuliza,

Mheshimiwa Mbunge mbolea ilikuja lakini hatukuiona, lakini wakati wanapanga Kamati za Kugawa Mbolea Wabunge wanakuwa hawashirikishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba kabisa Wabunge pamoja na Madiwani japokuwa hata baadhi ya Madiwani nao siyo waaminifu. Nasema na msema ukweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu, wapo baadhi ya Madiwani nao wanafanya biashara ya kuuza mbolea. Kama wapo na nina hakika wapo, wajisahihishe na wajirekebishe. Tukisaidiana Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, Ma-*VEO* na Wenyeviti wa Vijiji malalamiko yatakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwataarifu na wananchi wetu kwamba, wanakuwa ni wa kwanza kulalamika pale wanapokuwa wamepatwa na matatizo, naomba na wao wanapokuja kusainishwa zile vocha kwa kupewa sh. 5,000/= au shilingi 2,000/= wakatae na wao wanatuletea matatizo. Wanasainishwa, wanapewa fedha kidogo, hatimaye walanguzi wanakuja kubeba ile mbolea na ikiondoka baadaye wanakuja kuilalamikia Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba yenyewe ndiyo inayochakachua mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweka mipango madhubuti kwa ajili ya kuwasaidia wananchi isipokuwa baadhi ya watu ambao siyo waaminifu ndiyo walanguaji na wanasababisha matatizo kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Kasulu. Wakulima katika Wilaya ya Kasulu wamechakachuliwa na makampuni haya yanayokuja kununua tumbaku, wakati mwingine mtu anakuwa na tumbaku yake, lakini ili aweze kuuza wanalazimika kuchangishana pesa kuwapatia wale wanunuzi. Naomba kama wananisikia waweze kuacha tabia hiyo ya kuwalangua wananchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Josephine, na sasa tunaendelea na Mheshimiwa Clara Mwatuka atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi!

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia zaidi zao la korosho ambalo ni kilio kikubwa kwa watu wa Kusini. Kwa kweli zao la korosho lilikuwa ni zao mama, zao tegemezi kwa biashara, lilikuwa linawapatia wananchi pesa na wengine wakatajirika kupitia zao hili la korosho. Lakini kadri miaka inavyoendelea sasa hivi imefika mahali hasa kwamba wananchi wengine wanaweza wakaamua basi waache kulima korosho kama wengine walivyoacha kulima karafuu kule Zanzibar kwa kuona kwamba soko halina uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho mwanzoni ilikuwa inanunuliwa na Wahindi walikuwa wanakwenda vizuri tu hata hakukuwa na malalamiko. Lakini baadaye ilivyokuja kuzuka mpango wa stakabadhi ghalani imekuwa tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani siyo mbaya kama ungekuwa unakwenda vizuri. Lakini hii hali ya kwamba, watu wanapewa pesa zao kwa mikupuo miwili, unapata nusu nusu kwa kweli inarudisha maendeleo nyuma. Kwa sababu hata wafanyakazi, hata sisi hapa ndani sidhani kama kuna ambaye anaridhika kupata mshahara wake nusu nusu. Maana hapa tungekuwa

tunapata nusu nusu *ATM* zingekuwa zinatia tabu, lakini kama ni *perdiem* tunapata zote na mshahara tunapata wote, vinginevyo tungekuwa tunalalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na wakulima pia inawauma, kwa kweli wanalalamika na hawana wa kuwasemea, ni sisi hapa ambao inabidi tuwasemee, utaratibu huu pengine uondolewe. Kwa sababu zao la korosho hivi sasa wanaonufaika ni wale wa Ushirika, Vyama vya Msingi na Mashirika mbalimbali ambayo kwa kweli hayana msaada wowote kwa wakulima kutokana na makato wanayokatwa ambayo ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria mkulima au mfanyabiashara, niseme anapokusudia kununua mazao kwa ajili ya biashara, magunia anatafuta mwenyewe, anajua kwamba mazao nitakayokwenda kununua yanahitajika magunia, wapi atatunza, atayasafirisha namna gani, hayo ni majukumu yake mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ajabu ni kwamba mkulima wa zao hili la korosho kila kitu kinamgharimu yeye; magunia yeye, halafu kuna mambo mengine humo ndani ambayo hayaeleweki, kuna unyaufu. Korosho zile zinakaa pale kwa muda mfupi tu, inawezekanaje kwamba pawe na kiasi cha unyaufu anaokatwa mkulima eti kwamba zimenyauka, zimepungua kilo. Hili halikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusafirisha pesa kutoka benki kwenda pale wanaponunulia korosho, pesa hizo zinasafirishwa na mkulima wa korosho. Yaani pesa hizo zina uzito gani mpaka atozwe huyu mkulima, huu ni uonevu. Naomba kwa kweli Serikali iliangalie hili. Mambo ni mengi sana anayokatwa mkulima. Sasa watu wamefikia hatua wanaona ni afadhali uondolewe huu mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikuhakikishie kwamba, kuna utaratibu watu wanajaza fomu ya kuomba Serikali iondoe mfumo huu kwa sababu unarudisha maendeleo nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho, mpaka kupatikana mazao ya kutosha ni kwamba mashamba yanakuwa makubwa, mkulima hawezi kulima mwenyewe pekee yake, kupalilia hiyo mikorosho, anahitaji nguvu kutoka kwa wananchi wenzake. Wanakwenda kwa mkopo kwamba, akishauza korosho zake basi aweze kuwalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hali hii ya kulipwa nusu nusu, akipata nusu ya kwanza ile anamaliza kuwalipa wale waliomsaidia kazi, anahitaji kupata matibabu, anahitaji kusomesha watoto, zile zote zinakwisha. Sasa kama alikusudia kwamba anataka kujenga nyumba, kama angepata pesa zote kwa mara moja, ukweli angekuwa amejenga nyumba. Lakini sasa hii nusu inarudisha maendeleo nyuma kwa sababu zile zinazobaki za pili kupatikana kwake kuna tabu, hazipatikani kwa muda muafaka, zinachukua muda mwingi kabla hajapata na isitoshe zile pesa za kwanza kwa kuwa zilikwisha, lengo halitimii. Kama alitaka kujenga nyumba basi limekatika ina maana kwamba pale maendeleo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, hao wanaonufaika wa Ujamaa na Ushirika, utakuta mwingine ameanza kazi mwaka huo huo, lakini anaweza kujenga nyumba ya kifahari, atanunua gari, utajiuliza kwa mshahara gani unaomfikisha huyu kupata vitu vyote hivyo?

Mheshimiwa Spika, zamani tulielewa kwamba watu wa Kaskazini kwenda kufanya kazi Mikoa ya Kusini ilikuwa ni kero kubwa na kwamba walikuwa hawataki. Lakini hivi sasa watu wanakimbilia sana kwa sababu wakienda kule wanatajirika mara moja. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali huo mfumo siyo mbaya, nilimsikia Naibu Waziri hapa juzi kwa maelezo yake alitutia moyo na kuona kwamba kwa kweli ingekuwa inafuatwa hivi mambo yangekuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa utakuta akina MAMCU hawana msaada wowote, hawana mchango wowote, lakini ndiyo matajiri wakubwa kupitia pesa za

korosho. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali hili litazamwe sana kwa uangalifu kwa sababu zao hili ndiyo wanalotegemea wakulima wa Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo utakuta wa Vyama vya Msingi hawa Makarani wanakata sana na Wenyeviti na Makatibu kile Chama ni chao kwamba hao wanachama hawawezi kuuliza chochote wakiuliza Ujamaa na Ushirika wanakuja juu na kutetea sana viongozi kwa kweli inakatisha tamaa. Naomba hawa nao waangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na hilo, kuna mazao machanganyiko. Kwa kweli mazao ya chakula yanayolimwa kule Kusini, nikichukulia Wilaya ya Newala wanalima mihogo. Kwa hiyo, makopa yanakuwa mengi yanakosa soko. Kwa hiyo, mengine wanafikia hatua ya kuyamwaga porini kwa kukosa soko. Kunalimwa njugu mawe, kunalimwa karanga, kunalimwa kunde Mikoa ile lakini soko la uhakika hawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndipo pale inapofikia, watu wakauza vyakula vyao kwenye *kangomba,* hawafanyi makusudi. Hakuna kingine wanachotegemea, wanategemea kipato chao kutokana na kilimo. Sasa zinapokosekana fedha, akishavuna mahindi yake anajua hana chumvi, hana sabuni, hana pesa za kumpeleka mtoto hospitali, anapokuja mwenzake kutaka ampatie chakula inabidi amuuzie kwa *kangomba* ili apate senti amalizie matatizo yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusiwalaumu tu kwamba wanauza kwenye *kangomba*, korosho zinauzwa kwenye *kangomba* wakati soko linachelewa na matatizo wanayo kwa nini wasiwauzie wale ambao wanahitaji? Kwa hiyo, Serikali iangalie, iwapatie soko ili pale wanapokatazwa kuuza kangomba watoe fedha mbadala au msaada mbadala kwamba tunawazuia hili basi hebu tuwape ili ziweze kuwasaidia. Naomba sana soko litafutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye pembejeo, ni tabu, upatikanaji unakuwa wa kusuasua, bei imekuwa ghali, mkulima anashindwa, ziende kwa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kilimo tulichonacho ni kile cha jembe la mkono ambalo hivi sasa limepitwa na wakati. Nimemsikia mwenzangu mmoja hapa anasema matrekta kwao yanapatikana. Kwetu sisi Kusini matrekta yamekuwa ni kitu ambacho ni haramu. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali, tafadhali ili kuinua uchumi wetu, tupate matrekta na sisi tujidai, tupanue kilimo ili tupate pesa za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walileta *Power Tiller* wakati ule, *Power Tiller* hivi sasa hazitegemewi kwa kilimo, zile watu wamezifanya kwa ajili ya *transport.* Kwa hiyo, naomba tuangaliwe sana na tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Clara kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Selemani Zedi, naona hayupo, anafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kirigini na yeye hayupo. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Azza Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kusema kwamba, ukiona kwako kunaungua basi kwa mwenzako kunateketea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kusema hivyo kwa sababu, kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ukurasa wake wa 10, kuhusu hali ya chakula. Naomba nisome kwa ruhusa yako paragraph ya kwanza anasema: “Aidha, Serikali imekuwa ikitoa chakula

cha njaa kulingana na maombi yanayowasilishwa na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya."

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisikitisha sana, toka nimeingia ndani ya Bunge hili hakuna siku ambayo nimesimama na nisiongee kuhusu suala la njaa katika Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hotuba hii hii ya Waziri, kule ndani kwenye takwimu zake ukurasa wa 80 na 81 anaonesha Mkoa wa Shiyanga; Shinyanga Mjini jumla ya mgao tani 144, uchukuaji tani 144, salio hakuna. Shinyanga Vijijini, tani 314, salio hakuna. Ukurasa wa 81, Shinyanga Mjini inaonekana jumla ya mgao ni tani 4,000, uchukuaji hakuna, salio tani 4,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakatisha tamaa. Halmashauri zetu zimekuwa mara kwa mara zikiomba chakula hicho Ofisi ya Waziri Mkuu. Nakumbuka mwaka jana wakati nikichangia Ofisi ya Waziri Mkuu mwezi Julai, nilisema neno hili na leo narudia tena kulisema, hatupendi kuomba chakula cha njaa, bali hali ya hewa iliyopo Mkoa wa Shinyanga ndiyo inayotufanya tusimame hapa na kuomba chakula hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kweli Waziri anasema wanatoa chakula kutokana na Halmashauri kuomba, siyo kweli ni uongo. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imeshaomba chakula zaidi ya mara tatu. Mara ya kwanza imeomba chakula tani 4,700, zimeletwa tani 314 pekee yake mpaka hivi ninavyoongea na ilikuwa mwaka jana mwezi Julai, mpaka hivi ninavyoongea ni tani 314 ndiyo zilizoletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Halmashauri haikuchoka imeendelea kuomba, Mbunge wa Jimbo amekwenda mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu akaiona hali halisi, akaiandikia Halmashauri kwamba watatupa tani 4,000, ulikuwa mwezi wa Februari, mwaka huu.

Baada ya Waziri Mkuu kuandika ile barua mpaka hivi ninavyoongea hakuna chakula ambacho kimefika Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza chakula hicho ambacho tulikiomba mwaka jana, tunakisema ni cha mwaka jana au ni cha mwaka huu, lakini mpaka hivi ninavyoongea chakula hicho hakijafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu anatujua watu wa Shinyanga na anatutetea, lakini waliopo chini yake wanamwangusha. Najiuliza hiki Kitengo cha Maafa kiko kwa sababu gani? Wanapotoka huku wanapokwenda kwenye Halmashauri zetu kwamba, wanakwenda kutathmini hali ya chakula, wanakwenda kuishia kwenye Ofisi za Halmashauri, sana sana wakitoka watakwenda kwenye Kata moja au Kata mbili na si vinginevyo. Sasa kama ndiyo hivyo kwa nini wasiziache Halmashauri ndiyo zikafanya tathmini ya chakula na wakazifanyia kazi taarifa zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linanisikitisha sana na kwa sababu hiyo basi, nasema siungi mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mpaka pale nitakapopewa majibu sahihi, kwa sababu wananchi wa Shinyanga watanishangaa sana. Sasa hivi ni kipindi cha mavuno, debe la mahindi linauzwa sh. 10,000/= mpaka sh. 12,000/=, wakati lilipaswa kuuzwa sh. 5,000/=, hiyo ni hali halisi iliyopo Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mvua zinazonyesha sasa hivi hata kwa wale wachache ambao walitegemea hata mpunga watavuna, hawavuni tena, kwa sababu mpunga ule umeharibiwa na mvua kubwa zinazonyesha Mkoa wa Shinyanga. Ina maana narudia kutangaza tena, Mkoa wa Shinyanga tuna chakula kwa mara nyingine wakati chakula cha mwaka jana sijakipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihame kwenye hali ya chakula. Niende kwenye suala la umwagiliaji.

Inanisikitisha sana, hotuba yote ya Waziri hakuna Wilaya hata moja ambayo ameonesha kwamba kuna bwawa hata moja litawekwa la umwagiliaji. Hapa inanipa tafsiri kwamba, aliyenacho ndiyo anaongezewa asiyekuwa nacho aendelee kukosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maana gani kusema hivyo. Kigoma wana mvua za kutosha, lakini humu kuna bwawa linachimbwa Kakonko. Yaani maeneo yote ambayo wana mvua za kutosha ndipo ambapo kuna kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Mkoa wa Shinyanga wametuweka kwenye fungu gani? Nikiangalia Shinyanga, Simiyu, Geita hakuna sehemu yoyote ambayo kuna kilimo cha umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri labda atwambie kama sisi watu wa Kanda ya Ziwa tumemkosea Mheshimiwa Waziri atwambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipenda sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na mtu anayekupenda lazima akwambie ukweli. Nisiposema ukweli sijakusaidia bado. Kama kila siku Shinyanga tunaomba chakula na chakula chenyewe hamtupi na kilimo cha umwagiliaji na kwenyewe mnatunyima mabwawa mnategemea tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha na inakatisha tamaa. Lakini bado nitarudia hoja yangu ile ile, Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni Serikali yangu, nasema naipenda na inafanya kazi vizuri, lakini watendaji wanaiharibu. Iliahidi katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Kijiji cha Kata ya Mazengwa kuchimba bwawa la umwagiliaji katika mradi wa umwagiliaji toka mwaka 2007, mwaka 2011 nimelisema humu ndani Bungeni, mwaka jana nimelisema na leo narudia kulisema, lakini bado kwenye hotuba ya Waziri sioni kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika sasa hivi Shinyanga mvua zinavyoonyesha mito inatiririsha maji, maji hayana

mahali pa kwenda, mwishowe maji yanakwenda kuangusha nyumba za wananchi. Lakini je, tungekuwa tumechukua hata hiyo skimu moja ninayoisema maji haya ya Mto Manonga yangekusanywa na lile bwawa tungeweza kusaidia angalau Kata moja kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, lakini maji yale yanapotea. Serikali inaangalia, haioni iyapeleke wapi, wananchi wanalia njaa na Wabunge wanalia njaa, tunafanya nini? Inasikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwambia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, nawapenda sana, lakini kwa hoja hii nawapenda kulikoni wananchi wa Shinyanga. Yaani wananchi wa Shinyanga ni zaidi yenu nyie, sitounga mkono hoja hii mpaka niambiwe bwawa la Masengwa litachimbwa lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwaambie, niliuliza swali humu Bungeni mwaka jana na likajibiwa kwamba Wilaya ya Kahama ndiyo Wilaya pekee yake ambayo imeonwa na Serikali itatengwa kwa ajili ya kusaidia Mkoa wa Shinyanga kwa ajili ya chakula. Lakini bado kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona kitu chochote ambacho wanasema Kahama wanafanya kitu gani kwa ajili ya kuukomboa Mkoa wa Shinyanga kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema, siungi mkono bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa sababu hizo nilizozitaja. *(Makofi)*

*(Kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza tunakushuru kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, kabisa naunga mkono hoja hii kwa sababu mimi mwenyewe ni Mwanakamati ambaye nimeishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ushauri kwa Serikali. Serikali ili iweze kutatua kero nyingi za wakulima hapa nchini, lazima tuwekeze kwenye kilimo. Lazima tuweke bajeti ya kutosha ambayo itakidhi mahitaji ya wakulima wa nchi hii. Wakulima wa nchi hii ni wengi karibu asilimia 75 wanategemea shughuli za kilimo. Kwa hiyo, tusipowawezesha hatuwezi kufanya shughuli zozote za kilimo. Ni vyema Serikali ikajiwekeza kwa nguvu zote kuhakikisha inatenga fedha nyingi kwa ajili ya kuendesha kilimo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itawekeza kwenye kilimo, naamini vijana walio wengi katika nchi hii watapata ajira, naamini akinamama walio wengi katika nchi hii watapata ajira za kufanya shughuli zao binafsi. Naiomba Serikali iwekeze fedha nyingi kwenye pembejeo, iweke ruzuku ya pembejeo za kutosha, tena kwa mazao yote. Tuwekeze kwenye mazao ya chakula, tuwekeze kwenye mazao ya biashara ili yaweze kuwasaidia wananchi kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itawekeza kwa nguvu zote, naamini Watanzania walio wengi watakuwa wamenufaika na Serikali yao ya Chama Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itoe kodi za kilimo kwenye vifaa vya kilimo na madawa. Kama tutatoa hizo kodi tutakuwa tumewasaidia sana wakulima ili waweze kuendesha shughuli zao kwa upana zaidi. Leo hii wakulima wengi wanapata shida sana, wananunua pembejeo kwa bei ghali kwa mfano *sulphur* kwa zao la korosho, wanapata tabu sana wakulima wa korosho kwa sababu *sulphur* zina bei ya juu na bado kuna urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iweze kutatua eneo hilo, lakini iweke mazingira mazuri kwenye vifaa vya kurahisisha shughuli za kilimo kama matrekta ambayo kama tutakuwa tumetoa kodi na tukasambaza matrekta kwa wingi, naamini nchi hii itakuwa na uzalishaji mkubwa sana, Serikali hii ya nchi yetu itakuwa imetatua tatizo la njaa, nchi yetu itakuwa na kipato kikubwa sana kwani tutakuwa na mazao yanayouzwa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninaloishauri Serikali ni kutafuta masoko. Kelele nyingi za Wabunge hapa wanalalamikia masoko. Tuna mazao ya biashara ambayo ni muhimu kwa Taifa hili na yanayoongeza kipato kwa nchi hii. Kama Serikali ikiwekeza vizuri tuna uwezo wa sekta ya kilimo kutegemewa ikawa ni ya kwanza kabisa kwa uzalishaji. Niiombe Serikali ifanye kila jitihada za makusudi kuhakikisha tunapata masoko yenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele iliyopo kwenye zao la korosho ni kwa sababu hatuna soko la uhakika. Masoko yale tunategemea wafanyabishara wenye asili ya India pekee, huko ndiko ambako tunakotegemea korosho ya nchi hii iende kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ipanue wigo na ifikirie sasa kurudisha viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa kwenye usindikaji wa zao la korosho ili viweze kuwa miliki ya wakulima, vitawasaidia sana kupandisha thamani ya mazao yake. Ni vizuri tukiwekeza hapo tunaweza tukawasaidia sana wakulima tukaachana na kelele za muda mrefu ambazo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuwamilikisha ardhi wakulima. Wakullima walio wengi sana hawana ardhi ambayo inatambuliwa na Serikali. Wakulima wanalima tu kwa mazoea waliyozoea. Kama Serikali itawawezesha wakulima wakawa na miliki ya ardhi, wana uhakika wa kuweza kukopeshwa na vyombo vya fedha wakawa na

uzalishaji mkubwa ambao utawasaidia kutatua kero mbalimbali katika maisha yao na kuongeza uchumi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Serikali iharakishe mpango wa kuwamilikisha ardhi katika maeneo mengi ambayo hawana miliki ya ardhi. Tukiwasaidia katika eneo hili tutakuwa tumepanua wigo wa kuwafanya Watanzania wawe na uhakika wa uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tunahitaji kuzalisha kwa tija ni lazima Serikali iwekeze kwenye utafiti. Katika eneo hili Serikali bado iko nyuma sana. Tuna vituo vingi sana ambavyo viko hapa nchini ambavyo havijapewa fedha ya kutosha kuweza kuwekeza kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikawekeza huko ili kupata wataalam wa kutosha watakaowasaidia wakulima olo waweze kuzalisha kwa tija sambamba na kuajiri wataalam. Serikali haina wataalam wa kutosha inaoajiri huko vijijini, karibu wananchi wote wanalima kilimo cha mazoea tu ambacho hakina utaalam wowote, kama tukielekeza nguvu zetu huko tutakuwa tumewasaidia.

Mhes

himiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine naomba nizungumzie suala la ushirika. Kwenye ushirika ni vyema tukatoa elimu ya kutosha na Serikali iwekeze fedha za kutosha kwenye kada hii ya Ushirika. Tutailalamikia sana Idara hii kwa sababu haina uwezeshwaji wa kutosha. Idara ya Ushirika haijawezeshwa vya kutosha, lakini katika kila jambo linalojitokeza tunaiona Idara ya Ushirika ni muhimu, *SACCOS* zikifumuka wanahitaji Wanaushirika, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya pili au ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kakoso. Waheshimiwa Wabunge nilisema nitamwita Mheshimiwa Josephat Kandege, lakini simwoni ndani ya ukumbi wa Bunge, kwa hali hiyo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Zarina Madabida.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naanza kwa kusema naunga mkono hoja. Naomba nizungumze mambo mawili tu. Moja liko kwenye ukurasa wa 69 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri, Programu ya Vijana katika kilimo na la pili kuongeza thamani ya mazao hususan usindikaji wa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilianza kuzungumza, lakini muda haukunitosha, naomba nirudie, kwa sababu naamini ni suala muhimu sana kuhusu vijana na ajira. Tunasema kwamba sasa hivi Tanzania vijana ni takribani asilimia 60 ambayo ukiweka katika idadi ya watu walioko sasa hivi, tunazungumzia vijana milioni 24 mpaka 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vijana wengi sana na asilimia kubwa sana ya hao hawana ajira. Sasa nimesoma katika ukurasa wako huo, programu ya vijana katika kilimo. Nawapongeza Wizara angalau kufikiria suala hili. Lakini ukisoma takwimu ambazo wamezitoa hapa sijui 1,000 vikundi vya vijana, vijana 150, vijana 250 ni wachache sana. Tunazungumzia mamilioni ya vijana ambao hawana ajira, lakini huwezi kumwambia kijana aende akajikite kwenye kilimo kisichokuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kisichokuwa na tija ni hiki ambacho sasa hivi tunalima cha jembe la mkono, ambalo huyu kijana umtoe hapa umwambie aende ukampe shamba

alime kwa mkono, hata kama utamkopesha mbegu, lakini mwisho wa siku hatovuna kitu ambacho yeye kitaweza kumpa faraja na kumkidhi mahitaji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa rai na natoa tena rai hiyo kwamba, Serikali ifanye mkakati wa makusudi kama vile mkazo tunavyoutoa kwenye kilimo kwanza, vijana hawa ndio nguvukazi ya Tanzania. Tumewasikiliza hapa Waheshimiwa Wabunge, kama Mbunge wa Ulanga anasema kuna ardhi yenye rutuba iliyozungukwa na mito 17 ambayo wanaweza hata kufanya kilimo cha kumwagilia, wana eka 30,000 lakini zinazotumika ni 1,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini kama kweli Serikali iko *serious* katika kuinua kilimo, lakini vile vile katika kuinua maisha ya vijana na Tanzania kwa ujumla, tusiende kuwasaidia vijana hawa kwa kutayarisha haya mashamba. Tutayarishe mashamba makubwa, tutoe mbegu bora, tutoe mbolea, tutoe dawa na la mwisho kabisa tuwahakikishie masoko ya mazao watakayolima ili kusudi mwisho wa siku vijana wengi waone kwamba kwenda kulima ni tija na si adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vijana wamezagaa mijini wanafanya kazi, mtu siku nzima anatembea na visu mkononi na mikanda anauza, wakati tunaweza kumsaidia na ile mikanda anayouza, visu anavyouza, jeki anazouza sio zake, amepewa na tajiri malikauli akauze, tunapoteza na kodi kwa kupewa yeye malikauli ambayo haina risiti, anapeleka kule anamtajirisha mtu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wakisaidiwa nina hakika kabisa itasaidia. Naiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu, ilichukue hili ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ajira kwa vijana, vijana wawe *involved* katika kilimo, hatuzungumzii vijana 1,000 wala 20,000, tunazungumza mamilioni ya vijana na ardhi tunayo, hilo linawezekana tukiwa tu na utashi wa

Serikali. Kwa hiyo, naomba sana na siishii hapo tu, wakati ule wakati wakisubiri kuvuna Serikali iwasaidie ili kusudi angalau waweze kujikimu mpaka watakapovuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwaambii wawape bure, nasema *cost* zote zile Serikali izichukue, mwisho wa siku wale vijana walipie na kila watakachokilipa kinakuwa kama *revolving fund* ya kwenda kusaidia vijana wengine. Vijana milioni 24 ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiseme hapa, tunasoma kwenye kitabu kwamba tutoe sifa kwa vijana ambao wamesaidiwa 1,000 au 2,000 hapana, ni vijana wengi sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilichukue hilo, iende ikalifanyie kazi kwa dhati kabisa na natoa ushauri huu kwa dhati kabisa, naomba wauchukue, waende wakaufanyie kazi. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Tanzania tumejaliwa tuna matunda ya kila aina na kwanza na-*declare,* mimi ni mkulima wa matunda na hususan maembe. Lakini Tanzania kila tunda linakubali, mananasi yanakubali vizuri sana, machungwa yanakubali vizuri sana, maembe yanakubali vizuri sana na nilifurahi kweli nilipoona kule nyuma ya kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweka mti wa maembe uliozaa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matunda haya kila msimu yanaoza bila kufanyiwa kazi yoyote na hata nyanya zinaoza. Hivi leo kweli umevuna yameoza, kesho utarudi kwenda kulima? Huwezi kurudi kwenda kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, vile viwanda vyote ambavyo vilikuweko vya kusindika matunda viko wapi? Kama vilibinafsishwa, najua sheria inasema kwamba, mtu asibadili matumizi yale aliyochukulia kile kiwanda, sasa viwanda wanavyo akina nani na kwa nini havifanyi kazi ile ambayo ilikuwa imepangwa ifanywe mpaka kiasi kwamba matunda yaharibike bila kutengenezwa katika bidhaa zilizokwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna juisi, vipande na hapo ndio pangeweza kuleta tija ya mtu kuona kwamba aongeze uzalishaji. Unakwenda nchi ya Botswana kinchi kidogodogo tu, uko juu ya anga unaanza kuona bahari ya mananasi, sisi hapa tunashindwa kitu gani? Lakini huyu atalima nanasi lile, *at the end of the day* anakwenda kurundika pale, baada ya siku mbili au tatu unaacha yaozee hapo hapo, hali kadhalika machungwa, maembe na nyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata majibu ya Mheshimiwa Waziri, hivi viwanda vile vilivyokuwa vinatengeneza viko wapi na kama vilibinafsishwa vilikuwa vinatakiwa viendelee na kazi ile ya kusindika. Humu ndani nimeona mmeandika *PPP*, lakini *PPP* mbona tunarudi kinyumenyume, si vilikuweko viko wapi? Kama wamevinunua wanafanya navyo nini? Nataka nipate majibu ya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, hawa Mabwana Shamba na mimi ni mkulima, napenda sana kulima, ndiyo *hobby* yangu na sasa hivi ni mwaka wa ishirini nalima. Ninakolima Mkoa wa Pwani kwa muda wa miaka 20, nimemwona Bwana Shamba mara mbili tu, kwa mtindo huo kweli tutafika?....

*(Hapa kengele ililia kushiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, lakini naomba nipate maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zarina. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nitamwita Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngonyani, na Mheshimiwa Kessy ajiandae.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ili nichangie hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kupitisha bajeti yake ya mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu malalamiko ya wakulima na zao la tumbaku. Nitaelezea kidogo mfumo wa pembejeo na nina ushauri nataka kuipa Serikali. Mfumo wa uagizaji wa mbolea kupitia Vyama vya Ushirika ulioanzishwa mwaka 2009 kwa lengo la kumpa mkulima ahueni na uwezo wa kukopa. Sasa baadhi ya Watendaji na Viongozi wa Vyama vya Ushirika wameugeuza kuwa nyenzo ya kumgandamiza mkulima, tena kwa kasi kubwa na kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na sifa zilizopatikana katika msimu wa kwanza kabisa wa mfumo huu kutumika ambapo wakulima walikopa shilingi bilioni 88 na kuzilipa zote na walipata faida kubwa kabisa, yamefunikwa kabisa kwa mtindo huu ambao unaendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kuagiza pembejeo kwa kuchukua makisio ya wakulima au kwa Vyama vya Msingi na kuyapitisha kwenye Vyama Vikuu ambavyo ni *Union* na kupeleka Chama Kilele halafu kuyakusanya, inaleta mianya ya ubadhirifu mkubwa sana. Mfumo huu unawaumiza sana wakulima kwa kumwongezea gharama zisizo na msingi na za kifasadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara sasa hivi ya kupambana na changamoto zilizopo katika ushirika na sheria yake, nashauri kwa sasa hatua za haraka zichukuliwe:-

Moja, mfumo wa kukusanya mahitaji ya mkulima ya kukopa kupitia *Union* kwenda *Apex* uvunjwe mara moja.

Pili, uwepo mfumo utakaozingatia ufanisi zaidi na kuziba mianya ya ubadhirifu. Pia *Apex* ibaki na jukumu lake

la Kitaifa la kutetea wakulima na kuwakilisha wakulima katika vikao vya Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Tatu, kupitia mfumo huu *Union, Apex* unasababisha ubadhirifu, gharama kubwa kwa mkulima ambazo analazimishwa mkulima kuzilipa. Ushauri wangu mwingine ni kwamba, mikataba yote ya maendeleo kwa Vyama vya Msingi kwa maana ya kujenga maghala, kwa maana ya kujenga mabani na mikopo yote iridhiwe na Mkutano Mkuu wa Vyama vya Msingi wenyewe.

Nne, ushirika wa Tumbaku nchi nzima ukaguliwe sasa hivi na adhabu kali zitolewe ili kutoa mfano. Tukianza na wahalifu waliogundulika kwenye ripoti ya ukaguzi wa awali ya sasa hivi, kwa mfano kule *WETCU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio ushauri wangu kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirudi kwenye kilimo cha mahindi. Mwaka huu mfumo na taratibu na muda wa Serikali kuweka bajeti yake umebadilika. Sasa hivi tumeanza mwezi Aprili, naamini kabisa pia mfumo wa uuzaji wa soko au uanzishaji wa soko la mahindi utaanza mapema. Kwa hiyo, naomba Serikali iwahakikishie wakulima mwezi Julai, mahindi yatanunuliwa. *NFRA* wapate hela yao mapema ili mahindi yanunuliwe mapema ili mkulima asibabaike na soko. Tunaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kubwa malipo ya *District Cess* kutoka Serikalini, tunaomba sana myalipe. Sisi tunadai shilingi milioni 83, lakini mpaka leo hatujalipwa na mwaka jana Wizara ya Kilimo walituahidi wataipa *NFRA* fedha ili itulipe, lakini haijalipa. Sasa sisi tunashindwa kuendesha shughuli zetu za ndani. Tunaomba sana Wizara isimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu na mawazo yangu katika mchango huo yalikuwa ni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba nimwite mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Ngonyani, atafutiwa na Mheshimiwa Keissy.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pia nimpongeze sana Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kunipatia pesa za kuweza kuendeleza Bonde la Mto Mkomazi. Naomba sasa wamalizie ile sehemu iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwa sasa kwamba, wameanzisha miradi mingi sana, lakini miradi hii inakuwa haimaliziki kwa wakati, inakaa juu juu tu. Nitoe mfano, kwenye upande wa skimu kuna hiyo skimu ya Mkomazi, nashukuru Serikali mmeamua kunisaidia, lakini skimu hii ina shida, kuna wakati maji yanakauka. Maji mengi tunategemea kutoka Wilaya ya Same katika Ziwa Kalimawe, lakini kuna wakati maji haya wananchi hawapewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ili isipoteze gharama kubwa sana kuna ule Mto Ruvu ambapo pale Bwiko unakuja moja kwa moja mpaka bonde la Mto Mkomazi, unafika mpaka Kata ya Mazinde inakwenda mpaka kwenye skimu ya Mombo. Wananchi wa bonde lile wangekuwa wamepata maji mengi sana kuliko kutegemea maji kutoka Ziwa Kalimawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri Serikali, badala ya kutumia muda mwingi kupoteza pesa, hizo pesa zingetumika kubomoa eneo lile la Mto Ruvu ambapo ni sehemu kidogo sana, ambapo wananchi walipewa ahadi kwamba kutajengwa bwawa, lakini bwawa hili lilishindaka kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna skimu ambazo Serikali mmezitengeneza, mmetumia muda mwingi sana, kwa

mfano Mazinde pale. *TASAF* wametengeneza mifereji pale, lakini mifereji hiyo haijakaguliwa, imeliwa hela, hakuna chochote cha maana ambacho wananchi wanakiona. Unakwenda mpaka Mswaha kuna mfereji wa skimu ambao umejengwa tayari, lakini leo ni mwaka wa tatu maji hakuna kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda Mafweta kuna mfereji umejengwa na Mbunge aliyenitangulia. Lakini je, wananchi wa Mafweta katika Kata ya Maswaha huu mfereji wao unawasaidia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda katika Kata ya Kwagunda, kuna sehemu kule Lengela Mkokola, kuna skimu ambayo ilikuwa inatengenezwa, watu wamepima vizuri na wakasema hapa panakuwa na skimu. Sasa kuna vitu vingi vinajitokeza kule, sisi Wabunge tukifika kule tunalaumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu katika Jimbo langu hakuna sehemu ambayo wananchi wangu wanaweza wakapata sehemu ya kulima. Sehemu kubwa imetawaliwa na mashamba ya mkonge, hatuukatia mkonge, kwanza tunawashukuru watu wa Katani *Limited* wamefanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia wakulima wadogowadogo, Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo ya mashamba mengine ambayo sasa hivi hayaendelezwi na ninyi wenzetu kila tunapouliza mnasema hati zipo kwa Mheshimiwa Rais na hili leo narudia. Tunajaribu kwamba sasa watu waende kulima kwa kilimo cha umwagiliaji ili wakwepe zile sehemu ambazo hati ziko kwa Rais. Sijui hizi hati kwa Rais zinangoja nini? Miaka yote hati iko kwa Rais, jamani Rais si msikivu, Rais si wa Chama cha Mapinduzi? Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba atusaidie hili suala, linakuwa kero sana kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akitusaidia hili, tutakwenda tukiwa na nguvu. Lakini leo hii kuna mashamba ambayo hayaendelezwi kabisa, ni misitu na wananchi wakienda kulima pale wanakuja wanapokonywa. Wanapopokonywa

wanasema Serikali gani hii? Naamini kabisa Serikali yetu ni sikivu na inafanya kazi kwa matakwa ya wananchi, naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kama kweli wananchi wangu wa Korogwe Vijijini anataka wawe imara na wasiwe ombaomba anisaidie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma Mkoa wa Tanga ulikuwa unaongoza kwa kilimo cha mahindi. Leo hii tunategemea mahindi ya msaada tupewe na Waziri Mkuu, ni vioja! Leo hii chakula cha msaada juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amenipa na bado leo nimekuja kuomba. Nimeomba tena leo anipe mahindi mengi kwa sababu ya wananchi wangu. Lakini siku za nyuma tulikuwa tuna sehemu za kulima. Leo hii mwananchi wa kawaida akienda kulima kwenye maeneo ambapo yako mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi, anakuja kupokonywa na kupanda mtu mwingine? Huu ni ustaarabu kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliunda Tume imekwenda katika Mkoa wa Tanga, imekagua mashamba, tunaomba ile Tume itueleze, ni maeneo gani ambayo wananchi wa Mkoa wa Tanga watapata kwa ajili ya sehemu za kufanya kazi. Lakini tukikaa namna hii tunapendeza tu, wengine tukifika kule ni kazi ya lawama kwamba, mnakwenda kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa nataka nikwambie kitu, lakini nitakwambia baadaye nikifika kwenye hotuba yangu ya mwisho. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye mambo ya pembejeo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nataka aniambie wale wote waliopeleka pembejeo vijijini ambapo pembejeo hizo hazikufanya kazi mnawachukulia hatua gani? Naomba kwenye majumuisho yake anieleze kwa sababu wamepelekewa mbolea, mbolea hiyo wameuziwa kwa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mkulima ambaye hana hata eneo la kulima, amelima nusu heka, heka hiyo

inahitaji apate msaada kutoka Serikalini, anafika pale mbolea anauziwa sh. 80,000/=, wakati hata gunia moja la mahindi hana, ataipata wapi? Naomba pembejeo hizi ambazo zimekwenda Korogwe Vijijini na waliopeleka kule wanajulikana naomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ni msikivu, Naibu wake ni msikivu, Katibu Mkuu wake ni msikivu, hebu lifuatilieni hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msiwaachie wale watu wa Mazinde ambao wamechukua hela za wananchi wakidai wanawatengenezea mifereji na mifereji hiyo mpaka leo hakuna kitu. Leo sisi tunalalamikia mkonge, mkonge wakati kuna mabonde makubwa ambayo kama maji yangekuwa yanatoka vizuri wala nisingekuwa nakuja hapa Bungeni kulalamikia suala la mkonge. Huu mkonge nalalamikia kwa sababu hatuna sehemu ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nataka niwaambie kuna maeneo ya viwanda. Kuna viwanda vingi tu, kulikuwa na Kiwanda cha Matunda pale Korogwe na Mkoa wa Tanga ndiyo tunaoongoza Tanzania hii. Hebu niambie kuna kiwanda gani cha matunda Mkoa wa Tanga? Leo haya tunaambiwa hapa masoko. Tulime sisi Mkoa wa Tanga matunda yakauzwe Kenya au Dar es Salaam wakati pale palikuwa na viwanda na leo hii viwanda vimekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni msikivu, amenisaidia sana kwenye Jimbo langu, hili asilifumbie macho. Lakini sitaacha kumwunga mkonom ninamwunga mkono kwa asilimia mia kwa sababu wanajua kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri ameeleza hapa kuhusu chakula cha msaada. Lakini chakula cha msaada wamenipa tani 310, nashukuru. Je, hizi tani 142 zilizobaki nitazipataje? Naomba nizipate kwa sababu sasa hivi katika Jimbo langu kuna ukame ambao umejitokeza. Nimesema maafa yaliyotokea, nilisema wakati wa kujadili hotuba ya Waziri Mkuu na leo kwa sababu mambo haya yapo kwa Waziri wa Kilimo, ahakikishe wale wananchi wa Magamba, Mombo, Magoma

ambao nyumba zao zilimezwa na matope wanapata chakula cha msaada kwa wingi ili kiwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wanalala nje katika Jimbo langu na naamini kabisa kwamba, unalisikiliza hili. Leo nimeulizwa kule Korogwe kwamba, wewe unazungumzia mambo ya chakula cha msaada, tumemsikia Mheshimiwa Waziri anazungumzia chakula cha msaada na bahati mbaya watendaji wanaopelekewa chakula cha msaada wengi si waaminifu, wanachukua chakula cha msaada kingine wanakificha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna habari ambazo zimekuja na Wizara naomba ifuatilie, kuna magunia mengine yamefishwa. Chakula hicho hicho cha msaada ambacho ninyi Serikali imetupa bure, lakini watendaji wenu kule vijijini wanakuwa hawafuatilii haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri naona anacheka, naomba kwa sababu na yeye alitoka huko, hebu ayafuatilie haya asiyaachie na mkiyaachia nitaleta majina yote hapa Bungeni na nione kama mtawachukulia hatua gani? Siwezi kuja kulalamika hapa na napewa chakula na Waziri Mkuu na yeye mwenyewe ana-*support,* halafu wananchi wangu kule wawe wanapata shida. Hii haiwezekani. Sikuwa Mbunge wa kuja kukaa kutanua, nimekuja kutetea wanyonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa mfereji wa Makorora, mnasema kwamba unachimbwa, naomba mnihakikishie kwamba huu mfereji utachimbwa kwa muda huo. Naamini kabisa kwamba mtafanya kazi vizuri, Makorora kule Magoma ili wananchi wetu wapate msaada mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfereji wa Mkomazi wameniambia kwamba, wanatoa kuanzia mwezi wa Tano mwaka huu, mpaka mwezi wa Tisa uwe umekwisha. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anisaidie sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sana, mashamba yaliyotelekezwa Mkoa wa Tanga, bado napenda kurudia yapo mashamba makubwa, sio kwa upande wa Mkonge tu, kuna maeneo mengine makubwa tu, kuna mashamba ambayo akina Chavda wameyakimbia, kuna mashamba ambayo wananchi sasa wako huko kwa muda wa zaidi ya miaka 20, leo hii mwekezaji anakuja anasema anataka awaondoe. Hii si haki, naomba Waziri wa Kilimo kama anajali basi hakikisha ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mara ya kwanza naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa mara ya kwanza kwa sababu Serikali ilikubali hoja yangu ya kuachia huru wakulima wa Rukwa wauze mahindi bei wanayotaka. Hiyo naishukuru sana Serikali ilisikia. Lakini kesho kutwa anapokwenda Dar es Salaam, huyu Mkurugenzi wa Hifadhi ya Taifa, aandike hundi kwa Mkurugenzi wa Namanyere ya shilingi milioni 340/= tunazodai kwa ajili ya ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamesema hapa, vyakula vilikwenda, mahindi wanagawiwa bure tu, lakini vyote vilitoka Nkasi. Kwa hiyo, nataka nikifika Dar es Salaam nikute hundi imeshakwenda kwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya Nkasi ya sh. 340,000,000/=. Sisi Wilaya yetu maskini, tunalima kwa tabu na mkichelewa tu naongeza riba pale pale hakuna msalie Mtume. Tunaelewana Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena namsifu sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo katika Wizara ambayo kuna Waziri ukimpigia simu hata saa sita usiku, Waziri na Naibu Waziri

wa Kilimo wanapokea simu mara moja. Hii sipendelei naeleza ukweli na Mawaziri wengine igeni tabia ya Waziri na Naibu Waziri wa Kilimo, wanakuwa wasikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwingine ukimpigia simu hana habari, hapokei kabisa. Sijui anadhani mimi mpiga kura anaomba hela? Sielewi! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu skimu za umwagiliaji; tuna skimu za Katongoro, skimu ya Malieza kule Rukwa, walitenga tangu mwaka 2010/2011 na skimu ya Rwanfi walitenga shilingi milioni 531/- mwaka jana hazikupelekwa na mwaka huu hakuna. Vibanio vya Sakalilo na miundombinu ya Sakalilo milioni 354.5/= mwaka jana hazikwenda na mwaka huu kwenye kitabu sikuziona. Sasa Mheshimiwa Waziri wananchi kule watalimaje mpunga. Tuendelee kuagiza mpunga wa Thailand, tuzidi kuwatajirisha Wahindi wa Pakistan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimepiga simu kule Rukwa upande wa Mpanda, wananchi sikilizeni gunia la mpunga shilingi 18,000/- na nyie mmeagiza michele mibovu, wakulima wetu watauzaje? Kilando 30,000/=, Sumbawanga 30,000/= debe saba, nataka Hifadhi ya Taifa mwaka huu kununua mpunga kama zao la dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi watapeleka wapi mpunga? Bado Mkoa wa Mbeya hatujui kiasi gani cha mpunga walichonacho kwenye maghala yao. Kwa hiyo mnunue mpunga mjue kwa kuupeleka, kama Pakistan, kama Thailand mpeleke wenyewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea; ndugu zangu tunalaumu Serikali ya CCM. Wanapoajiriwa watumishi wa Serikali sio kama zamani, unaambiwa onesha kadi ya CCM, wanaajiriwa kutokana na *CV* zao humuo humu kuna Vyama Vingi na wengine wanahujumu CCM. Huu ni ushauri wa bure kuanzia sasa mambo ya mbolea ya ruzuku yafutwe. Zile pesa ziingizeni kwenye mbolea, bei ishuke kila mtu apate.

Hakuna msalie Mtume, hakuna mtu mwaminifu, kila mtu ukimpa hiyo kazi, ikiwa Benki au nane tumbo lake liko mbele. Hakuna mwenye tumbo nyuma hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwajui wanatupiga vita hao hao watu wa humo ndani ndiyo wabaya kwa CCM. Nyie mnakaa mnapeleka mbolea, wanapata ruzuku wanajenga majumba, wanajenga maghorofa kwenye ruzuku za mbolea. Futeni wazo la ruzuku punguzeni bei ya mbolea kila mtu apate. Kwanza ni lawama wanapata wachache, kwa mfano, Nkasi wako wakulima 3000 mnapeleka mbolea ya watu 20 wengine waende wapi? Sio Watanzania hao? Futeni mambo ya ruzuku, hakuna cha benki hakuna cha nini, Benki kwenyewe wizi mtupu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbolea Minjingu Sumbawanga, huyu Minjingu ni nani? Kwa nini Serikali inamlea na kumbeba huyu Minjingu. Kuna tani 1,000 Sumbawanga, Serikali imeingia gharama leo miaka mitatu. Huku wanadai hela za *godown* na mbolea imekaa pale miaka mitatu, akaichukue mbolea yake Sumbawanga hatuitaki kabisa ile mbolea imekaa miaka mitatu. Wakasema wanaongeza tani nyingine, wanaendea kuchakachua lakini tani 1000 zipo Sumbawanga, imekaa kwenye ma-*godown*. Mwenye *godown* anadai kodi kila mwezi. Vimbolea haviuziki, vimekaa palepale, kavichukueni vimbolea, Minjingu ni nani huyu? Ameitia Serikali mfukoni? Nawaleteeni moja baada ya moja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia *standard* ya kilimo. Nilizungumza hata wakati wa bajeti ya Waziri Mkuu, tujue idadi ya *power tiller* zilizoingia, gharama yake na tukipiga hesabu ongezeko la chakula nchini. Kama kweli kuna ongezeko mbona mmeagiza mchele nje na *power tillers* na matrekta mnayo? Hii imekuwa ni dampo, chuma chakavu kutuletea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waagize matrekta ambayo yamelima nchi nyingine yamefanyiwa majaribio, wawezesheni wakulima, kule Kabwe Korongwe, kuna bonde

kubwa. Mheshimiwa Waziri atume watu wake wakaangalie, apeleke skimu ya umwagiliaji. Kuna Kijiji cha Korongwe, Penge na Utinta watalima mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tujengewe *godown* Namanyere, Mtenga hakuna *godown*, Swahila hakuna *godown*. Mtu analima gunia 300 hadi 400, nyumba yake ya chumba kimoja cha mita kumi kwa mita kumi, ataweka wapi mahindi? Yataharibikia mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake aweze kujenga *godown* Swahila, kuongeza *godown* Namanyere Mjini na Mtenga. Wanalima mazao ya kutosha hakuna pa kuhifadhi. Mtu ana chumba kimoja mita nne kwa mita nne unataka mazao yake apeleke wapi? Mazao anatakiwa auze au aweke kwenye *godown* la Serikali, kwa sababu la kwake ikija mvua maturubai hakuna mahindi, yanalowana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi naomba hayo uyaekeleze, mambo ya ruzuku ya mbolea yafutiliwe mbali, ipunguzwe bei ya mbolea ili kila mtu aweze kununua. Hela ambazo hawakutenga kwa Lwanfi na skimu ya kule Isakalilo zipelekwe haraka ili wananchi wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki wananchi wa Rukwa waje Dar es Salaam waanze kuuza vichupi na sidiria. Nyie mnataka kila mwananchi awe Machinga? Wawekeeni miundombinu wananchi wetu wapate kulima, wapate pesa. Nilizungumza hata kwenye bajeti ya Waziri Mkuu, hakuna kijana wa Mkoa wa Rukwa anakuwa Mmachinga Dar es Salaam, wote ni kutoka Kusini.

**WABUNGE FULANI:** Aaahh!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono moja kwa mara ya kwanza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy kwa kweli ametusaidia sana kutunza muda na amempa nafasi Mheshimiwa Obama ambaye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Yangu yatakuwa machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, aangalie zao la kahawa. Kule kwangu ni wakulima wa kahawa na tuna matatizo matatu. La kwanza, bei ya kahawa kwa mwaka huu imeshuka sana na wananchi wamenituma kwamba, aangalie namna ya kufanya ili bei yao iweze kurudi kwenye sh. 8,000/= kwa sababu sasa hivi ni sh. 4,000/= kwa kilo moja. Kwa hiyo, hilo ni ombi lao la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili wameomba ofisi ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo iwasaidie fedha za maghala. Kahawa inayozalishwa ni nyingi, lakini sehemu ya kuhifadhi wanapata shida. Kwa hiyo, naomba nalo hilo liwekee kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu ni wizi, watu wanaokwenda kuwaibia wakulima wa kahawa. Wameshakopwa hela zao nyingi zaidi ya milioni 300/= ziko kwa makampuni ambayo yamechukua hiyo kahawa, lakini miaka miwili sasa wakulima wale hawajapata zile fedha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na hili ana taarifa nalo, kwa kweli atusaidie namna ya ku-*recover*. Ile *price stability* ninayoifikiria sisi itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri ameonesha masoko, tuna soko la Mnanila pale kwa ajili ya kuhifadhi mazao, umesema ukarabati; wahandisi wameshafanya *feasibility* study, wamemaliza. Nataka kujua hilo soko linaanza lini kwa sababu sasa ni miaka miwili na nusu tunaliongelea, lakini bado halijatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la wataalam. Wataalam wa kilimo kwenye Wilaya yangu tunao watano ambao hawatoshi, naomba kwenye huu mgao ambao mnataka kugawa Jimbo langu na Wilaya yangu mpya ya Buhigwe Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, wazo la Mheshimiwa Waziri kwamba, vijana waweze kusaidiwa kwenye kilimo ni wazo zuri, naomba sasa idadi kama wengine walivyosema kuwa, unaandika kwenye hotuba kwamba kuna vikundi vya watu wawili au watatu, nafikiri sio idadi, tutashindwa kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo kama wenzetu wanavyosema, inaleta ugomvi ndani ya vijiji na maeneo yetu. Serikali ikae chini iliangalie kwa kina. Mbolea inayoletwa ni kidogo na wakulima ni wengi. Kwa hiyo, tungeomba kabisa aidha, itolewe ruzuku kwenye bei, mwache soko liendelee kuliko kuja kuwapa watu wachache, itatuletea ugomvi na wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupoteza muda, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana. Nafikiri kwa orodha tuliyonayo leo tuhitimishe shughuli hizi sasa. Tutaendelea na utaratibu wa hoja hii siku ya kesho na tutaihitimisha hoja hii siku ya kesho.

Kwa hiyo, baada ya kusema maneno hayo mafupi, naomba niahirishe shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

*(Saa 1.43 Usiku, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 23 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*